**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Tatu - Tarehe 30 Machi, 2006**

(*Mkutano Ulianza Saa Saa Tatu Asubuhi*)

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge napenda kuwatambua Madiwani wa Halmashauri ya Moshi Vijijini. Jimbo la Vunjo na Jimbo la Moshi Vijijini. (*Makofi*)

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU k.n.y WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:-**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni *BRELA* kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2004. *(The Annual Report and Audited Accounts of the Business Registrations and Licensing Agency for the year ended 30th June, 2006)*

**MASWALI NA MAJIBU**

**Na. 30**

**MHE. SALIM H. KHAMIS (k.n.y. MHE. MOHAMED ALI SAID)** aliuliza:-

Kwa kuwa, vijana ndiyo nguvu kazi ya Taifa letu lakini vijana wengi sasa hivi wameathirika na wanaendelea kuathirika kutokana na kutumia dawa za kulevya; na kwa kuwa, kuna wafanyabiashara maalum wanaoleta dawa hizo hapa nchini:-

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani za kuwadhibiti wafanyabiashara hao ili wasiendelee kuleta dawa hizo hatari kwa vijana wetu hapa nchini?

(b) Je, kuna wafanyabiashara wangapi hadi sasa ambao wamewahi kukamatwa kwa kuhusika na usafirishaji wa dawa za kulevya na wamechukuliwa hatua gani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI (MHE. DR. LUKA J. SIYAME)** alijibu:

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Ali Said, Mbunge wa Mgogoni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli baadhi ya vijana wetu wameathirika na wengine wanaendelea kuathirika kutokana na kutumia dawa za kulevya. Hili ni tatizo kubwa kwa jami yetu na kwa kutambua hivyo, Serikali imechukua na inaendelea kuchukua hatua mbalimbali kukabiliana nalo. Zifuatazo ni baadhi ya hatua hizo kama ifuatavyo:-

(i) Mwaka 1991, Serikali ilianzisha kitengo cha kuzuia dawa za kulevya cha Jeshi la Polisi kwa mtizamo wa kudhibiti matumizi na kuzuia uingizwaji na na usafirishaji wa dawa hizo.

(ii) Mwaka 1995, Bunge lilipitisha Sheria ya Nchi ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya Na. 9 (*The Drugs and Prevention of Illicit Traffic in Drugs Act, 1995*). Sheria hiyo iliunganisha Sheria mbalimbali za kudhibiti dawa za kulevya kuwa moja ili kuongeza ufanisi. Aidha, sheria hiyo ilianzisha chombo cha kuratibu udhibiti wa dawa hizo ambacho kinaelekeza, kuhamasisha na kuratibu Sera ya Serikali ya Udhibiti wa dawa za kulevya.

(iii) Serikali imejitahidi kueleimisha na kuhamasisha jamii kwenye ngazi ya kijiji na kata katika baadhi ya Wilaya ili wananchi washiriki kikamilifu katika kubaini na kuteketeza zao la bangi. Wilaya tisa za Hanang, Babati, Simanjiro, Moshi Mjini na Vijijini, Lushoto, Tarime, Same na Korogwe zilihusishwa. Matokeo ya jitihada hizi ni nchi yetu kuwa miongoni mwa nchi tatu za Afrika zilizobaini na kuharibu kwa wingi zao la bangi kati ya mwaka 2003 na 2004.

(iv) Serikali imeridhia mikataba yote ya Kimataifa inayohusu udhibiti wa dawa za kulevya.

(v) Serikali imeweka utaratibu wa mafunzo kila mwaka kwa wataalamu wake kuweza kudhibiti dawa za kulevya. Wataalamu hao wanatoka Jeshi la Polisi, Shirika la Posta, Idara ya Uhamiaji na Idara ya Ushuru wa Forodha. Aidha, zaidi ya maafisa 70 katika mipaka tisa ya nchi yetu, viwanja vya ndege vitatu na bandari za Dar es Salaam na Zanzibar nao wamepatiwa mafunzo hayo.

(vi) Serikali imepeleka mipakani vifaa na vitendea kazi muhimu kwa lengo la kuimarisha udhibiti na kutambua wahalifu. Hivi ni pamoja na Pikipiki 9, *Radio Calls 3*, magari na kompyuta pia mbwa wa kunusa dawa hizo na vifaa vya kutokea dawa (*drug loo*) vimewekwa katika uwanja wa ndege wa Dar es Salaam.

(b) Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha mwaka 2000 hadi 2004 waliotuhumiwa kujihusisha na dawa za kulevya ni 27,555. Jumla ya kesi 20,514 zilifunguliwa mahakamani kuhusiana na biashara, matumizi au kulima mazao ambayo ni jamii ya madawa ya kulevya. Kati ya hizo, kesi 17,981 sawa na asilimia 88 zilikuwa ni za bangi. Kesi 1,203 sawa na asilimia 6 zilikuwa ni za mirungi, kesi 1,044 sawa na asilimia 5 zilikuwa za *Heroin* na jumla ya kesi 286 sawa na asilimia moja (1%) zilikuwa za bangi iliyosindikwa, *cocaine*, *mandrax* na *morphine*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia takwimu nilizotoa, kwa kweli mtakubalana nami kuwa tatizo la biashara ya matumizi ya dawa za kulevya za kiasili kama bangi au zile zinazotoka nje ya nchi kama vile *heroin* na *cocaine* ni kubwa katika jamii yetu na hivyo jitihada za pamoja zinahitajika kulikabili.

Kwa maana hiyo, napenda kutoa wito kwa wananchi wote kushirikiana na Vyombo vya Ulinzi na Usalama kwa kuwafichua wale wote wanaojihusisha na biashara hiyo haramu ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa mara moja dhidi yao. Napenda kuwahakikishia kuwa, Serikali itawalinda wale wote watakaosaidia kufichua wahalifu hao.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu nina swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, inaonekana hawa watumiaji wa madawa ya kulevya wakiisha tumia ni rahisi sana kuwagundua hata kuwajua mitaani tu hivi, je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuweza kuwafuatilia vijana hawa kuwakamata na kuwaweka kwenye vituo maalumu vya kuwatibu na kuwapa ushauri nasaha ili wasiendelee kuathirika kwa sababu kila leo Taifa linaonekana linaanza kupata hasara kwa vijana hawa kupata ugonjwa huo ambao mwisho unawapelekea na kupata ugonjwa wa akili?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI (MHE. DR. LUKA J. SIYAME):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mpaka hivi sasa Serikali inavyo vituo ambavyo inavitumia kwa ajili ya kutoa ushauri nasaha kwani vijana wote wanaojihusisha na madawa ya kulevya ambao wao kwa hiari yao wamekiri kwamba hapo nyuma wamekuwa wakitumia hayo madawa ya kulevya ama kwa wakati huo wanatumia hayo madawa ya kulevya na wanataka kuachana nayo.

Naamini kabisa kwa ukubwa wa nchi yetu ni vigumu kwa Serikali kuweza peke yake bila ushirikiano wa wananchi kudhibiti matumizi ya dawa za kulevya na hivyo narudia tena kutoa ushuri na wito kwamba kila mwananchi ajihusishe katika kuhakikisha anatoa *report* juu ya matumizi ya madawa ya kulevya.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa wanaowajua wauzaji au wanaoshughulikia na biashara ya madawa ya kulevya ni mateja, wale wavutaji na kwa kuwa wavutaji wakiondoka katika *withdraw syndrome* ambayo Wizara ya Afya kupitia Muhimbili na Kitengo cha Hospitali hapa Mirembe wanaweza kazi hiyo.

Je, Serikali haionekani sasa ni wakati muafaka tuombe kila Wilaya katika Hospitali zao kuwe na kitengo kinachofanana na Mirembe ili hao wateja wakishaondokana wao watawaambia nani wanawauzia?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI (MHE. DR. LUKA J. SIYAME):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Dr. Zainab Amir Gama katika swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Hospitali alizozitaja zina wataalam wa magonjwa ya akili na utumiaji wa madawa ya kulevya unaangukia katika kundi la magonjwa ya akili. Kwa hiyo, naamini inahitaji tuwe na wataalam kila Wilaya wa magonjwa ya akili.

Sasa mpaka sasa tunao wachache na wanapatikana sehemu chache za hospitali za Rufaa mbalimbali nchini na Hospitali maalum ya Mirembe hivyo itakuwa vigumu kwa wakati huu kumhakikishia kwamba kila Hospitali ya Wilaya inakuwa na wataalam wa aina hiyo wa kushughulikia hayo madawa ya kulevya.

**Na. 31**

**Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo**

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wabunge ni mawakala wa maendeleo katika maeneo yao ya uchaguzi na hii imethibitika wazi pale ambapo kila jambo linalofanyika Jimboni lazima Mbunge ahusike na wakati mwingine hulazimika kutumia fedha zake za mfukoni kwa matatizo mbalimbali ya shughuli za maendeleo na wananchi wake:-

Je, isingekuwa vyema sasa Serikali ikaleta Bungeni Muswada wa kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kwa Wabunge wote ili kuleta usawa na kuimarisha maendeleo katika nchi kama Mabunge mengine kama Kenya, Ghana na Uganda yanavyofanya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI (MHE. DR. LUKA J. SIYAME)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Waheshimiwa Wabunge ni mawakala na hali kadhalika ni wadau wa maendeleo katika maeneo yao ya uchaguzi. Aidha, serikali inakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa kutokana na hamasa, kuna wakati Wabunge hulazimika kutumia fedha zao binafsi kwa matatizo mbalimbali ya shughuli za maendeleo ya wananchi wao na kitaifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa utaratibu mzima wa kuandaa mipango ya maendeleo na usimamizi hapa nchini, Serikali imekubali inatekeleza jukumu hilo kwa kuhakikisha kuwa wananchi wengi walioko ngazi ya kijiji hadi Wilaya wanashirikishwa. Ushirikishwaji huo wa wananchi katika kujiletea maendeleo hutekelezwa hivyo kwa lengo la kubainisha wadau na mchango wao katika kufanikisha mpango mzima. Aidha, katika mipango mingi ya maendeleo ya wananchi kumekuwa na upungufu wa rasilimali kutokana na uwezo mdogo wa Serikali kuweza kukidhi mahitaji ya mipango yote nchini. Hivyo basi, Serikali kwa kutambua hilo, imekuwa inawashirikisha Viongozi mbalimbali na wadau wengine wa maendeleo kutoa michango ya hiari ili kuendeleza juhudi zilizokwishaanzishwa na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu maalum unaotumiwa na viongozi Wakuu akiwemo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu kuchangia maendeleo ya wananchi kila inapobidi una sura ya kitaifa.

Utaratibu huo ulibuniwa kwa Viongozi hao wachache ili kuhamasisha wananchi waweze kubuni, kupanga na kutekeleza mipango yao ya maendeleo kwa kutegemea rasilimali walizonazo. Michango inayotolewa na Viongozi hao inakuwa ni kuunga mkono na kuongezea pale nguvu za wananchi zilipokomea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa imedhihirika kwamba mara nyingi fedha zinazotengwa kwa mipango mbalimbali ya maendeleo katika Wilaya na Halmashauri zimekuwa hazitoshelezi kutokana na ufinyu wa bajeti, kuwa na mfuko wa maendeleo ya

jimbo kwa Wabunge ni hatua muhimu itakayowawezesha Wabunge kuhamasisha zaidi maendeleo katika maeneo wanayoyahudumia.

Hivyo, kwa misingi hiyo, Serikali inapenda kumshauri Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba kuliwasilisha suala hili kwenye Ofisi ya Spika, ili kwa kuzingatia Kanuni na taratibu za Bunge letu Tukufu, liweze kujadiliwa na hatimaye kuwasilishwa rasmi Serikalini na kuweza kufanyiwa kazi.(*Makofi*)

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Ahsante kwa kiniruhusu niulize swali la nyongeza.

Nashukuru sana kwa majibu mazuri aliyonipa yenye matumaini kwa kuwa yeye ni Mbunge na Mheshimiwa Waziri Mkuu ni Mbunge nina imani kwamba watanisaidia. Je, wako tayari kuungana nami katika kulisukuma kwa Spika liende haraka?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri naona wanashukuru kwamba umeelewa basi Mheshimiwa Dr. Mzindakaya swali la nyongeza.

**MHE. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Spika wa Bunge la Kenya alipokuja hapa kwenye Semina ya Bunge hili, alieleza kwamba wao utaratibu huu ulishaanza wa kutoa fedha kwa ajili ya kusaidia Wabunge kutoa pesa kwa ajili ya miradi hii kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Mbunge; na tulipokuwa Kenya tuliambiwa kwamba wao kiwango cha chini kabisa ni milioni 200 kwa Jimbo kinafika mpaka milioni 300.

Sasa swali langu ni kwamba je, Waziri atakutali kwamba ni vizuri utaratibu huu uanze na sisi katika Bunge hili mwaka huu wa fedha?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI (MHE. DR. LUKA J. SIYAME):** Mheshimiwa Naibu Spika, katika jibu langu la swali la Msingi nilisema kwamba namshauri Mheshimiwa Mbunge awasilishe hoja yake kwa Ofisi ya Spika ili liweze kujadiliwa na kufanyiwa kazi na baada ya hapo basi hatua zinazostahili zitachukuliwa. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Swali ni kuomba *constituency alloncе*, nadhani ya nyongeza hayapo. Swali linalofuata Mheshimiwa Riziki Saidi Lulida.

**Na. 32**

**Halmashauri ya Mji wa Lindi Kufanywa Manispaa**

**MHE. RIZIKI SAID LULIDA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali haijaibadilisha Halmashauri ya Mji wa Lindi kuwa Manispaa licha ya jitihada zilizofanywa na uongozi wa Mkoa wa Lindi na Halmashauri ya Mji wa Lindi za kukamilisha vigezo vyote vunavyotakiwa kwa Mji kuwa Manispaa; na kwa

kuwa, mji wa Lindi ulikuwa Makao Makuu ya *South Province* iliyojumuisha mikoa ya Mtwara, Ruvuma na Njombe lakini kwa sasa hivi Mtwara na Songea ni Manispaa, bado tu Mji wa Lindi:-

(a) Je, ni lini Mji wa Lindi utapata hadhi ya Manispaa?

(b) Je, vigezo vinavyotumika havitoshelezi kuipa Halmashauri ya Mji wa Lindi haki ya kuwa Manispaa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. CELINA OMPESHI KOMBANI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Riziki Saidi Lulida, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 5 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Na. 8 ya mwaka 1982, Waziri mwenye Dhamana ya Serikali za Mitaa ndiye mwenye Mamlaka ya kuanzisha Mamlaka ya Manispaa baada ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa husika kutimiza vigezo vilivyowekwa. Vigezo vinavyotumika na ambavyo vinazingatia Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, vipo vigezo ambavyo Mji wa Lindi unaweza ukavitimiza. Suala la Msingi ni kwamba huangalii kigezo kimoja pekee katika kutoa hadhi bali vinaangaliwa kwa pamoja. Takwimu na taarifa zilizopo zinaonyesha kuwa Halmashauri ya Mji wa Lindi haijatimiza baadhi ya vigezo vinavyotumika. Vigezo hivyo ni pamoja na :-

(i) Idadi ya wakazi. Kwa mujibu wa Sensa ya Kitaifa ya Idadi ya Watu ya mwaka 2002, Mji wa Lindi ulikuwa na wakazi wapatao 41,549, hiyo ni asilimia 41 ya idadi ya watu wanaotakiwa.

(ii) Uwezo mdogo wa kijiendesha. Kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2000 hadi mwaka 2005, Halmashauri ya Mji wa Lindi ilikuwa inakusanya mapato kwa wastani wa shilingi 109.6 kwa mwaka. Mapato hayo yaliyokusanywa yanatosheleza asilimia 40 tu ya mahitaji ya utoaji wa huduma pamoja na uendeshwaji wa shughuli zake. Halmashauri ya Mji wa Lindi inategemea ruzuku kutoka Serikali Kuu kwa asilimia 80.

(iii) Kutoendelea kujengeka au kukua kwa Mji. Hali ya ujenzi wa nyumba katika Mji wa Lindi pamoja na huduma nyingine ni wa chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kusisitiza Mheshimiwa Lulida kuwa Mji wa Lindi utapata hadhi ya kuwa Manispaa baada ya vigezo hivyo kutimizwa. Aidha, napenda kutoa wito kwa Uongozi wa Halmashauri ya Mji wa Lindi uwahamasishe Wananchi wa Mji huo ili waendeleze Mji wao pindi vigezo hivyo vitakapotimizwa Mji wa Lindi utabadilishwa kuwa Manispaa.

**MHE. RIZIKI SAID LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja majibu mazuri ya Naibu Waziri napenda kuongeza swali dogo la nyongeza.

Kama kigezo kimojawapo ni idadi ya watu kwa nini eneo la Lindi Mjini lisiongezewe vijiji vifuatavyo:-

Mingoyo, Kikwetu, Mbanja, Chikonji na Mkupama?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lulida, kama ifuatavyo:-

Mwenyewe ameshasema kwamba hivyo ni vijiji, katika manispaa kuna mitaa na siyo vijiji kwa hiyo hilo naona halitawezekana.

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona.

Kwa kuwa wananchi wa Mji wa Lindi tokea mji huo ukiwa Makao Makuu ya *Southern Province* wamekuwa wakijitahidi kuendeleza vigezo vilivyotajwa na Mheshimiwa Naibu Waziri mpaka pale Serikali ilipoamua kukandamiza juhudi hizo kwa kuhamisha Makao Makuu kwenda Mtwara, kwa kuhamisha Bandari kwenda Mtwara, kwa kuhamisha Uwanja wa Ndege kwenda Mtwara. Je, hivi sasa Serikali kwa kuwa ina nia njema ya kuukuza Mji wa Lindi kufikia kiwango chaManispaa watakuwa tayari kurejesha huduma hizo muhimu katika mji wa Lindi ili kukua kwa watu kuongezeke? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mudhihir kama ifuatavyo:-

Maamuzi ya kuhamisha baadhi ya huduma zilizokuwa katika mji wa Lindi kwenda Mtwara yalikuwa ni maamuzi ya Serikali na yalikuwa halali kabisa na yalizingatia vigezo ambavyo vilionekana vinajidhihirisha.

Kwa sasa hatuwezi kwa kweli kugeuka tena tukasema turudishe hizo huduma kwa sababu huko ziliko nako zinafanya kazi nzuri. Cha Msingi tunamwomba tu Mheshimiwa Mudhihir, Mbunge wa Mkoa huo wa Lindi wafanye haya ambayo tunawaomba wayafanye sasa ni kweli mengine ni magumu lakini wakijitahidi angalau katika maeneo yale mengine ya Msingi ambayo tumeyataja tunaweza tukafikiria kupandisha hadhi ya mji wa Lindi kuwa Manispaa. (*Makofi*)

Na. 33

**Uharibifu wa Mazingira Nchini**

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, suala la uharibifu wa mazingira nchini limekithiri, hali inayopelekea nchi yetu kuwa jangwa kama hatua za haraka hazitachulikuwa; na kwa kuwa uharibufu mkubwa umesababishwa na uvunaji wa magogo na mbao unaofanywa na wafanyabiashara wakubwa kjtoka Dar es Salaam na maeneo mengine ambayo hawana uchungui na Maliasili hizo.

(a) Je, Serikali haioni kwamba kuendelea kutoa vibali kwa wafanyabiashara hao ni kuchangia moja kwa moja uharibifu wa mazingira yanchi yetu hasa baada ya kuona athari za uharibifu huo?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani kwa watumishi wake wanaoshiriki na kuchangia kwa kasi kabisa uvunaji wa misitu katika kujinufaisha wenyewe wakati wamepewa jukumu la kulinda na kuhifadhi misitu hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mbunge wa Viti Maalum, naomba kutoa maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba zipo sababu nyingine zinazosababisha uharibifu wa mazingira, nakubaliana na Mheshimiwa Sakaya, kwama uvunaji wa magogo unaofanywa na wavunaji wakubwa kutoka maeneo mbalimbali nchini likiwemo Jiji la Dar sa Salaam, unachangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa mazingira ya nchi yetu.

Aidha, imebainika kwaba baada ya ufunguzi wa Daraja la Mkapa, kumekuwa na wimbi kubwa la uvunaji wa misitu kwenye maeneo ya furjifi. Pia Serikali imetambua ya kwamba kuongezeka kwa biashara ya magogo nje ya nchi ndiyo chanzo na kichocheo kikubwa cha uharibifu wa mazingira.

Baada ya maelezo hayo mafupi kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Bunge limepitisha Sheria ya Misitu Na. 14 ya mwaka 2002 inayohusu masuala yote ya usimamizi wa misitu nchini. Aidha kwa mujibu wa Kanuni Na. 50 kanuni ndogo Na (1) ya Kanuni za Misitu zilizopitishwa mwaka 2004 na kuanza kufanya kazi tangu tarehe mosi Julai 2004 kwa mujibu wa tangazo la Serikali Na. 160 la tarehe 28 Mei 2004, Kanuni hizo zimepiga marufuku kusafirisha magogo nje ya nchi. Hii ni hatua mojawapo ya kupunguza kasi ya uharibifu wa mazingira hapa nchini.

Aidha, Bunge limepitisha Sheria Na. 20 ya mwaka 2004 inayotoa msukumu mpya katika usimamizi wa mazingira nchini. Pia serikal kwa kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii, imeandaa mwongozi mpya unaoainisha uvunaji endelevu wa miti.

Vilevile elimu ya matumizi endelevu ya mazao ya misitu na utunzaji wa mazingirta inatolewa kwa wananchi kwa njia mbalimbali kama vile mikutano, mafunzo ya ana kwa ana, majarida, vipeperushi, redio na televisheni ili wananchi washiriki kikamilifu katika kulinda raslimali hii muhimu.

(b) Itakumbukwa kwamba mwaka 2004 na 2005 Serikali iliwachukulia hatua za kinidhamu watumishi mbalimbali wa Wizara ya Maliasili na Utalii waliohusika na uvunaji holela wa misitu nchini. Serikali itaendelea kuwachukulia hatua za kinidhamu watumishi wanaovunja Sheria, kanuni na taratibu za nchi kuhusu uvunaji wa misitu kwa kujinufaisha wenyewe.

Ningependa nikuombeni Waheshimiwa Wabunge kuwahamasisha wananchi kuwafichua wale wote wanaohujumu misitu nchini.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri, pamoja na majibu hayo mazuri naomba nimuulize swali dogo.

Kwa kuwa, usimamizi wa misitu hasa kwa maeneo ya vijijini yanasimamiwa na maafisa misitu wa kata na tarafa, na kwa kuwa watumishi hawa wanasimamiwa na

Halmashauri na imedhihirika kabisa kwamba Halmashauri kidogo wako dhaifu katika kusimamia hawa watumishi wao.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka *direct link* ya kuweka mahusiano ya moja kwa moja kati ya watumishi hao na Serikali ili waweze kuwadhibiti katika usimamizi wa misitu hiyo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Madgalena Sakaya, kama ifuatavyo:-

Ni kweli baadhi ya matatizo kama jibu la Msingi lilivyotolewa kwamba linasababishwa na baadhi ya watendaji na watendaji hawa ni kweli wako kwenye mamlaka mbalimbali ikiwemo na mamlaka ya Halmashauri na ndiyo sababu Serikali sasa hivi inazingatia kwamba sheria na taratibu zote zinafuatwa na watendaji wa ngazi zote.

Kwa hiyo, hatua ambazo tumezieleza zitaendelea kuchukuliwa kwa wale wote wanaovunja sheria kwa vile sheria inakata kila sehemu siyo kwamba inawalinda wafanyakazi.

Kwa hiyo, tunazidi kusisitiza kwamba tutaendelea kuchukua hatua kali kwa wafanyakazi wote ambao hawasimamii sheria na kanuni zilizowekwa na nchi hii.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Serikali imekataza au imezuia vibali vya kukata na kusafirisha magogo, lakini bado inatoa vibali kwa wawekezaji ambao wanakuja kukata magogo katika nchi hii na kuwekeza katika misitu yetu. Je, Serikali inasemaje kuhusu hawa wawekezaji?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, siyo kweli kwamba vibali vinatolewa kwa Wawekezaji. Kuna baadhi ya mazao ya misitu ambao tunayaona *especially* hii ya njia ya kutokea Morogoro kwenda Dar es Salaam ambayo inahusisha mazao ya miti ya mitiki ambayo inatoka kwenye shamba la Serikali. Mpaka leo tunaruhusu mahali ambapo uvunaji unahusisha mashamba ya watu binafsi au ya Serikali ya kupanda. Katazo lililowekwa ni kwa misitu ya asili na magogo ya kutoka misitu ya asili ndiyo hatutaki mtu yeyote yule ayavune kwa ajili ya kusafirisha nje ya nchi. Ila tunaruhusu uvunaji ambao unazingatia kwamba mbao zake au mazao yake yatauzwa hapa hapa nchini. Kwa hiyo, si sahihi kwamba tunaruhusu kwa kutumia vibali maalum.

**Na. 34**

**Vifaa Vilivvyotengenezwa kwa Plastiki**

**MHE. WILLIAM H. SHELUKINDO** aliuliza:-

Kwa kuwa imedhihirka waziwazi kwamba, vifaa vilivyotengenezwa kwa plastiki vikiwemo viti, meza, vikombe, sahani, ndoo na kadhalika baada ya kuchakaa vinatupwa ovyo na kuwa chanzo cha uchafuzi wa mazingira ikiwemo mifuko ya Rambo ambayo inaonekana kuzagaa nchi nzima.

(a) Je, Serikali inafahamu kwamba Shirika la *Tanzania Industrial Research Development (TIRDO*) limebuni mashine ya kuchakata vifaa vya plastiki ili kutengeneza vifaa vingine kama mabomba ya maji taka na kadhalika?

(b) Je, Serikali imesaidiaje *TIRDO* katika juhudi zake hizo kwa lengo la kupunguza kero ya uagizaji wa vifaa vya plastiki?

(c) Je, Serikali itakubali kuwasaidia Wamachinga wawe wakala wa *TIRDO* wa kukusanya vifaa chakavu vya plastiki na kuviuza kwenye Shirika hilo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO k.n.y WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, napenda kujibu swali la Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inafahamu kuwa Shirika la Kuendeleza Utafiti wa Viwanda (*Tanzania Industrial Research Development Organization)* lina mashine ya kuchakata vifaa chakavu na taka za plastiki ili kutengeneza malighafi ya viwanda vya plastiki. Hata hivyo, Shirika hilo halijabuni mitambo hiyo. Mitambo hiyo imepatikana kwa msaada wa Serikali ya Norway kupitia Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (*UNIDO*)

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa mitambo ya kuchakata taka za plastiki ni sehemu ya utekelezaji wa Programu ya Shirikishi ya Maendeleo ya Viwanda Nchini. Serikali inatekeleza programu hii toka mwaka 1999. Lengo la programu hii ni kukuza uendelezaji wa viwanda vidogo vidogo vinavyozalisha malighafi kwa ajili ya viwanda vingine, kuongeza fursa za ajira na kukuza matumizi ya taka kama rasilimali na hivyo kuboresha usafi wa mazingira.

Kwa sasa mitambo ya *TIRDO* iko katika hatua ya majiribio. Serikali inahamasisha viwanda vinavyotengeneza bidhaa za plastiki kukitumia kituo cha *TIRDO* kama chanzo cha malighafi ya shughuli zao. Pia Serikali inatoa motisha ya punguzo la kodi kwenye mitambo na kemikali kwa ajili ya viwanda vinavyorejeleza taka hususan taka za plastiki. Serikali itaendelea kuelimisha wawekezaji ili kuinua shughuli za urejelezaji taka nchini.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inashirikisha sekta binafsi katika shughuli za uzoaji na utupaji taka Mijini. Serikali itaendelea kutoa vitendea kazi kwa vikundi vinavyojishughulisha na ukusanyaji wa taka mbalimbali. Aidha, Serikali itaimarisha mfumo wa kurejeleza taka za plastiki ili kituo kipate malighafi ya kutosha. Nawashauri wamachinga ambao wanakusudia kuingia katika biashara ya kukusanya vifaa chakavu na taka za plastiki kuunda vikundi na kuwasiliana na viwanda husika ili waweze kuingia mikataba ya kuwa wakala wa viwanda hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuwaomba wananchi wajenge tabia ya kutenganisha taka mahali zinapozalishwa na kuzihifadhi katika hali ya usafi ili kupata malighafi bora za viwanda husika.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, ningependa kuuliza je, mashine hizi ziko katika Miji gani mingine na isingekuwa vizuri sasa maadam tumeishajua kwamba kuna mashine za kuchakata vifaa hivyo chakavu vya *plastiki* tukaweza kuzipeleka kwenye Miji mingine ili kuzidi kufanya mazingira yetu yawe safi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO (k.n.y WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa mashine hizi ziko katika Miji ya Dar es Salaam na kiwanda kimoja kiko katika Mji wa Morogoro. Tunatambua kwamba urejelezaji wa taka za plastiki kwa kiwango kikubwa utapunguza matatizo ya uharibifu wa mazingira yanayosababishwa na taka za plastiki. Kwa hiyo, baada ya majaribio ya *TIRDO* endapo itaonekana kuna ufanisi unaotakiwa, basi Serikali itahamasisha wafanyabiashara wengine waweze kufungua viwanda hivyo katika Mikoa mingine.

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Je, Serikali ina mikakati gani ya kuona kwamba sasa ipo haja ya kuhamasisha wananchi kutumia vikapu vinavyotokana na vitu vyetu vya asili ambavyo vingepunguza matumizi ya mifuko ya plastiki ambayo inazagaa kila mahali, na hivyo ingesaidia vilevile kuinua viwanda vidogo vidogo vinavyotengeneza vikapu hivyo ambavyo kimsingi vimekuwa kivutio kwa watalii wengi? Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO (k.n.y WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la swali la msingi ni kwamba Serikali sasa hivi inahamasisha wananchi kwa njia kadhaa vikiwemo vyombo vya habari na mikutano ya ana kwa ana. Lengo na madhumuni ni kuhakikisha kwamba wananchi wanatumia nyenzo mbadala badala ya kutumia mifuko ya plastiki kama anavyoshauri Mheshimiwa Mbunge.

Serikali itaendelea na hamasa hizo lakini wakati huo huo kwa sababu tayari kuna taka nyingi sana za plastiki Serikali ina mikakati kadhaa ya kuweza kuhakikisha kwamba taka hizo zinarejelezwa, na viwanda vinavyofanya hivyo vinapata unafuu wa kodi na wale wananchi wanaojihusisha na kazi hiyo wanapewa vitendea kazi. Haya yote yana lengo la kupunguza taka za pastiki. Lakini wakati huo huo tutahakikisha kwamba tunatoa hamasa kwa ajili ya kutumia vikapu badala ya mifuko ya plastiki kama anavyoshauri Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**Na. 35**

**Malipo Hewa Yaliyobainishwa katika Ripoti ya *CAG***

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2004 imebaini kwamba Wizara ya Ujenzi iliilipa Kampuni ya *Impresaa Del Benaco* malipo hewa ya shilingi 372,143, 940/= hapo tarehe 3/6/2004; na kwa kuwa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete katika hotuba yake ya kulizundua Bunge aliagiza kuwa ni vema ikawepo Sheria ya kumpa madaraka zaidi Mkaguzi Mkuu wa Serikali:-

(a) Je, Serikali imechukua hatua zipi za kisheria dhidi ya waliohusika kutoa malipo hewa?

(b) Je, Serikali inaweza kutamka ni lini italeta Bungeni mapendekezo ya Sheria ya kumpa Mkaguzi Mkuu uwezo wa kuchukua hatua za kisheria dhidi ya wahalifu kama hao?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haijachukua hatua yoyote dhidi ya waliohusika na malipo ya shilingi 372,142,940/= yalifayofanywa kwa kampuni ya *Impresaa Del Benaco* kwa kuwa malipo hayo yalikuwa halali. Kampuni hiyo ilikuwa Mkandarasi wa barabara ya Rusumo – Lusahunga ambaye alikuwa anaidai Serikali jumla ya dola za kimarekani milioni 1.6 mwaka 1988.

Serikali ilikuwa ikilipa deni hilo kidogo kidogo hadi mwaka 1993 ambapo malipo yalisimama kutokana na ufinyu wa bajeti. Wakati huo deni lilikuwa limebaki kiasi cha dola za kimarekani 364,847.01.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa deni hilo lililobaki lililipwa mwaka 2003/ 2004 ilibidi kutumia viwango vya kuwa kubadilisha fedha (*exchange rate*) vya wakati wa kulipa na si vya wakati mkataba wa ujenzi ulipotiwa saini mwezi Desemba 1977. Hivyo, katika shilingi za Tanzania yakawa makubwa kuliko ambavyo ingekuwa hapo awali. Si kwamba yalikuwa hewa ila kwa sababu tu wakati wa malipo thamani ya shilingi yetu ilikuwa imeshuka.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Fedha, imekuwa ikifanya marekebisho ya mara kwa mara katika Sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia mapato na matumizi ya fedha za Serikali kwa lengo la kuboresha utendaji katika usimamizi na uwajibikaji wa mapato na matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Ununuzi ya mwaka 2001 na Kanuni zake ilifutwa na kutungwa sheria nyingine ya mwaka 2004 ili kuboresha taratibu za ununuzi wa bidhaa na huduma kwa Serikali. Pia Sheria ya Fedha ya mwaka 2001 na kanuni zake ilifanyiwa marekebisho makubwa katika mwaka wa fedha ulioishia Juni, 2004 kwa lengo la kuimarisha utendaji katika usimamizi wa fedha za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na marekebisho yaliyokwishafanyika, Serikali inakusudia katika mwaka ujao wa fedha kuziangalia upya sheria hizi na kuzifanyia marekebisho sheria zote hizi na hasa Sheria ya Fedha 2001 kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa fedha za umma. Katika marekebisho hayo, maagizo ya Mheshimiwa Rais kuhusu uwezo na mamlaka ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yatazingatiwa ipasavyo.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na mimi kuuliza swali dogo la nyongeza. Ningependa kumuuliza Naibu Waziri pamoja na majibu mazuri. Wakati ule wanaingia mkataba kulikuwa na *clause* yoyote ambayo ilikuwa inaonyesha kwamba wakati wa malipo watatumia *exchange rate* ya wakati huo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba ulioingiwa kati ya Serikali na Kampuni hiyo ulikuwa wa fedha za dola za Kimerakani. Kwa hiyo, mhusika alitakiwa kulipwa kwa dola za Kimarekani. Sasa kama angelipwa wakati ilipohitajika kulipwa kusingekuwa na malipo yoyote zaidi kwa fedha za Kitanzania.

**Na. 36**

**Ubinafsishaji wa *NMB***

**MHE. LUCAS L. SELELII** aliuliza:-

Kwa kuwa, *NMB* Benki yenye mtandao mkubwa hadi vijijini ambako ndipo walipo wananchi wengi:-

Je, utaratibu uliotumika kuibinafsisha utahakikisha wamiliki wapya hawafungi matawi yaliyoko Wilayani?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii, Mbunge wa Nzega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya makubaliano muhimu kati ya Serikali na Muungano wa Wawekezaji unaoongozwa na *Rabobank* ni utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo (*Business Plan*) wa *NMB* ambao unajumuisha masharti ya kufunga au kufungua matawi. Kulingana na Mpango huo Muungano wa Wawekezaji utayaongezea hadhi (*up-grade*) matawi yote 108 yalipo hivi sasa. Kwa kuanzia matawi 47 majengo yake yameanza kufanyiwa ukarabati na kupatiwa vifaa vya kisasa ili yafanane na matawi ya mabenki mengine.

Vilevile, matawi kumi na moja (11) yatahamishwa (*re-located*). Kwa mfano, pale ambapo inaonekana kwamba nyumba au mazingira ambapo tawi hilo lipo hayafai tawi hilo litahamishiwa kwenye nyumba au mazingira mengine. Hata hivyo, tawi halitahamishwa kutoka katika Wilaya moja kwenda katika Wilaya nyingine.

Aidha, Muungano wa Wawekezaji hawa umepanga kufungua matawi mengine yasiyopungua hamsini (50) ndani ya muda wa miaka mitano ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango huu wa wawekezaji ni sehemu ya mkataba wa mauzo kati yao na Serikali. Wizara yangu itahakikisha kuwa makubaliano haya yanatekelezwa kulingana na mkataba.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Naibu Waziri. Lakini kwa mujibu wa taratibu za Wawekezaji wote huwa wanaangalia faida zaidi kuliko huduma; na kwa kuwa benki hii ya *NMB* ina mtandao katika maeneo ya Wilaya mbalimbali ambazo ni za pembezoni na pengine hazitafanya faida. Je, Serikali itakuwa tayari kubeba hasara ambayo itapatikana katika Wilaya hizo ili benki hii ambayo itakuwa na wawekezaji katika Wilaya ambazo zina hasara matawi yale yasifungwe?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatana na mkataba na kwa sasa hivi tuna matawi 108, matawi wakati *NMB* inaanzisha yalikuwa mengi zaidi ya 108. Haya 108 yaliyobakia yapo sehemu ambazo benki inaamini kwamba itapata faida. Yale matawi mengine 50 ambayo yanataka kuanzishwa katika muda wa miaka mitano ijayo benki imeishafanya

tathmini na inaamini kwamba kule ambako matawi haya 50 yatapelekwa benki itapata faida.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi nami niulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa vile katika Wilaya ya Rudewa kulikuwa na tawi la Benki katika Tarafa kubwa ya Wilaya hiyo inayoitwa Mlangali ambayo inazalisha mazao ya biashara na ya chakula kwa wingi katika Wilaya ile kuliko hata Makao Makuu ya Wilaya yenyewe. Je, Wizara inaweza ikasaidia kwa kuhakikisha kwamba benki ile iliyokuwepo Mlangali *NMB* inafunguliwa upya ili iweze kuwahudumia wananchi ambao wanapata shida ya kusafiri kwenda kilomita zaidi 80 Njombe au kwenda kilomita nyingine 80 Wilayani Ludewa? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Naibu Spika, tunalipokea ombi lake, tutazungumza na *NMB* na tutaangalia uwezekano wa kuanzisha tawi la benki pale. *(Makofi)*

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa vile *NMB* inaonyesha kwamba inajali sana watu wanyonge hata mpaka vijijini inapeleka matawi ya benki; na kwa vile Jimboni kwangu mimi Njombe Magharibi hakuna hata benki moja au chombo chochote cha kifedha ambacho kiko kule. Je, *NMB* ina mpango wowote wa kupeleka huduma hii ya *NMB* kwenye Mji mdogo wa Ilembula ili wananchi wangu wapate kufaidika na huduma za kibenki? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyomjibu Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, tutalitazama, tutazungumza na *NMB,* wataangalia kama wanaweza kupata faida kwa kuweka tawi la benki pale, tawi litafunguliwa katika sehemu ile. *(Makofi)*

**Na. 37**

**Mikopo ya Wanawake**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilikuwa ikitoa Sh.4,000,000/= kila mwaka katika Halmashauri zote kwa ajili ya kuwakopesha wanawake lakini mfuko huo sasa hautolewi tena; na kwa kuwa wanawake wengi ni waaminifu katika kurejesha mikopo hiyo:-

(a) Je, kwa nini Mfuko uliokuwa ukitoa Sh.4,000,00 umesitishwa?

(b) Je, ni lini Mfuko huo utaanza tena kupeleka fedha za mikopo katika Halmashauri hizo?

(c) Je, Serikali itawasaidiaje wanawake na vijana kushirikishwa katika kukuza uchumi?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Kabadi Nyawazwa, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Esther Kabadi Nyawazwa Mbunge kuwa Serikali haijasitisha utoaji wa fedha za Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake katika Halmashauri.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kupeleka fedha za mikopo, katika Halmashauri zilizokwisha kamilisha marejesho ya fedha walizopatiwa. Hii, ni kutokana na utaratibu tuliojiwekea, ili kuhakikisha kuwa fedha hizo zinarejeshwa.

Baadhi ya Halmashauri, zimekuwa zikirejesha fedha hizo kwa muda waliopangiwa. Halmashauri hizo ni pamoja na zile za Mkoa wa Mwanza ambazo ni Geita, Jiji la Mwanza, Magu, Kwimba na Sengerema. Mkoa ambao Mheshimiwa Mbunge ameuliza.

(c)Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuwawezesha wanawake na vijana kiuchumi. Hii ikiwa ni pamoja na kuanzisha Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Mfuko wa Maendeleo wa Vijana.

Mifuko mingine ni pamoja na Mfuko wa Mikopo kwa Wafanyabiashara Wadogo Wadogo *(SELF),* Mfuko wa Maendeleo wa Wajasiriamali *(NEDF)* na Asasi ya Mikopo kwa Wanawake Wazalishaji *(CREW) (T)*. Mikopo hiyo, hutolewa baada ya walengwa kupatiwa mafunzo maalum, ya ujasiliamali ili kuwawezesha kutumia mikopo hiyo vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuanzisha mifuko hiyo, wanawake na vijana wanaendelea kuhamasishwa kujiunga na Vyama vya Ushirika vya Kuweka na Kukopa *(SACCOS)* na *(SACCAS)* na hatimaye kuanzishwa kwa Benki Kata. Serikali pia inaendelea na mchakato wa kuanzisha Benki ya Wanawake. Juhudi hizi zote zinafanyika ili kuhakikisha kuwa wanawake na vijana wanapatiwa mikopo ambayo itawaendeleza na kuwainua kiuchumi na hatimaye kuboresha maisha yao.

Aidha, Wizara yangu kupitia Maafisa wa Maendeleo ya Jamii katika ngazi ya Halmashauri wana jukumu kubwa la kuhamasisha jamii kutumia rasilimali na fursa zilizopo ili wajiletee maendeleo endelevu. Waheshimiwa Wabunge nawasihi watumieni ipasavyo maafisa hao muhimu kwa maendeleo katika Majimbo yenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kupitia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ambavyo vipo kila Mkoa Tanzania Bara, Wizara yangu hutoa mafunzo na stadi mbalimbali kwa wananchi ili waweze kukuza uchumi wao. Kwa mfano, katika mwaka 2004/2005, Vyuo hivi vilitoa mafunzo na stadi kwa wananchi 24,658, ambapo 13,085

walikuwa wanawake na wanaume walikuwa 11,573 na wengi wao wakiwa vijana. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba niulize kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba fedha zile bado zinapelekwa kwenye Halmashauri za Wilaya. Lakini kuna Halmashauri zingine ambazo zinasema kwamba mfuko huu ulisitishwa. Je, Serikali inazichukulia hatua gani Halmashauri ambazo haziwapitii mikopo wanawake zinapotolewa?

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Sh. 4,000,000/= ambazo Serikali bado inapeleka kwenye Halmashauri za Wilaya ni kiasi kidogo sana na akinamama katika swali langu la msingi nimesema ni waaminifu wa kurejesha mikopo hiyo na ni fedha ambazo hazipotei. Je, Serikali sasa haioni umuhimu wa kuongeza kiwango hiki cha Sh. 4,000,000/= kizidi hata kiwe Sh. 10,000,00/=? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ambazo hazijereshi fedha kwa kweli tatizo kubwa lipo katika wale wakopeshwaji wenyewe hawarudishi mikopo. Kwa sababu Wizara haiwezi kutoa fedha nyingine kabla ya zile fedha za mwanzo hazijarejeshwa, basi tunashindwa kuwapa mikopo mingine. Lakini Mheshimiwa Mbunge yeye ni mmoja katika Baraza la Madiwani, kwa hiyo ana nafasi kubwa ya kuwahamasisha hawa Wakurugenzi warejeshe zile fedha ambazo zimerudishwa na pia walete maombi mapya ili waweze kupata *allocation* nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Wizara ina fedha nyingi, lakini inashindwa kuzitoa kwa Halmashauri kutokana na uzembe wa Halmashauri zenyewe kuchelewa kuomba na hiyo wanafanya makusudi na wanashindwa kuleta yale mahesabu kwa sababu hawayaweki vizuri.

Kwa hiyo, hata Serikali ikiwa nazo hizi fedha tutaendelea kukaa nazo na kwa sasa tuna zaidi ya shilingi bilioni 1.4 ambazo zinasubiri Halmashauri zilete maombi na pia kuna mkataba lazima wasaini. Kwa mfano, katika Mkoa wake wa Mwanza, Halmashauri ya Misungwi, Ukerewe na Ilemela hizi Halmashauri bado hazijakamilisha marejesho. Lakini zipo Halmashauri nyingine hazijatimizi yale masharti ya mkataba tu na fedha zipo zinasubiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili, ni kweli Sh. 4,000,000/= ni ndogo, lakini ningependa ikumbukwe kwamba pamoja na Sh. 4,000,000/=, zipo tena fedha ambazo zinatolewa kwa akinamama na vijana ambao ni asilimia 10 ya mapato ya Halmashauri zote. Waheshimiwa Wabunge mkiwa kama Madiwani mna nafasi kubwa ya kuhakikisha kwamba hii asilimia 10, ambapo asilimia 5 inakwenda kwa vijana na

asilimia 5 kwa wanawake inatolewa ipasavyo wakati mnapokuwa mnajadili bajeti za Halmashauri zenu. *(Makofi)*

**MHE. MERYCE MUSSA EMMANUEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Waziri. Napenda kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Serikali imekuwa ikitoa fedha katika Halmashauri zote na fedha hizi zimekuwa haziwafikii walengwa badala yake watumishi wameunda vikundi vya wake zao na wao wenyewe. Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba wanawake hawa wa Halmashauri hizi fedha zinawafikia kama jinsi ilivyopangwa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana kuwa wapo watumishi ambao ni wabadhirifu na wanafanya vitendo kama hivyo. Lakini bado suala hili linarudi kwetu sisi Waheshimiwa Wabunge tukiwa kama ni wasimamizi kule chini, sisi tumo katika zile Kamati. Kuna Madiwani ambao mikopo inajadiliwa katika ngazi ya Kata na katika Kata Diwani ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo hapo ndipo zinapogawiwa zile fedha.

Kwa hiyo, huyo Afisa ambaye anafanya hivyo inabidi pengine aweze kum-*convince* mpaka na Diwani. Kwa hiyo, sisi kama viongozi wa siasa tunawajibika kuhakikisha kwamba ubadhirifu kama huo hautokei. *(Makofi)*

**Na. 38**

**Kuwawezesha Wanawake**

**MHE. JANETH M. MASSABURI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wanawake wengi nchini wanaishi katika hali ngumu ya maisha na kujikuta katika hatari ya kuambukizwa magonjwa ya zinaa kama UKIMWI na kusababisha ongezeko la watoto yatima nchini:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa dharura wa kuwapatia Wanawake mafunzo ya ujasiliamali, sambamba na elimu ya UKIMWI, biashara na ushirika?

(b) Je, Wizara husika imejiandaaje kuhusu suala hilo la Wanawake kuondokana umaskini?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mbunge Viti Maalum, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine imekuwa ikitoa mafunzo ya ujasiriamali sambamba na elimu ya UKIMWI, biashara na ushirika kwa Wanawake. Aidha, mafunzo ya ujasiriamali

pamoja na elimu ya UKIMWI kwa Wanawake hutolewa na Maafisa Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri husika wakishirikiana na wadau mbalimbali kama *SIDO, ILO, UNIDO, TACAIDS* na kadhalika.

Aidha, Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya ni waratibu wa shughuli hizo Wilayani wakishirikiana na Maafisa wa Maendeleo ya Jamii katika ngazi mbalimbali za Wilaya.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati ambayo Wizara yangu imejiwekea ni kuanzisha na kutekeleza programu mahsusi za kuwezesha Wanawake katika ngazi zote, kiuchumi, kwa kuwapatia mafunzo zaidi ya ujasiriamali, jinsia na uongozi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

Aidha, kuimarisha Mifuko ya Mikopo ya Wanawake, kuhamasisha uundwaji wa Vikundi vya Ushirika vya Wanawake vya kuweka na kukopa, *SACCOS, SACCAS* na hatimaye kuwa na Benki Kata. Mifano mizuri ya kuigwa ni kazi nzuri zilizofanywa na Maafisa wa Maendeleo ya Jamii katika Mikoa ya Mbeya na Kilimanjaro katika Wilaya ya Rombo. (*Makofi)*

Wizara pia imeandaa programu za mafunzo ya UKIMWI kwa jamii ambazo zitatekelezwa kwa ushirikiano na *TACAIDS*. *(Makofi)*

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa idadi kubwa ya wahudumu wa Mabaa ambao wengi wao ni Wanawake nchini na hasa Mkoa wa Dar es Salaam wanafanya kazi kwa saa 18 kwa siku na wanalipwa shilingi 20,000/= kwa mwezi. Je, Serikali haioni eneo hili ni chanzo cha ongezeko la UKIMWI kutokana na kipato kidogo wanachokipata wahudumu hawa? (*Makofi)*

Pili, Serikali haioni umuhimu wa Wanawake na iko haja ya kushirikiana na wamiliki wa Mabaa kwa kuweza kuratibu au kuwapangia mishahara wafanyakazi hao angalau wapate shilingi 60,000/= ingawaje bado ni kidogo kiwango hiki? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana naye kwamba wafanyakazi katika Mabaa wanakuwa katika hali mbaya kutokana na masaa mengi wanayofanya na ile hali ya kazi yenyewe kwani walevi wanapolewa wanakuwa wanapata misisimko mbalimbali na hivyo wanakuwa katika nafasi mbaya ya kushawishiwa hao wateja wao.

Kwa hiyo natoa wito kwa wafanyakazi akinamama na akinababa wote ambao wanafanya kazi baa wajitahidi waepukane na vitendo vya ngono ambavyo vitawaletea gonjwa hili la UKIMWI.

Pili, ni kweli kwamba wamiliki wa Mabaa wanawalipa kiwango kidogo sana wafanyakazi katika Mabaa ambako wanafanya kazi kwa muda wa masaa mengi. Sheria ipo ambayo inawataka iwalipe wafanyakazi kiwango cha chini na pia wapate muda wa kupumzika. Kwa hiyo, hili ni suala la sheria hao wafanyakazi wa Mabaa wanaweza wakaungana pamoja na kutafuta haki zao. *(Makofi)*

Na. 39

**Ujenzi wa Barabara ya Bomang'ombe**

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika hotuba ya Bajeti ya mwaka jana Serikali ilikubali kuijenga barabara itokayo Bomang'ombe kupitia Wilaya ya Siha ka;tika Mji mdogo wa Sanya – Juu hadi Ngarenairobi na Kamwanga; na kwa kuwa, aliyekuwa Waziri wa Ujenzi wakati huo Mheshimiwa Magufuli wakati Rais Mstaafu Mheshimiwa Mkapa alipokuwa anaweka jiwe la Msingi la Barabara ya Rombo itokayo Marangu hadi Tarakea aliahidi kuwa, barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami; na kwa kuwa, barabara hiyo ni muhimu sana kwa shughuli za kiuchumi hasa zile za kitalii ikiwa ni pamoja na kupanda Mlima Kilimanjaro:-

Je, ukiacha masuala ya upembuzi yakinifu, ni lini barabara hiyo itaanza kujengwa ili wananchi wa Siha wajiandae kwa ajili ya ujenzi huo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aggrey Deaisile Mwanri, Mbunge wa Siha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa barabara ya Sanyajuu kupitia Ngarenairobi hadi Kamwanga yenye urefu wa kilometa 74.0 ni muhimu sana katika shughuli za kiuchumi na kijamii. Aidha, ni kweli kwamba Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu na Waziri wa iliyokuwa Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa John Pombe Magufuli, kwa pamoja walisisitiza azma ya kuiendeleza barabara ya Tarakea – Kamwanga inayojengwa sasa kwa kiwango cha lami, ili izunguke Mlima Kilimanjaro kupitia Ngarenairobi hadi Sanyajuu na Bomang'ombe, na hivyo kuwawezesha Watalii na wananchi wasioweza kupanda mlima huo angalau wafurahie mandari yake ya kipekee duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu huo, iliyokuwa Wizara ya Ujenzi ilitenga fedha za kufanya upembuzi yakinifu wa sehemu husika katika bajeti ya mwaka 2005/06 kama ilivyofafanuliwa kwenye hotuba ya bajeti ya Wizara hiyo ukurasa 141. Wataalamu wa kufanya kazi hiyo wamekwisha orodheshwa tayari kwa kuteuliwa. Matokeo ya upembuzi yakinifu huo ndiyo yatakayoiwezesha Serikali na *TANROADS* kuamua juu ya hatma ya barabara hiyo. Kwa sababu hiyo ni mapema mno kutamka ni lini hasa itaanza kujengwa.

Hata hivyo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* Mkoa wa Kilimanjaro itaendelea kuifanyia matengenezo ili iendelee kupitika wakati wote.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Naomba nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo ameyatoa.

Kwa kuwa imethibitika kwamba sasa Mlima kama wa Kilimanjaro ungekuwa katika nchi kama *South Africa almost 50%* ya bajeti yake ingekuwa inatokana na mafao yanayotokana na Mlima huo. Na kwa kuwa kuna *activities* nyingi sana za kiuchumi zinazofanyika katika eneo la West Kilimanjaro. Kuna mashamba kule ya *TBL* ya *NAFCO.* Je, Serikali haioni kwa vile sasa kuna barabara nyingi nchini ambazo hazijatengenezwa kwa ku-*invest* katika barabara hii ninayoizungumzia itawezesha hata barabara zingine za nchi hii kuweza kufanyiwa matengenezo na kujengwa katika kiwango cha lami kama nilivyozungumza. Na kwa hiyo basi, huo ni umuhimu wa kuingiza hii katika bajeti walau inayokuja ili tuweze kuanza kazi hiyo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi ni nia ya Serikali kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Ndiyo maana tayari fedha zimetengwa za kufanya upembuzi yakinifu. Serikali isingeweza kutenga mamilioni ya fedha kuanza kazi hii ya upembuzi yakinifu kama isingekuwa na nia thabiti ya kuja kujenga barabara hii. Kama nilivyosema ili ujenge barabara kwanza lazima uanzie upembuzi yakinifu na baadaye ufanye *designs.* Sasa yote hayo ni hatua, kwa hiyo namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba nia hii ya Serikali itatekelezwa kwa kadri ya mipango ilivyowekwa. *(Makofi)*

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niiulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali iliona kwamba hii barabara ni muhimu ndiyo maana wamejenga mwaka wa 1970, miaka ya 70 imejenga barabara hii kutoka Bomang'ombe ikapita Sanyajuu wakaiacha. Na mpaka wakati huu ndio wanataka tena kujenga. Je, kwa kuwa barabara hii ni muhimu zaidi ndiyo imeonekana kwamba inafaa iendelezwe. Kwa nini Serikali ina kigugumizi miaka yote kumalizia barabara hii ifike Kamwanga kama ilivyopendekezwa miaka ya nyuma?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii inafika Kamwanga ambacho ndicho kijiji cha mwisho cha Wilaya ya Rombo kupakana na Wilaya yake ya Longido, Hai, Kajiado Kusini upande wa Kenya na ni kijiji cha kipekee. Kwa hiyo, mkandarasi anaendelea wakati wowote atafika Kamwanga na baada ya pale ndio upembuzi huu alioutaja Naibu Waziri na *design* hiyo aliyotaja Naibu Waziri zitaonyesha kama barabara hiyo izunguke mbele ya Kamwanga kuelekea Wilaya ya Hai yaani Bomang'ombe, Ngarenairobi na kadhalika kama alivyosema mwuliza swali au la. Lakini tumaini langu ni kwamba upembuzi huu utaonyesha matumaini kwa sababu upembuzi wa awali wa huko nyuma ulikuwa umeonyesha hivyo lakini sasa tumerudia ili tufanye kazi ya kisayansi zaidi. Sisi wote katika Wizara tuna matumaini na naomba watuache tufanye hiyo kazi kwa mujibu wa utaratibu.

**Na. 40**

**Huduma ya Simu za Mkononi – Somangila**

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI** aliuliza:-

Kwa kuwa, kutoka Kata ya Somangila hadi Pemba Mnazi ni maeneo yenye neema ya biashara ya Utalii kutokana na fukwe za maeneo hayo lakini hakuna mawasiliano ya uhakika wa simu za mkononi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhamasisha Kampuni za Simu za Mkononi za *CELTEL, VODACOM* na *MOBITEL* kuongeza mnara katika maeneo ya Somangila na Pemba Mnazi ili kuwaondolea kero wananchi na watalii wanaofika katika maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mbunge wa Kigamboni kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa huduma za mawasiliano ya simu ni muhimu katika kuharakisha maendeleo ya Taifa kwa kuhudumia shughuli za sekta za kijamii na kiuchumi ikiwemo ya Utalii. Serikali kupitia Wizara yangu imeendelea na juhudi za kuhakikisha huduma za mawasiliano zinafikishwa katika sehemu zote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kata za Somangila na Pemba Mnazi, Wizara imekwishafanya mawasiliano na Makampuni ya *CELTEL, VODACOM* na *MOBITEL* ambayo yamehamasika kutoa huduma hizo kama ifuatavyo:-

*CELTEL* – Wanatarajia kufanya tathmini ya Pemba Mnazi ili kuainisha mikakati na mpango wa kupeleka huduma za simu huko. Hivi sasa tathmini ya Kazimzumbwi imekamilika.

*VODACOM* – Baadhi ya sehemu katika maeneo ya Kata hizo yanapata huduma za simu ingawa hazikidhi mahitaji. Kampuni ya *VODACOM* wametuarifu kuwa watatembelea eneo hilo na kufanya uchambuzi sahihi ili kubaini nini kifanyike. Wizara kwa upande wake itafuatilia kwa karibu zaidi utekelezaji wake.

*MOBITEL* – Inao mpango wa kuweka mitambo katika maeneo ya Kimbiji na Ras Sultan katika kipindi cha miezi mitatu ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inamwomba Mheshimiwa Mbunge naye aendelee kuhamasisha wananchi ili watumie kikamilifu huduma za Makampuni hayo zitakapo wafikia ili gharama za uwekezaji wao ziweze kuwaletea tija na hivyo wapate ari ya kwenda maeneo mengine nchini. *(Makofi)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona. Nashukuru majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri na mimi naomba kuuliza swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa matatizo yanayolikumba jimbo ambalo Mheshimiwa ametoka kujibiwa swali ni tatizo linaloikumba pia Muleba Kaskazini. Kata zile ambazo ziko karibu na Ziwa Victoria ambako kuna bonde kama Kata za Mayonde, Izigo na Kagama pamoja na Kata zingine hazipati mawasiliano. Kwa kuwa mawasiliano ya simu zote alizozitaja Kampuni zote zipo katika jimbo la Muleba Kaskazini. Je, Serikali itakuwa tayari kunisaidia kuhakikisha kwamba kusikika huko kunaweza kuwepo hata katika jimbo la Muleba Kaskazini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ukitaka kujibu, jibu. Lakini swali lilikuwa la Kigamboni.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo nadhani nimjibu Mheshimiwa Ruth Msafiri. Kwa kweli ni nia ya Makampuni haya ya simu kuweka mtandao wa simu nchi nzima isipokuwa katika kila Kampuni hizi ni Kampuni zinazofanya biashara lazima zifanye tathmini ya kiuchumi, ya ki-*technical studies* na vile vile kuangalia *market survey*. Kwa hiyo, nina hakika katika jimbo lake baada ya kufanya tathmini hizi Makampuni hayo yataingia katika maeneo ambapo hayajafikiwa bado.

**Na. 41**

**Elimu kwa Watoto Wasio na Makazi**

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imeunda Sera ya Elimu ambayo itasaidia na kuwawezesha watoto wetu kujipatia elimu bora:-

(a) Je, Sera hiyo ina utaratibu wowote wa kutoa Elimu ya Sekondari kwa lazima kwa Watoto wa Mitaani ambao wamepatikana kutokana na uzazi usio rasmi?

(b) Je, kuna fedha zozote au shule maalum zilizotengwa kwa ajili ya watoto wa aina hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge wa Dimani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Elimu na Mafunzo inatamka wazi kuwa Elimu ya Msingi ni haki kwa kila mtoto na ya lazima ikiwa ni pamoja na watoto wa mitaani. Hadi sasa kwa mujibu wa Sera hiyo, Elimu ya Sekondari bado si ya lazima kwa watoto wote. Katika ngazi ya Elimu ya Msingi, Serikali ilianzisha Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa (MEMKWA). Baadhi ya wanafunzi wa mpango huo ni watoto wa mitaani na wale waliotoka katika ajira mbaya. Kuanzia mwaka 2003 hadi 2005, jumla ya wanafunzi 239 wa MEMKWA, wamefaulu mtihani wa darasa la saba na kuingia katika Shule za Sekondari za Serikali.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna shule maalum zilizotengwa kwa ajili ya watoto wa aina hiyo. Hata hivyo, Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES), unao utaratibu wa kugharamia Elimu ya Sekondari, kwa watoto wanaotoka katika familia zenye kipato duni wakiwemo watoto wa mitaani. Kwa mfano katika mwaka wa fedha 2005/2006 jumla ya wanafunzi 25,481 wamefaidika na utaratibu huo.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake sahihi. Lakini nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu watoto wa mitaani ni watoto ambao hawana utaratibu maalum. Je, Serikali inao utaratibu maalum wa kuwakusanya vijana hawa na kuwawekea Elimu hiyo ya Msingi hadi Sekondari?

Lakini pili kwa sababu watoto hao kwa hivi sasa wamekuwa ni wengi kwa Tanzania, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza akaliambia Bunge hili kwamba endapo

atatokea mfadhili kutoka nje na akawaomba vijana hawa awachukue kwa ajili ya kuwasomesha nje ya Tanzania, je Serikali iko tayari?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Naibu Spika, (a) hadi sasa baadhi ya wafadhili ndani ya nchi au asasi zisizo za Serikali zinazosaidia kuwakusanya hawa watoto na kuwasomesha mojawapo ni *Dogodogo Centre* na ziko nyingi zikiwa chini ya Wizara nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, (b) sidhani kama itakuwa ni busara kuwaruhusu wafadhili kutoka nje kuwakusanya watoto wetu na kwenda kuwasomesha nje ili mradi tu ni wa mitaani. Napenda kulitamkia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali ina mpango mzuri tu wa kuwasaidia watoto wa mitaani ili wapate elimu. Kwa mfano tumeona mpango wa MMES na hata MMEM imewasaidia na baada ya hapo zipo Wizara zingine ambazo zina mikakati rasmi ya kuwasaidia watoto wa mitaani. Sioni kama ni busara kufanya hivyo. Ahsante. *(Makofi)*

Na. 42

**Kuboresha Elimu Kwa Walemavu**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa, elimu ni mojawapo ya agenda zinazozingatiwa na Serikali ya Awamu ya Nne; na kwa kuwa, hadi sasa elimu kwa kundi la walemavu haijapewa upendeleo mkubwa kwa maana ya miundombinu ili kuiboresha:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani maalum wa kuipatia Wizara ya Elimu fedha kwa ajili ya kununulia magari, mashine na vifaa vingine kwa ajili ya kundi hilo la walemavu?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuziongeza shule hizo za watoto wenye ulemavu Mikoani?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWAMTUM B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anna Lupembe, Mbunge wa Viti Maalum, yenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikiipatia Wizara yangu fedha kwa ajili ya kununulia magari, mashine na vifaa vingine kwa ajili ya kununulia magari na vifaa vingine kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu kupitia bajeti ya kawaida iliyoidhinishwa na Bunge hili. Kwa mfano mwaka wa fedha 2005/2006 jumla ya shilingi 437,843,375/= zimetumika kununua magari mawili na mtambo mmoja wa kuchapisha vitabu vya wasioona. Vile vile Wizara imenunua vifaa vingine vya kujifunzia na

kufundishia wanafunzi wenye ulemavu. Aidha, Wizara imeweza kutoa Ruzuku ya Maendeleo jumla ya Tshs. 528,658,250,000/= kwa ajili ya shule na vitengo 77 vya Elimu Maalum. Madhumuni ya fedha hizo ni kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa miundombinu kama ifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| Shule za walemavu wa viungo | 3 |
| Shule za viziwi | 22 |
| Shule za Wasioona | 26 |
| Shule za Walemavu wa Akili | 44 |
| Shule za Viziwi Wasioona | 2 |
| JUMLA | 77 |

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu ina idadi ya shule na vitengo vipatavyo 198 vyenye jumla ya wanafunzi 17,207. Shule na vitengo hivyo vimegawanyika kwa aina ya Ulemavu kama ifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| Shule za Wasioona | 31 |
| Shule za Viziwi | 32 |
| Wenye Ulemavu wa Akili | 126 |
| Viziwi Wasioona | 4 |
| Walemavu wa Viungo | 5 |
| JUMLA | 198 |

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali ikishirikiana na wadau mbalimbali inaongeza uwezo wa shule zilizopo na kuboresha miundombinu ili ziweze kupokea wanafunzi zaidi. Aidha, upo mpango wa kubaini mahitaji halisi ya kundi hilo kwa kila Mkoa. Serikali itaendelea kuongeza shule hizo kadri ya uwezo uliopo.

## Na. 43

### *Organic Farming*

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS** aliuliza:-

Kwa kuwa, mimea inayopandwa bila kutumia mbolea ya chumvi chumvi *(organic farming)* hutoa mazao bora na ambayo bei zake huwa nzuri kwenye soko la nje ya nchi:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kuwasaidia wakulima kutumia njia hiyo ya kilimo kwa lengo la kuinua kipato chao?

(b) Je, kuna utafiti wowote uliofanywa na Serikali kuhusu kilimo cha aina hiyo ili kubaini faida au hasara zake kiuchumi zikoje ikilinganishwa na kilimo kilichozoeleka kwa wakulima wengi cha kutumia mbolea za chumvi chumvi?

(c) Je, kuna hasara zozote kiafya kwa walaji wa muda mrefu wa mboga mboga zinazolimwa kwa kutumia mbolea za chumvi chumvi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani, napenda kutoa maelezo ya awali kama ifuatavyo:-

Kilimo hai au *organic farming* ni aina ya kilimo kinachozingatia matumizi endelevu ya rasilimali za uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo. Kilimo hicho kinatumia mbolea na madawa yasiyotengenezwa viwandani na kinazingatia utunzaji wa mazingira kwa ajili ya manufaa kwa jamii, kiuchumi na kiafya. Ili bidhaa zikubalike katika Soko la Kimataifa kuwa zimezalishwa kwa kutumia mbinu za kilimo hai, zinapaswa kwanza kupitishwa na Taasisi zinazosimamia ubora wa bidhaa hizo.

Taasisi hizo ni *International Federation of Organic Agriculture Movement (IFOAM)* na Shirika la Ubora wa Viwango vya Vyakula la Umoja wa Mataifa (*Codeaux Alimentarius Commission*). Soko la mazao ya kilimo hai hutegemea walaji wa mazao hayo ambao wapo tayari kulipa bei kubwa kwa mazao ambayo yamezalishwa bila ya kutumia viatilifu na mbolea za viwandani.

Kwa mfano, katika mwaka 2003/2004 wastani wa bei za mazao ya kilimo hai ilikuwa takriban asilimia 20 – 50 juu ya bei za mazao yasiyo ya kilimo hai katika Soko la Jumuiya ya Ulaya na Marekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya awali, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo hai nchini kilianza kupata umaarufu katika miaka ya 1990 baada ya Serikali kuruhusu Taasisi kadhaa zisizo za Kiserikali *(NGO)* zikiwemo *EGAJ, INADESTZ, PELUM, Meatu Cotton Projects*, *Babati LAMP* na nyinginezo zilizojitokeza kueneza elimu na teknolojia za kilimo hai.

Aidha, Serikali kwa kutambua umuhimu wa kilimo hai na nia ya kuwasaidia wakulima kuendeleza kilimo hicho imeweka vipengele muhimu kwenye sera yake ya kilimo ikiwa ni pamoja na kuruhusu Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kusimamia biashara na bidhaa zake ambapo mwaka 2005 iliruhusu kuundwa kwa *Tanzania Organic Agriculture Movement (TOAM)* yenye lengo la kuwaunganisha wadau wa kilimo hai na kuwajengea uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na juhudi hizo hivi sasa kilimo hai kinalimwa katika Mikoa ya Kilimanjaro, Tanga, Kigoma, Iringa, Pwani, Kagera, Mbeya, Morogoro, Shinyanga na Arusha. Mazao yanayozalishwa kwa njia ya mkataba ni pamoja na kahawa, chai, korosho, cocoa na pamba. Mazao mengine ni matunda na viungo hususan mananasi, tangawizi, *tumeric, vanilla*, pilipili na vitunguu.

Sehemu kubwa ya bidhaa wanazozalisha zinauzwa moja kwa moja katika Soko la Jumuiya ya Ulaya na kiasi kidogo katika Soko la Marekani.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua faida inayoweza kuletwa kwa kuendeleza kilimo hai nchini ili kuhakikisha kuwa wakulima wanapata bei nzuri na masoko yenye uhakika ya mazao hayo.

Kwa mfano: katika Soko la Dunia, kwa mwaka 2005/2006 kahawa iliyozalishwa kwa kilimo hai (*organic coffee*) iliuzwa kwa Dola za Kimarekani *(USD) 65.7* kwa kilo 50 ikilinganishwa na *USD 50.0* kwa kilo 50 za kahawa iliyozalishwa kwa kutumia kemikali za kilimo *(agro-chemicals).* Aidha, *vanilla* iliyouzwa nchi za Jumuiya ya Ulaya ilipata *premium* ya asilimia 20 hadi 300.
Hata hivyo, masharti yanayoambatana na kilimo hai yanakuwa magumu kwa baadhi ya wakulima na hivyo wakulima wengi kushindwa kuzalisha mazao hayo pamoja na kuwa yana bei kubwa. Wizara yangu itaendelea kushirikiana kwa karibu na Taasisi zinazoendeleza kilimo hai nchini ili kuhakikisha kwamba ubora wa mazao yanayozalishwa ni wa juu kulingana na viwango vya Kimataifa.

Utafiti wa kina unafanywa na Mashirika ya Nchi za Afrika Mashariki ambayo ni (*Kenya Organic Agricultural Network (KOAN), National Organic Agricultural Movement of Uganda (NGAMU)* na *Tanzania Organic Agricultural Movement (TOAM)* ili kuboresha uzalishaji na fursa za biashara ya bidhaa za kilimo hai katika nchi za Afrika Mashariki. Matokeo yatatolewa baada ya utafiti kukamilika.

( c) Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa hakuna tafiti zilizoonyesha hasara zozote kiafya zinazoweza kumpata mlaji wa muda mrefu wa mboga au mazao yoyote yaliyozalishwa kwa kutumia mbolea za chumvichumvi. *(Makofi)*

**Na. 44**

**Makato Mbalimbali kwa Zao la Pamba**

**MHE. LUHAGA J. MPIMA** aliuliza:-

Kwa kuwa, pamoja na Pamba kushuka ubora na thamani kwenye Soko la Dunia, lakini shilingi 20/=; *Tanzania Cotton Lint and Seed Board* 5/=; mchango wa Mfuko wa Elimu shilingi 5/=, Pembejeo shilingi 15/=; na kwa kuwa, zao hilo ndilo zao kuu la biashara kwa Wakulima wa Meatu, na maeneo mengine ya Shinyanga, Mwanza, Singida, Mara na Tabora:-

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya uongezaji wa bei ya zao hilo kuanzia msimu wa 2006/2007?

(b) Je, ni lini Serikali itatenga ruzuku kulipia ushuru wa makato ambayo wakulima wanakatwa kwa kila kilo ya Pamba?

(c) Je, usimamizi wa ubora ukoje kuanzia vyama vya msingi hadi kiwandani?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge wa Kisesa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kumekuwepo na makato mbalimbali kwa kilo kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kuendeleza zao la pamba kama alivyoainisha Mheshimiwa Mbunge. Makato hayo kwa ujumla wake hupunguza bei ya pamba ya mkulima.

Hata hivyo, kufuatia kuanzishwa kwa mfumo wa uchumi wa Soko unaozingatia taratibu za soko huria, Serikali haipangi bei za mazao ya kilimo ikiwemo pamba. Utaratibu unaotumika ni ule wa makubaliano kati ya muuzaji na mnunuaji kwa kuzingatia misingi ya soko huru inayojali mahitaji na upatikanaji wa bidhaa (*demand and supply)*.

Pamoja na hivyo Serikali imeamua kuboresha bei ya pamba kwa mkulima kwa kuondoa ushuru wa shilingi 5/= kwa kilo uliokuwa unatozwa kwa ajili ya kugharamia uendeshaji wa Bodi za Mazao ikiwemo Bodi ya Pamba kuanzia mwaka wa fedha wa 2006/2007.

Aidha mchango kwa ajili ya mfuko wa elimu umepitwa na wakati kwa sababu ua kuwepo kwa mipango ya MMEM, MMES na *TASAF*. Kwa mantiki hiyo bei ya pamba inatarajiwa kuboreka kwa kuwa baadhi ya makato yatakuwa yameondolewa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua mzigo mzito uliokuwa unabewa na wakulima kuanzia mwaka 2006/2007, Serikali itatoa ruzuku kwa ajili ya kugharamia Bodi ya pamba badala ya kutegemea makato ya mazao ya pamba aliyokuwa akikatwa mkulima. Tangazo la Serikali juu ya uamuzi huu limekwisha kutolewa.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, zao la pamba limewekewa usimamizi wa ubora katika hatua mbalimbali. Pamba husimamiwa kuanzia shambani kwa wakulima, kuelimishwa kanuni za kilimo bora cha pamba kupitia mabwana shamba, vipindi vya redio na vipeperushi. Katika ngazi ya magulio, Bodi ya Pamba kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya hukagua pamba inayonunuliwa mara kwa mara.

Aidha mnunuzi anawajibika kununua pamba iliyotengwa katika madaraja ya A na B na isiyokuwa na uchafu wa aina yoyote. Katika ngazi ya viwanda Bodi ya Pamba imekuwa ikiajiri makampuni binafsi kwa ajili ya kusimamia ubora na usafi wa pamba na ukusanyaji wa takwimu za pamba. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda umekwisha pia. Nina matangazo mawili, kwanza Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi Dr. Abdallah Kigoda, anawatangazia wajumbe wa Kamati yake waende sasa hivi kwenye chumba namba 227 kwa ajili ya kuendelea kuujadili Muswada unaofuatia.

Tangazo la pili, Mheshimiwa James Msalika, Mwenyekiti wa Chama cha *Amani Forum* anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote waliojisajili kuwa wananchama wa Amani *forum* Tanzania na ambao wanapenda kujiunga na Chama cha kihiari Bungeni kuwa wakutane leo tarehe 30/3/2006 katika ukumbi 227 ghorofa ya pili katika jengo la utawala saa saba mchana. Wale wengine ni saa tano asubuhi chumba hicho hicho, na ajenda kuu ya kikao hicho ni kuchagua uongozi wa *Amani Forum* tawi la Tanzani.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Benki Kuu wa Mwaka, 2006
### *(The Bank of Tanzania Bill, 2006)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kuanza kwa kuwapongeza, kwanza kumpongeza Waziri wa Fedha na pia Watendaji wote wa Wizara yake kwa kuona umuhimu wa kuleta Muswada ili kubadirisha Sheria ya Benki yetu katika kipindi hiki.

Ni kweli kwamba kwa dunia ya leo tusingweza kuendesha Benki yetu kwa Sheria ya zamani. Kuna mambo mengi sana ambayo kwa kweli yamo kwenye Muswada huu

mzuri, mpya ambao tumeupata ambao naomba kuupongeza. Nimefurahishwa sana na vipengele vingi lakini ningependa kujikita zaidi kwenye vipengele ambavyo pengine ni maoni yangu kwamba vingeboreshwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitapenda kuanzia kifungu namba 53 ambacho kinazungumzia ushiriki wa Benki katika ku-*deal* na *gold*. Kama walivyochangia wenzangu jana, nilifikiri ni muda muafaka sasa kwa Benki yetu kushiriki moja kwa moja kama ilivyo kwenye Sheria ilivyopendekeza kuliko ilivyo hivi sasa kwamba madini haya ambayo ni muhimu kabisa kwa nchi yetu sasa, kwani inavyoonekana ni kwamba Serikali imeacha zaidi yaendeshwe na wafanyabiashara wawekezaji wa nje, na kwa sheria ambazo zinakuwepo zinakuwa hazitoi nafasi nzuri kwa watanzania kunufaika na madini yao; na kwa kuwa madini haya ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi na ni *reserve* ya Benki, nilifikiri ni vizuri ushiriki wa Benki ukaongezwa kwa namna fulani siyo lazima kuwa kama ilivyokuwa zamani kwamba Benki Kuu ilikuwa inashiriki moja kwa moja ununuaji wa dhahabu na madini mengine lakini walau ukawepo ushiriki wa Benki wa karibu zaidi kuliko ambavyo mazingira yaliweza kujengeka kwa siku za karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika ningependa kuchangia kwenye vipengele vinavyohusu uendeshaji wa Benki yenyewe yaani *Management* ya Benki. Nashukuru kuona kwenye mapendekezo marekebisho ya Muswada kwamba sasa walau kwenye Bodi kuna kuwepo na upigaji kura lakini bado ninaona kabisa kwamba kuna mapungufu katika *Management* au tuseme utawala wenyewe unapungukiwa *accountability;* na kama ulivyo Muswada wenyewe unatoa nafasi kubwa kwa Gavana na watendaji wake wa karibu katika Benki kuweza ku-*miss use* mamlaka yao. Nitaoa mfano kwa kupitia baadhi ya vipengele ambavyo bado vipo kwenye Muswada uliopendekezwa.

Kwa kuzingatia kwamba Gavana ndiyo atakayekuwa Mwenyekiti wa Bodi na upigaji kura unapofikia wakati kifungu namba 11 (7) kinampa mamlaka Gavana kuwa na uamuzi wa mwisho na wale Manaibu Gavana watatu ni Watendaji wa siku hata siku wa shughuli za Benki. Ninakuwa bado na wasi wasi kwamba maamuzi muhimu bado yataendeshwa kwa mtizamo au mwenendo ambao utamnufaisha zaidi au watafurahisha zaidi hawa watendaji wakuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika, Bodi kuwa inaendeshwa chini ya uwenyekiti wa Gavana pamoja na kwamba kunawachangiaji ambao wamesema kwamba kwa mujibu wa utafiti uliofanyika kwenye Benki za Sehemu nyingine kwamba Mwenyekiti yafaa awe Gavana wa Benki, lakini mimi nilikuwa bado nina wasiwasi wa utaratibu huo kutokana na tofauti ya kimazingira kati ya nchi yetu na nchi nyingine zilizotolewa mfano kama Nigeria. Kwa mazingira yetu ya sasa mimi nisingependa kusikia nchi yetu inatumbukia kwenye *scandal* kubwa kama ilivyo kwenye nchi nyingine za jirani kwa sababu tu mazingira ambayo tumeyaweka kwa watendaji hawa wa Benki yametoa uhuru mno kuwapa nafasi kufanya wanachokitaka.

Sehemu na namna nzuri kabisa ya kupunguza matatizo, ufisadi tuseme kwa lugha ya moja kwa moja ni kuweka *controls* katika *systems* na sio kutegemea uaminifu wa watu au ku-*copy model* ya sehemu nyingine ambayo hai-*fit* mazingira yenu. Kwa hiyo, mimi

nilifikiri kwamba ni vizuri sana ukizingatia kwamba hii ni Tanzania sio Nigeria. Kwa hiyo, bado tungeweza kusema kwamba Mwenyekiti wa Bodi awe mtu mwingine ili kuweza kuweka uwajibikaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hayo kama nilivyosema kwa wasi wasi kwamba kwa kuwa Gavana ndiye anayehusika na utendaji wa siku hadi siku wa Benki, *internal controls* zinazokuwa zimewekwa zinakuwa ni hafifu mno ukizingatia kuwa Gavana anakuwa na mamlaka ya kuajiri na kufukuza kazi watu kwa mujibu wa kifungu namba 15 (1). Maana yake ni kwamba endapo kutatokea matatizo ya kawaida kwa mfano *Director* fulani katika Benki Kuu akawa ameshindwa kufanya kazi kwa matarajio ya Gavana au wakakwaruzana kibinadamu kukawa na pendekezo la kufukuzwa kazi akafanya *referral* au akapinga, akakata rufaa kwenye Bodi akaenda kukumbana na Gavana yule yule ambaye ndiye mwajari wake na Mwenyekiti huko, naamini katika mazingira hayo tatizo bado litakuwepo. Kwa hiyo nilifikiri hilo eneo ni vizuri likaangaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili nilikuwa na wasiwasi pia na kipengere namba 65 kinachoweka *immunity* kwa watendaji wakuu wa Benki nikimaanisha Gavana na wafasnyakazi wengine kwamba wafanyakazi hawa wasiwajibishwe endapo watafanya kazi katika maeneo yao ya kazi, na hapa limetumiwa neno kama wame-*deal in good faith.*Neno *good faith* ni gumu sana ku-*establish* dhamila ya mtu kwamba hii ni *good faith* au sio *good faith*. Nilifikiria *immunity* hii iliyowekwa bado inaweza ikatumika vibaya na kwa maana hiyo nilifikiria ni vizuri kipengere hicho kikaboreshwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo jingine ningependa kumalizia kuchangia ni kuhusu mamlaka ya Bodi kutengeneza *By-laws* zinazohusu uendeshaji wa Benki na pia uwezo wa Bodi kuamua *allowances* za *Board Members* kwa mujibu wa kifungu namba 24. Nilifikiria pamoja na mamlaka au uhuru ambao watendaji wakuu wa Benki wanapenda waupate ni vizuri hayo yakizingatiwa lakini hicho kifungu kikaboreshwa zaidi. Nina wasi wasi kwamba *personal interest* bado zinaweza zikawa na nafasi na kwa mazingira hafifu ya kikanuni. Kwetu sisi wahasibu tunaamini kwamba *segregation of duties* ni njia moja nzuri sana ya kuweza kusaidia kupunguza matatizo ya *mis-management* au *under performance* katika maeneo yoyote ya kiutawala. Sasa hayo yasipozingatiwa matatizo yanaweza yakatokea na nisingependa matatizo yatokee Muswada umekuja tumeuona nilifikiria ni vizuri tukachangia hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa mchango huo naomba tu nimalizie kama nilivyoanza kwa kutoa pongezi sana kwa Wizara kwa maeneo mengine yote ya kiutendaji tuseme *professional areas* ya kiutendaji wa Benki, kama *Monitory Policies* yamechangiwa sana na wenzangu na sina matatizo katika maeneo hayo na kwa ujumla nauunga mkono Muswada vizuri kabisa naukubali ila ningefurahi sana kama tungeweza kuangalia maeneo machache yaliyokuwa yamebaki ili tuyaboreshe zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Muswada huu, naomba tu kabla ya kutoa mchango wangu ni-*declare interest* zangu kwamba ni mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi na kwa muda wa takribani siku nne, tulikuwa Dar es Salaam pamoja na watu wa Benki Kuu kwa ajili ya mjadala wa Muswada huu. Kwa maana hiyo ni kwamba yale ambayo yalielezwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi , yote kwa pamoja nakubaliana nayo.

Lakini kuna baadhi ya maeneo ambayo nataka kuchangia kwa ajili ya kusaidia kuboreshwa kwa muswada wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba niweke wazi kwamba Muswada huu umekuja wakati muafaka. Kwa sababu kuna mabadiliko makubwa sana katika sekta ya fedha na mabadiliko hayo yanahitaji kutungiwa sheria, na ndiyo maana napenda niwapongeze sana watu wa Benki Kuu na watu wa Wizara ya Fedha kwa kuamua kwa dhati kabisa kwamba badala ya kufanya mabadiliko au marekebisho katika Sheria ya zamani wameamua kuleta Sheria mpya; na hili ni jambo la msingi kabisa kwa sababu ni lazima nchi yetu iendane na nchi nyingine kwa sababu sisi sio kisiwa na kwa sasa yale mabadiliko ambayo tulikuwa tunazungumza zamani kwamba mazingira yetu ni tofauti na maeneo mengine yanaanza kubadilika kufuatana na hali halisi ya utandawazi na mfumo wa soko ambao unaendelea dunia nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa baadhi ya maeneo ambayo ningependa kuchangia ni suala zima la uhuru wa Benki Kuu. Suala hili la Benki Kuu linaweza likawa linatisha Waheshimiwa Wabunge wengi sana hata baadhi ya watu wengine ambao wanajiuliza ni uhuru kwa ajili ya nini. Lakini nimepitia baadhi ya Sheria za Benki Kuu nyingine; kwa mfano Benki Kuu ya Mauritius, Benki Kuu ya *South Africa* na *Reserve Bank of Australia.* Sheria zao zimeonyesha wazi kabisa kwamba Benki Kuu inapaswa kuwa huru kwa sababu ya kuwa na *authority* ya kufanya *monitory decisions.* Juzi wakati wa semina Mheshimiwa Rostam Aziz alizungumzia mamlaka mbali mbali katika nchi kuhusiana na masuala ya kisera ya kiuchumi akazungumzia kwa Wizara ya Fedha inashughulikia *Fiscal Policies*, Wizara ya Mipango na Uchumi na Uwezeshaji inazungumzia *Development Policies* na Benki Kuu inahusiana na suala la *Monitory Policies.*

Kwa hiyo, kuna umuhimu mkubwa sana wa kuwa na Benki Kuu ambayo ni huru kama jinsi ambavyo ipo katika nchi nyingine. Baadhi ya nchi nyingi Sheria imetaja wazi kabisa kwamba Benki Kuu ni *autonomous* na hakuna sheria nyingine ya nchi ambayo inakuwa zaidi ya hiyo lakini hii yetu kidogo tumeweza kuweka katokana na mazingira ya sheria nyingine kama *Finance Act* na masuala kama hayo.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa nasisitizia hili la uhuru wa Benki Kuu ili kuiwezesha kufanya maamuzi sawa sawa bila kuingiliwa katika masuala mazima ya kifedha. Nadhani kwa wale wanaosoma historia wanakumbuka kwamba tumewahi kuwa na Gavana wa Benki Kuu ya Uganda ambaye Rais wake alimwambia aende tu aka-*print* noti. Hii ni kwa sababu Benki haikuwa huru, lakini unapokuwa na Benki huru hata ukiwa na Rais wa

namna gani bado Gavana atakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi yake kutokana na mazingira ya kiuchumu.

Sasa kuna suala ambalo linazungumziwa sana kuhusiana na Gavana kuwa Mwenyekiti wa Bodi. Kwa suala zima la *checks and balance* ni kitu kizuri sana. Kwa Gavana kutokuwa Mwenyekiti ya Bodi ya Benki Kuu. Lakini jambo nililokuwa naomba tuliangalie kwa upana ni kwamba Benki Kuu siyo shirika kama shirika jingine lolote, sio shirika la uzalishaji. Ni shirika ambalo maamuzi yake zaid ni ya kisera kwa maana ya kwamba *the core-business* ya Benki Kuu sio kutengeneza faida. Faida inatokea kutokana na biashara mbalimbali ambazo zinafanyika lakini sio *core- business*. *Core-business* ya Benki Kuu ni ku-*maintain stability* ya thamani ya fedha yetu na vile vile kuhakikisha kwamba Benki Kuu inasaidia sera za kiuchumi za nchi.

Kwa hiyo, unapokuwa unachukua mtu mwingine kuja kuwa Mwenyekiti wa Bodi yaani aje kuwa juu ya Gavana tutaingia kwenye matatizo makubwa sana kwenye uhuru wa Benki kuu kufanya maamuzi yake ya masuala ya *monitory policy*. Kwa hiyo, mimi nilikuwa napenda nishauri Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuliangalie hili kama ni *specific* tusichanganye suala la Benki Kuu labda kama kampuni nyingine yoyote hili ni suala la msingi sana kwa sababu ni suala nyeti. Kwa hiyo mimi nilikuwa napenda kuwashauri kabisa Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba tuangalie kwamba ni sawa sawa kabisa kwa Gavana wa Benki Kuu kuwa Mwenyekiti wa Bodi kwa ajili ya kumpa yale mamlaka ya kuweza kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nilikuwa napenda kuchangia kuhusiana na suala zima la *share capital.* Sheria yetu nadhani kipengere cha 27, kinazungumzia kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiyo pekee ambayo imechangia *share capital* ya Benki Kuu. Lakini taaria mbalimbali zinaonyesha kwamba Benki Kuu imekuwa ikitoa gawio kwa Serikali zote mbili kwa kiwango cha Serikali ya Zanzibar asilmia 4.5 na Serikali ya Jamhuri ya Muungano asilimia 95.5 kama nitakuwa niko sahihi kwenye takwimu.

Sasa kama mchangiaji katika mtaji ni mmoja iweje *dividend* igawiwe kwa wawili? Kwa hiyo mimi nilikuwa nashauri kwamba Sheria kile kipengere cha 27 kiweze kuweka wazi kabisa wachangiaji wa mtaji wa Benki Kuu ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ili kuweze kuwa na *legality* ya kugawa gawao, tukiacha hivyo ipo siku anaweza kuja Gavana anaweza kusema kwamba sitoi gawio Zanzibar kwa sababu Zanzibar sio *share holder* wa Benki Kuu. Kwa hiyo mimi nashauri hili ili tuweze kuliangalia na vilevile tufuate ushauri na wataalam wa *IMF* mwaka 1994 kuhusiana na suala zima la *share holding* hasa kutokea kule kwa *East African Currency Board* ambao huwa nadhani kwa njia nyingine imekuwa inachangiwa na baadhi ya wajumbe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala hili la *allowances* kupangwa na Bodi yenyewe. Hili linabidi tuliangalie kwa makini kidogo. Kwa kuwa tayari Sheria inatoa uwezekano wa Gavana wa Benki Kuu na Waziri wa Fedha kushauriana mara kwa mara *consultation* ni vema kabla ya Bodi kupitisha au baada ya Bodi kupitisha hizi *allowances* na malipo mbalimbali basi Waziri wa Fedha aweze ku-*authorize at least* kuwe na jicho

lingine la kuweza kuangalia badala ya wajumbe wale wa Bodi kuweza kuangalia kila kitu wao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni kuhusiana na suala la Manaibu Gavana wa Benki Kuu. Baada ya maelezo ambayo nimeyapata kuhusiana na majukumu ya Benki Kuu mimi nakubaliana na kabisa na wazo la kuwa na Manaibu Magavana watatu. Lakini nilikuwa na ushauri na ili tupate uzoefu kutoka nchi nyingine kwa mfano; *Reserve Bank of South Africa* nayo pia ina Magavana watatu. Lakini *Reserve Bank of South Africa* Sheria yao imeweka wazi kabisa kwamba kutakuwa na *Senior Deputy Governor*. Mimi nilikuwa nashauri tuweze kuchukua hili pia sio vibaya kuiga kwa wenzetu, kwamba Sheria iseme wazi kabisa kwamba kati ya hawa watatu mmoja atakuwa ni *Senior Deputy Governor* na huyo *Senior Deputy Governor* basi kama *Governor* anatoka upande mmoja wa Muungano huyo *Senior Deputy Governor* atoke upande wa pili wa Muungano.

Benki Kuu ya Mauritius ina ma-*Deputy Governors* wawili, mmoja anaitwa *First Deputy Governor* na mwingine anaitwa *Second Deputy Governor.* Hii inasaidia kuweza kuweka ile *hierarchy* katika utendaji badala ya kuweka Ma-*Deputy Governors* watatu halafu Gavana anawapangia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ndiyo baadhi ya vitu ambavyo nilitaka nivichangie na nakushukuru sana kwa nafasi hii na ninaunga mkono Sheria yetu hii mpya ya Benki Kuu na nilikuwa naomba Bunge letu lipitishe kwa asilimia mia moja, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nitoe mchango wangu kidogo kwenye hoja hii.

Kwanza napenda kuipongeza sana Serikali kwa kuleta Muswada huu wa Benki Kuu ili uweze kurekebishwa na uende na wakati tulionao. Vilevile napenda kumshukuru sana na kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa taarifa yake nzuri na awali ya yote kabisa nasema naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine Serikali ingeeleza vizuri zaidi hadhi ya Benki Kuu. Benki Kuu mimi ninavyoelewa sio Shirika la Umma wala sio Idara ya Serikali. Ni namna ya Mamlaka ambayo inanafasi yake katika uchumi kwa hiyo huwezi kulinganisha na chombo kingine chochote kile. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hata haya mabadiriko yanakuja kwa msingi huo, kwamba Benki Kuu ni chomba kikuu kimewekwa mahali kinashauri na kusimamia sera za mambo ya fedha; na pamezungumziwa suala la uhuru wake, *antonym* au *independence*.

Hiyo hadhi yake ndiyo inaipa uhuru huo kwamba iko mahali sio shirika kwa hiyo hakuna sheria nyingine inayohusu *BOT* isipokuwa Sheria hii ambayo tunaizungumzia.

Kwa kweli *independence* au *antonym* ya Benki Kuu kiutekelezaji itakuja kuonekana vizuri sana wakati Serikali hizi mbili zinapotaka zipewe msaada au *advances*. Maana yake kama hakuna uhuru basi ni kupeleka tu barua toa hiki lete huku.

Sasa uhuru tunaozungumza ni huo, uhuru wa kutoa maamuzi ya kitaalam kwa maana ya maamuzi ya fedha na kwa kuwa Benki Kuu ya nchi haina tofauti na Benki Nyingine na kuna mambo ambayo yanataikiwa yaende sawa sawa na jinsi mabanki mengine *Central Banks* nyingi za nchi nyingine zinavyoendeshwa

Mheshimiwa Naibu Spika, jana wakati wa kutoa Michango Msemaji wa Kambi ya Upinzani alizungumzia suala la Zanzibar kutonufaika na mapato ya vyomba vya Muungano.

Vilevile kuna hoja zimetolewa hapa kuhusu chombo ambacho kimeundwa kwa jina la Tume ya Pamoja ya Fedha ya Muungano. Sasa napenda ku-*declare interest* kwamba mimi ni Mwenyekiti wa Tume hiyo na nitasaidia kutoa maelezo kuhusu Tume hii.

Tume hii ya Fedha ya Pamoja ya Muungano imeundwa kwa Sheria Namba 14 ya mwaka 1996 na Sheria hiyo imetokana na muafaka ulifikiwa na pande mbili za Muungano kuhusu masuala mbalimbali ya Muungano. Kwa hiyo, ikatungwa Sheria hiyo mwaka 1996 lakini utekelezaji wake ulitekelezwa au iliteuliwa mwaka 2003 na kuanza kazi mwezi Julai, 2003.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniruhusu ninukuu majukumu ya Tume hii ambayo iko katika Katiba Ibara ya 134 ambayo inasema hivi: “Kutakuwa na Tume ya pamoja ya fedha yenye wajumbe wasiozidi saba ambao watateuliwa na Rais.” Kwa mujibu wa ibara hii na masharti ya sheria iliyotungwa na Bunge na ndiyo sheria namba 14 niliyoitaja. Kwa hiyo. majukumu ya Tume kisheria ni kama yafuatayo:-

Majukumu ya tume yatakuwa ni kuchambua mapato na matumizi yanayotokana ua yanayohusu utekelezaji wa Mambo ya Muungano na kutoa mapendekezo kwa Serikali mbili kuhusu mchango na mgao wa kila mojawapo wa Serikali hizo. *(Makofi)*

Kuchunguza kwa wakati wote mfumo wa shughuli za fedha wa Jamhuri ya Muungano na pia uhusiano katika mambo ya kifedha kati ya Serikali mbili. Jukumu la tatu ni kutekelezwa kwa majukumu mengine ambayo Rais ataipatia Tume au kama Rais atakavyoagiza na kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge.

Sasa Sheria hii pamoja na Katiba imeeleza wazi kwamba Tume hii ni ya ushauri. Kwa hiyo, Tume yetu ina tatizo kwamba haiwezi kutangaza kitu chochote, ni Tume ya ushauri inashauri Serikali hizi mbili. Kwa hiyo, Serikali mbili ndiyo zenye jukumu kwa ushauri utakaotolewa. Kwa hiyo, tulipenda ieleweke hivyo isije ikasemwa kwamba Tume hii haifanyi kazi kwa sababu haitangazi mambo inayoyfanya. Tunashauri Serikali hizi mbili. Kwa hiyo, ni Serikali zenyewe baada ya kukubaliana ndizo zinatoa maelezo kwa wananchi. *(Makofi)*

Tume hii ina wajumbe kama nilivyosema saba, watatu kutoka Zanzibar, watatu kutoka Bara halafu na Mwenyekiti ambaye ni huyu Shellukindo anayezungumza hapa. Sekretarieti yake Gavana wa Benki Kuu ni mmojawapo katika hiyo Sekretarieti. Mwingine ni Kamishina Mkuu wa Mamlaka ya Mapato wa Serikali ya Muungano halafu na Mkurugenzi wa Bodi ya mapato wa Zanzibar. Hiyo *high power expertise* iko hapo. Sasa Tume hii inahusika sana na Muswada huu wa Benki kwa sababu inahusiana na mambo ya fedha na iko karibu sana na hawa hawa ambao wanashughulikia masuala ya sera za mambo ya fedha na kadharika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Zanzibar ilikuwa inachangia mambo ya Muungano lakini ilikoma kuchangia mwaka 1985 na hoja ni kwamba watachangia tu Tume itakapoundwa na kutoa ushauri. Kwa hiyo, Tume iliundwa, sheria yake ilitungwa baada ya muafaka kufikiwa mwaka 1994. Muafaka wa mambo ya Muungano likiwemo na suala hili la kuchangia gharama za Muungano na vilevile kugawana mapato ya Muungano. Kwa hiyo, Sheria ilitungwa mwaka 1996, Tume iliteuliwa mwaka 2003 na kuanza kazi Julai, 2003. *(Makofi)*

Kwa kweli hakukuwepo na Tume, lakini katika Kipindi hicho kuanzia Mwaka 1994 baada ya kupata Muafaka Zanzibar walikuwa wanapata mgao wa Benki Kuu na ulianza kutolewa baada ya Zanzibar kukubali Benki Kuu kuwa Benki yake. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kustahili kupata gawio, gawio hilo limeweza kutolewa kuanzia mwaka 1994 kwa maana ya mwaka wa fedha wa 1994/1995 hadi mwaka 2004 kwa Bajeti ya mwaka wa fedha 2004/2005. Ukijumlisha hayo mapato yake au gawio hilo kuanzia mwaka huo wa 1994 mpaka 2005 Juni, Zanzibar imepata shilingi 3,679,000,000 kwa jumla. Hiyo ni sawa sawa na asilimia 4.5 ya gawio la Benki Kuu la shilingi 81,765,000,000. Kwa hiyo, hakuna kupunjika hapa! Hii ni kwa mujibu wa *formula* hii ya asilimia 4.5 iliyotumika. Suala hili limetokana na ushauri wa Shirika la Fedha la Kimataifa *(International Monetary Fund)* na uamuzi huo wa ushauri ukakubaliwa na Serikali zote mbili na ukaanza kutumika na unatumika mpaka sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume hii kwa maana Zanzibar waliacha kuchangia mwaka 1985 kungojea Tume iundwe. Tume imeishaundwa na imeanza kazi. Kwa hiyo, kwa taarifa hii nadhani kwa kweli hakuna mtu ambaye anapunjika hapa, isipokuwa tu ni kwamba hicho kigezo cha asilimia 4.5 kiliwekwa wakati huo na Tume imeundwa na inafanya kazi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi zilizofanywa na Tume mpaka sasa hivi kwanza ni kuainisha Idara na Taasisi za Muungano. Hiyo ni moja, uzijue. Pili, Tume imechanganua gharama za Muungano tangu mwaka 1994 mpaka mwaka 2004/2005 ili baadaye iwe msingi wa kuweza kuangalia namna ya kuchangia. Vile vile, Tume imeainisha madeni ya pande zote mbili, ndiyo kazi iliyofanyika hiyo. Halafu Tume imepitia sheria namba 14 ya mwaka 1996 ambayo ina mapungufu mengi kwa sababu ilitungwa mwaka 1996 na Tume imeundwa mwaka 2003, hivyo kuna mabadiliko mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi nyingine ambayo imefanyika sasa ni kuchambua na kuchanganua vigezo vipya. Kazi hiyo imefanyika kwa kufanya yafuatayo:-

Kwanza, Tume imekwenda kupata uzoefu wa nchi ambazo zina namna ya Muungano kama wa kwetu. Tume imetembelea India, Australia na Finland. Finland kule kuna kisiwa kimoja kinaitwa Aland ambacho kipo mbali sana na Finland, wana ushirikiano au Muungano wa namna hiyo. Tumetembelea Uingereza na Spain. Spain kuna visiwa vinaitwa Canaries kule, kwa hiyo, wana Muungano huko, kwa hiyo, Tume imejielimisha. Sasa hivi ameteuliwa *International Consultant* wa kuchambua gharama hizo. Tumepata mtu ambaye hana upande wowote ili kuweza kuishauri Tume. Kwa hiyo, kazi hiyo imeanza. Sasa itakapomalizika ndipo Tume itatumia uzoefu ilioupata katika nchi hizo na ushauri wa huyu mshauri wa kitaalam ambaye ni wa Kimataifa ndipo sasa tutakaa, tutaishauri Serikali nini kifanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliona nilitoe hili ili kuondoa hisia kwamba kuna nia labda ya kupunja upande mmoja au upande mwingine. Kwa hiyo, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii, nadhani mengine hayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha ambaye ndiye kiungo chetu pamoja na mwenzake wa Zanzibar wataweza kusaidia kutoa maelezo mengine. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Awali ya yote naomba msamaha kwamba wakati uliponiita sikuwepo, nilikuwa nina simu ambayo ilikuwa ni lazima nizungumze na watu wa kutoka kwenye Jimbo langu. Kwa hiyo, samahani sana kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nataka kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia katika Muswada huu ambao ni wa maana sana katika uchumi wetu na zaidi wakati huu ambapo mambo mengi ya kifedha yanaenda kitaalam na pia yanaenda katika hali ya teknolojia mpya ambayo ni *electronic systems.* Kwa hiyo, ni vizuri tukaujadili huu Muswada na kupitisha uamuzi ili na sisi kama Watanzania tuweze kuwa katika wigo wa watu ambao wanaendesha mambo yao ya kifedha katika hali ya kisasa. Kwa hiyo, nashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili nataka kutoa pongezi nyingi sana kwa Kamati iliyoshughulikia Muswada huu. Nafikiri wamefanya kazi nzuri sana na Muswada sasa unavyoonekana ni mzuri zaidi kuliko ulivyokuja. Lakini pia nitakuwa nakosa fadhila nisipomtaja Waziri kwa jinsi alivyoueleza Muswada huu kwa lugha ambayo inaeleweka kwa kila mmoja na siyo lazima uwe *banker* ili kuelewa kuna kitu gani ambacho kinahitajiwa. Bila shaka ni lazima pia tuwataje Katibu Mkuu wa Wizara hii amefanya kazi nzuri, pamoja na wataalam wa *Bank of Tanzania.* Nina hakika nia yao ni nzuri. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo nataka kusema jambo moja tu la utangulizi ambalo lilijitokeza jana. Tuna Kambi ya Upinzani, lakini ningependa hii kambi ijulikane kama kambi rasmi au *CUF,* maana baadhi ya mambo ambayo yanasemwa hatukubaliani nayo.

Kwa hiyo, yanaposikika kwa wananchi kwamba ni Kambi ya Upinzani imesema hivi, basi inaonekana kama wote tumesema namna hiyo. Kwa hiyo, hili niliona niliweke wazi kabisa ili tusiwe tunachanganywa kwa mambo ambayo siyo mawazo ya kila mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, basi naomba nijikite sasa kwenye Muswada. La kwanza kabisa ambalo napenda kuzungumzia ni juu ya uhuru wa benki hii ambayo ndiyo tunaizungumzia leo. Nakubali na ni kweli kwamba hii benki ni lazima iwe mahiri na ni lazima iweze kupewa nafasi ya kufanya kazi. Lakini pia natahadharisha kwamba hakuna uhuru usiokuwa na mipaka na zaidi kwa benki kama hii ambayo fedha zote tunazokusanya kama kodi zinaingia katika benki hii. Malipo yote ya Serikali yanafanywa na benki hii. Malipo yote yanayofanywa na wafadhili wetu yanapitia kwenye benki hii na siyo hivyo tu, benki hii ndiyo inaangalia sera ya fedha ambayo pia ni sera ya Serikali.

Kwa hiyo, badala ya kufikiria tu uhuru usiokuwa na mipaka ni vizuri tukasisitiza pawepo na uhusiano wa karibu sana kati ya benki na Wizara ya Fedha ili iwe wazi kabisa. Mambo hayaendi kama vile tunatengeneza Wizara ndogo ya Fedha iliyo sawa na Waziri wa Fedha. Ni lazima hili jambo lisisitizwe ijulikane kwamba *Bank of Tanzania* ni chombo muhimu kinachotumiwa na Serikali. Kwa hiyo, chombo hakiwezi kuwa moja kwa moja ni huru na kwamba hakina uhusiano wa karibu zaidi na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, imefurahishwa katika *section* ya 13 kwamba Rais anamchagua Gavana na kwamba Waziri wa Fedha atashirikiana katika *consultation,* siyo kuarifiwa, bali kuweza kuzungumza mambo yanayohusu benki hii na kwamba *Permanent Secretary* wa Wizara pia naye yumo ndani ya bodi. Nafikiri hizi ni nyenzo za kuhakikisha kwamba kuna uhusiano wa karibu sana kati ya Serikali na benki. Kwa hiyo, ni uhuru ambao una *limitation,* siyo uhuru wa moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo nataka kukazia ni kuhusu ukaguzi. Nimefurahishwa sana kuona kwamba angalau imetamkwa bayana sasa katika Muswada huu kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali sasa atakagua mahesabu ya benki hii. Nilikuwa nashangaa kwa muda mrefu kwamba fedha za Serikali zimo ndani ya benki hii na ni pesa zetu, lakini mkaguzi anateuliwa tu na bodi! Sasa kwa kuingiza *CAG,* naona inakidhi mahitaji na *CAG* akiwa ndiyo jicho la Bunge na sisi tunaangalia fedha hizi za Benki Kuu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hapa nikazie jambo moja kwamba katika ukaguzi wa kisasa kuna uwezekano wa kuwa na teknolojia ambazo ziko juu sana katika Benki Kuu ambazo hazimo katika Idara ya *CAG* katika Serikali.Basi hapa ningeshauri kwamba *technological development* au maendeleo yoyote ya kihasibu ahusishwe Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ili ajue ni kitu gani atakachoenda kuangalia ili usije ukakuta kwamba Benki Kuu kiteknolojia iko hapa na Mkaguzi hayupo katika *level* ile inayotakiwa, ikibidi basi, itatakiwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu aweze kutumia watu wa nje ili kuhakikisha kwamba ile kazi inafanywa kufuatana na *International Standards*

na pia kufuatana na teknolojia iliyoko kwa sasa hivi. Katika *development* ya *technology,* ningeshauri uwe mkubwa zaidi na *CAG.*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningependa kukazia mambo yafuatayo, kwanza nimeangalia na nimefurahishwa na hii *section* ya 17 inayozungumzia juu ya *capital* au *shares* za benki hii. Nilikuwa nashangaa kwamba benki hii kwa muda mrefu imekuwa na *share capital* ya *10 billion,* lakini ukiangalia *reserves* ni bilioni 353 ambayo ni karibu asilimia 2 tu ya *reserves* zilizomo ndani. Ningeshauri kwamba hiyo *capital* ambayo imetajwa kisheria kuwa iwe bilioni 100, basi iongezwe mara moja ili kweli ifanane na ukubwa wa benki kama tunavyouangalia kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo ningependa kukazia juu ya benki hii ni matumizi. Matumizi ya benki ukiangalia katika *balance sheet* yake unaona ni matumizi makubwa sana kwamba matumizi ya mwaka jana kwa mfano 2005 ni bilioni 86.8 na mwaka uliopita ni bilioni 64.5, hii ni sawa sawa na madarasa karibu 30,000 ya watoto wa shule. Sasa hali kama hii mtu unajiuliza haya matumizi yataendelea kupanda mpaka wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia sasa hivi kweli tuna majengo makubwa na ofisi nyingi katika majengo marefu na mazuri ambapo pia na mimi nimeyatembelea. Lakini dhana isiwe kuongeza tu watu halafu unaongeza gharama za kuendesha hii benki. Naona kuna haja ya kuangalia kikomo fulani cha matumizi na ni matumaini yangu muundo mpya utahakikisha kwamba benki kwa sababu ina uhuru isiendelee kutumia tu, kutumia tu. Ikiendelea kutumia, ndiyo kusema kwamba gawio kwa *shareholder* litakuwa ni dogo na tayari katika mwaka huu imeonyesha kwamba gawio lililokuwa bilioni 127 mwaka uliopita sasa hivi limeshuka mpaka bilioni 9. Kwa hiyo, mtu unashangaa kinafanyika kitu gani katika benki hii!Kwa jinsi tunavyosisitiza juu ya uhuru, sijui itakuwa namna gani!

Mheshimiwa Naibu Spika, naona kuna haja ya Waziri wa Fedha kutueleza kwamba uwekezaji kwa mfano wa majengo hayo mawili umegharimu fedha kiasi gani na fedha hizi zimetoka wapi. Kwa sababu watu wanapita pale, wanaweza kuwa na mawazo ambayo ni potofu na siyo vizuri. Mimi nimetembelea hayo majengo, kiufundi imefanyika kazi nzuri sana, lakini Watanzania tuna haki ya kufahamu tunaelekea wapi na kama matumizi hayo yaliidhinishwa na Bunge au namna gani au kwa dhana hiyo hiyo ya uhuru basi mtu anabuni miradi ambayo ni mikubwa sana. Pia ningeongeza hapa kwa kusititiza kwamba Bunge hili lingehusishwa kwa njia moja au nyingine, labda kwa njia ya Bajeti juu ya matumizi makubwa zaidi, kama ni matumizi ya uwekezaji wa majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ambalo ningependa kukazia ni mchango wa benki hii kwa wakulima. Kama ripoti ya Benki Kuu inavyosema, kweli wana ripoti nzuri sana kwamba asilimia 46 ya *GDP,* mapato yote ya Taifa yanatokana na wakulima. Basi hii benki ingejiona kwamba ni benki ya wakulima. Kama ile wanayozungumzia juu ya sera zao za kifedha, basi akili nyingi zaidi na utafiti mwingi zaidi uwekwe ili kuhakikisha kwamba wakulima kweli wanasaidiwa. Kwa mfano, ukiangalia kama wakulima wa pamba ndiyo wale ambao wanawaletea fedha za kigeni katika nchi hii,

wakulima wa kahawa ndiyo hivyo wanaleta fedha za kigeni katika nchi hii na pia ndiyo wanapunguza sisi kutegemea watu wa nje katika mapato yetu ya fedha za nje. Kwa hiyo, ningependa hilo jambo liwekewe umuhimu sana katika muundo mpya wa benki yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo mawili mengine ambayo ningependa kusema kwa haraka. Jambo la kwanza ni udhibiti wa wageni wanaokopa katika *banking systems* zetu. Kuna nchi nyingi ambazo haziruhusu jambo hilo. Mgeni anakuja tu na *briefcase* yake, akifika pale hana chochote anaingia kwenye benki na zaidi kwa sababu ubaguzi wa rangi bado upo, tupende tusipende mtu ukienda mweusi utaonwa wewe hukopesheki, mtu akienda mweupe wanasema: *"yaah, this one you know* ana *qualification* za kupata *lending."* Sasa hali kama hii tumeona katika nchi yetu ambapo watu wameingia humu hawana chochote lakini wamepata mahoteli, wamepata biashara kubwa kubwa, wamepata pia viwanda kwa kupitia *assets* zetu hapa hapa ndani! Sasa kama yeye ni mwekezaji ameweka kitu gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, haya mambo ya *bank transfers* mara nyingi tumeona kuna wizi kila wakati. Hivi ni kwa nini watu wanaleta fedha kama vile unapeleka mafurushi? Katika utaalam wa sasa hivi hakuna njia kwamba fedha hizi zote zinaweza zikawa *transferred* kwa *Bank of Tanzania electronically* kwa njia ambazo zinajulikana kabisa kiulimwengu kuliko kukodi ndege? Ndege inaleta fedha, kumbe watu wamefanya utaratibu kule kwamba ndege itafika wakati gani na nani anaileta, njiani fedha zinakwenda. Tumeishaona matukio haya ambayo yameishatokea tayari. Ningeshauri kwamba *Bank of Tanzania* iliangalie suala hili ili pasiwe na upotevu usiokuwa wa lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa napenda kusema kwamba pawepo na usimamizi mkubwa zaidi katika baadhi ya mabenki. Naambiwa kwamba kuna baadhi ya mabenki wanafunga hesabu zao nje ya nchi. Sasa kama unafunga *balance* zako nje ya nchi pakitokea na kutoelewana kati ya nchi hizi itakuwaje? Hizi benki mara nyingine ni *lead banks.* Kwa hiyo, tungependa kuona usimamizi ule wa karibu zaidi ili tuhakikishe kwamba kweli tunaendesha uchumi huu sisi wenyewe kwa kupitia benki hii mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii pia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nitoe mchango wangu kuhusu Muswada huu. Naomba nitamke rasmi kwamba Muswada huu ninauunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri wa Fedha kwa kazi nzuri aliyoifanya katika kuelezea Muswada huu. Lakini nampongeza pia kwa marekebisho machache ambayo yeye na wenzake wameweza kuyafanya kuuboresha Muswada huu na nampongeza sana Gavana wa Benki Kuu kwa maelezo aliyoyatoa mbele ya Kamati ya

Bunge ya Fedha na Uchumi. Nawapongeza Makatibu Wakuu wa Wizara za Fedha za Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ambao wote kwa pamoja walihudhuria katika vikao vya Kamati ya Fedha na Uchumi na ninawapongeza wale wataalam wote waliokuja wakatuelekeza jinsi Muswada huu unavyofanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi na nilihudhuria baadhi ya vikao vilivyoendeshwa kujadili Muswada huu.Kwa hiyo, nakubaliana sana na maneno yote aliyoyazungumza Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi. Ninampongeza sana Mwenyekiti kwa sababu amejitahidi sana kuweka yale mambo yote pamoja na kuja nayo kama alivyoyazungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala moja ambalo nafikiri nilizungumzie ni *issue* ya *independence* ya benki. Suala hili ni *universal,* lakini wakati nilipokuwa nasoma Muswada huu na nikajaribu kulinganisha kinachoendelea katika nchi nyingine nilielewa kwamba kuna *degrees* tofauti za *Central Bank Monitoring* ambayo inahusiana na maendeleo ya *Financial and Banking System* ambayo ipo katika nchi. Sasa mahusiano hayo ndiyo ambayo ni lazima Wizara itueleze vizuri yatakuwaje kwa jinsi ambavyo hii *bill* ilivyotengenezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma kipengele kile cha *Monetary Policy Management* ambapo ukienda kifungu kile kinachozungumzia madaraka ya Gavana wa Benki na wale wenzake, ukikisoma kifungu kile cha 13 vizuri ndiyo unajua kwamba haya tunayozungumza na ninaomba ninukuu vile viwili 13(1) na 13(2) vinasema: *"Subject to the provisions of this Act, the management of the Bank and the direction of its business and affairs is vested in the Governor and the Governor shall, in the exercise of such functions and direction, conform with the policy and other decisions made by the Board."* Namba mbili kinasema: *"The Governor shall, unless the Board determines otherwise, exercise powers, perform functions and execute duties of the Bank, other than any function specifically conferred on the Board, and to authorize expenditure within the budged approved by the Board."*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma Muswada zaidi ni kwamba, pamoja na kuwa tuna Wakurugenzi nane wanaokaa pale ambao wanapiga kura, maana wale wawili hawapigi kura, kifungu hiki kilitupa taabu sana ndani ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mawazo yaliyokuja yalikuwa kwamba kama wako nusu kwa nusu na una *Deputy Governors* watatu na Gavana mwenyewe wa nne, wale wakati mwingine wanaweza kuona hakuna haja ya kumuita mtu ambaye ni *external. External member* anaweza asiitwe maana wako wanne na wao wako wanne na wana uwezo wa kuamua mambo ndani ya benki na wataamua na hakuna mtu atakayekuja kuuliza kitu hapa, eti benki ilifanya hivi. Aaah, tuliwapa madaraka sisi wenyewe, kwa hiyo, kama tunawapa sisi wenyewe tujue tunawapa. *Deputy Governors* watatu na Gavana wa nne wanaamua mambo. Mfano tuhamishe mabilioni ya fedha ya nchi hii tupeleke ng'ambo, huyu Daudi Balali hataendelea kuwepo, ni mzuri na tunampenda.Tulichokisema ni kwamba, *it cannot be.* Tukasema tunapendekeza Magavana wawili *for now* mpaka Wajumbe wa Bodi watakapopatikana ili wasiamue mambo kama hakuna Mjumbe wa nje ambaye yuko mle ndani.

Waheshimiwa Wabunge, kama tunasema hii sawa, ni sawa. Lakini likitokea jambo tusiseme ni Gavana, atawajibika kwa nani? Maana humu ndani hakuna mahali panaposema atakuja Bunge kuwaelezeni ninyi. Uwezo wa kitaratibu upo, ataitwa kwenye Kamati ya Bunge inayowawakilisha ninyi ndani ya Bunge hapa, lakini utaratibu wa sawa sawa wa kisheria haupo, ni hiyo *independence* ya benki inayozungumzwa. Ndiyo maana tunasema ni kweli tunampa madaraka. *Independence* ya benki *has always been there.* Hakuna wakati ambapo benki haikuwa na *independence.* Ilikuwepo wakati wote. Kama tunazungumzia *magnitude, that's a different matter,* lakini hiyo ilikuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *we have witnessed* mabenki mengi ndani ya Afrika yanahamisha pesa ovyo. Naweza kuwapa mfano, miaka iliyopita tulikuwa na njaa kama hivi hivi *in the seventies,* mimi nilikuwa Marekani mwaka 1976. *That is in the record, you can go and find out.* Watu wamepeleka madudu kwamba chakula kinanunuliwa mahali ambapo pesa zimeshalipwa, lakini pesa nyingine zinapelekwa huko *South East Asia* na nchi nyingi za Afrika zinafanya. Nigeria ni nchi inayojulikana, lakini ni nchi nyingi zinafanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulichokuwa tunasema kwenye hii ya *Management of the Bank and Powers of the Governor and Deputy Governors* ni kwamba hapana, kuwepo na *balance,* wale wa nje walingane na hawa wanapokaa. Ndiyo maana tukapendekeza kwenye Kamati kwamba *Deputy Governors* wawe wawili na tukawagawanya. Tukasema *Policy and Operations* mmoja halafu *Finance and Administration* mwingine mmoja. Sasa *Deputy Governors* watatu ni wengi kama hizo shughuli za benki zinaendelea kwa kiwango hicho, maana shughuli haziongezeki kwa mara moja, zinaongezeka kwa taratibu. Huo ni ushauri wangu, sisi tuuelewe kama Wabunge, lakini hilo lipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama *Monetary Policy and Management* ikienda vibaya, ikishindwa, *we have a problem.* Sisemi itashindwa, lakini ikishindwa *we have the problem.* Watu wa benki wenyewe wakipoteza mwelekeo tunalo tatizo maana watawajibika kwa nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Gavana Daudi Balali ni mnyenyekevu kweli, lakini mwingine atakwenda kukaa na Waziri anaweka miguu hivi, atafanya. *Let's be honest. We all have an interest in the development of this country. Let's be frank.* Hii ndiyo *tool* kubwa ya *management* ya nchi hii, *Management and Policy.* Sasa sisi tunaichukua *because* pengine hatuelewi vizuri kinachoelekea. Naomba niseme hivi, wawe wanatueleza. Hata kama *IMF* inasema watueleze kwamba jamani hapa wakubwa wanatusukuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unafika mahali unasema hutaki Katibu Mkuu apige kura hata kwa kile anachokiona ni *of interest to this government!* Unasema asipige kura kwa sababu hao wakubwa hawataki kwenda Wizarani wakazungumze na Katibu Mkuu, wanataka kwenda moja kwa moja Benki Kuu! Watasaidia kutuchagulia *Central Bank Governors,* utafanya nini? Wakisema huyu hatumtaki, wakimleta tusiyemtaka itakuwaje? Balali tunamtaka, tunampenda, lakini huyu hayupo kesho na keshokutwa,

watakuchagulia mwingine usiyemtaka atafanya ya wale, wewe utafanya nini? Miaka mitano atakaa pale wewe unafuata tu hayo anayoyataka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo nimeyasema ili tuelewane, lakini ipo mifuko inaundwa chini ya hili, maana yako mengi ningeweza kusema. Iko mifuko inaundwa. Ile mifuko sisi tuliweka tahadhari tukasema mifuko hii ni mizuri kwa maendeleo ya Taifa hili kama huyu atakayekuja atafanana na huyo Gavana Daudi Balali. Lakini inawezekana asifanane naye lakini tunahitaji maendeleo. Tumezungumzia habari ya *financial institutions* ambazo zinatakiwa ziwe *created* hapa mambo ya *development institution, mortgage finance institutions etc* ambazo kwa kweli nashukuru sana kama mmezielewa na ninyi tunavyoziona ziwepo zitusaidie kuleta maendeleo ya nchi hii. Hakuna nchi inayoendeshwa bila *development financial institutions* katika sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kikubwa kinachowagusa Watanzania walio wengi na ambao ndio sisi tunaowawakilisha wakulima na wananchi wetu wa kawaida wanaohangaika kila siku hakuna Mabenki wanabeba fedha wanaporwa njiani. Uundwe mfuko usaidie basi hizo *SACCOS* zifanye kazi nzuri ya kuhudumia wananchi. Haiwezekani mtu anabeba milioni tano, kumi kijijini huko lazima ataporwa hakuna Benki. Ni sehemu nyingi nilisikia mtu mmoja huko nadhani Lindi au Mtwara alikuwa anapeleka fedha Benki akaporwa zote njiani eti anakimbia Benki kilometa 70, zote zikaibiwa. Hana hata *insurance.* Mtusaidie mifuko hii ifanye kazi hiyo. *(Makofi)*

Lakini pili, tunahitaji *development* ya *micro finance* katika Taifa hili, *development* ya *micro finance* ndiyo itakayowasaidia wananchi wetu ndani ya nchi hii. Iende ikawasaidie utaalam ninyi ndiyo wa kutusaidia kuukuza. Benki Kuu itusaidie kukuza utaalam wa *micro finance* tupo nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho *interest rate* za nchi ziko juu sana. Tunasema tunataka kwenda na nchi jirani kama wanavyofanya, tunapewa mifano Zambia Magavana watatu, nani watatu, sijui wangapi, tufanye mambo kama sisi tunavyoyaelewa. Tumesoma tuna utalaam, tunaelewa tufanye haya yanayohusu nchi yetu. Gavana Balali *in his words* alisema sisi tuko *primary school* wenzetu wako Chuo Kikuu, unajilinganishaje wewe uko *primary school* na mwenzako yuko *university* ukafanya mambo sawa sawa na huyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tufanye mambo kama watu tunaotaka kwenda mbele, *when the time comes* hayo yanayofanana na *university* tutayafanya. Sasa tuko *primary school,* tujenge *infrastructure* ya ki-*primary school* ili tufike huko, ndiyo! Ndipo tutakwenda, lakini haya mambo ya leo mtu *is exhausted* analeta mambo humu Bungeni hapana! Mimi nafikiri na sisi tuwe *scientific, scientific* kwa maana tufanye mambo yanayolingana basi na huo utaratibu wetu, ukiwa-*push* watu sana nao hawataelewe ninyi mtakuwa mbali sisi tuko chini hatuelewi mnachofanya ndani ya Benki Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayasema haya kwa sababu ni ya muhimu sana kwa Taifa letu. Ninaiomba Benki Kuu, ifanye *review* ya *interest rates* zote katika nchi hii.

Kuhusu *both lending and borrowing* ikishakufanya hayo itupe *assurance* kwamba sera nzima itaangaliwa kwa upana wake na marefu yake ituletee ndiyo haya ya kuendesha uchumi. *Interest* ya 15 inakataza watu kufanya kazi, 15, 20 huwezi kukua hata kama ni mfanyabiashara. Huu utaratibu mwingine wa *policy* kwamba mzungu ndiyo akienda Benki ndiyo anaweza kupata fedha *it is a wrong policy we must refuse it, this is our country* na lazima tuendelee kwa misingi yetu hapa hapa. Utengenezwe utaratibu hizi *refuse* zifanywe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nafikiri siyo kwamba nakuwa mkali, *we are so poor.* Mtu unakuwa maskini lakini siyo maskini, *resources* zimetuzunguka hatuwezi kutengeneza taratibu za kukuza uchumi wa nchi hii. Lazima tuone uchungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Jimboni kwamba unavyoona wale maskini wanavyokuzunguka unalia unatoa machozi, unajiuliza hivi nilichaguliwa kufanya nini? Tunakuja hapa tunajigonga gonga hatuoni mambo yanavyokwenda. Mhubiri kanisani analihubiri neno la Mungu kama lilivyo. Uliendeleze kama lilivyo ili huyo anayetusikiliza ajue kwamba na wewe umeokoka. Wale tuliwadanganya tunakuja kuwasaidia humu ndani tunakuja ooh! Mimi naona sawa kwa sababu nani rafiki yangu acha hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja hii ni nzuri lakini inaweza kuboreshwa zaidi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu inayohusu Muswada wa Sheria ya Benki Kuu wa mwaka 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi ya awali kabisa kuipongeza sana Serikali kwa kuleta Muswada huu mpya hususan nampongeza sana Waziri wa Fedha, pamoja na wataalam wake kwa kuleta Muswada huu Bungeni kwa muda muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda nianze kwa kusema kwamba mimi nakubaliana na maoni na mapendekezo ambayo yametolewa na Kamati ya Uchumi na Fedha, katika marekebisho ya Muswada huu. Pia naunga mkono mapendekezo ya marekebisho ambayo yameletwa na Waziri wa Fedha. Nafikiri mapendekezo haya yanafanya jitihada ya kuboresha Muswada wenyewe. Pamoja na mapendekezo hayo na maoni ya Kamati ya Uchumi na Fedha na mimi napenda nichangie maeneo machache tu kwa lengo la kuboresha Muswada wenyewe. Kabla sijasahau napenda nianze kwa kusema kwamba naunga mkono Muswada huu muhimu wa Benki Kuu ya Tanzania mwaka 2006. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno haya ya utangulizi sasa niende kwenye Muswada wenyewe na mimi nitachangia maeneo mawili tu. Eneo la kwanza linahusu sehemu ya 8 ya Muswada wenyewe. Sehemu ya 8 (1) inatupa utaratibu wa namna Gavana wa Benki Kuu atakavyopatikana, namna ya kumpata kwa maana ya kuteuliwa na pia inaelezea sifa za mtu huyu atakayeteuliwa kuwa Gavana wa Benki.

Mimi napenda niungane na mapendekezo haya na nakubaliana kabisa na sifa zote ambazo zimetajwa wa mtu atakayeteuliwa kuwa Gavana zile sifa zinatosha. Hakuna sababu ya kupunguza. Kama jinsi kauli ya Wabunge walivyosema ni kwamba hii nafasi ni nyeti sana kwa hiyo, tusije tukalegeza zile sifa tukampata mtu mbovu. Ni taasisi nyeti, kwa hiyo, sifa zile pamoja na uzoefu ni muhimu awe nazo. Kwa hiyo, naungana na mapendekezo yaliyotolewa katika Muswada huu.

Lakini tatizo langu lipo kwenye Manaibu Magavana ambao ni sehemu ya 8(3) pale imeelezwa namna hawa Manaibu Gavana watatu watakavyopatikana. Lakini nasikitika kusema kwamba Muswada haujasema lolote kuhusu sifa zao. Sioni mahali popote katika Muswada huu hawa wanatakiwa wawe na sifa zipi. Sijui katika marekebisho ya Waziri nimepitia sijaona mahali popote ambapo sifa zinatajwa za Manaibu Gavana ambazo watakuwa nazo ili waweze kuteuliwa katika nafasi hizi.

Kwa hiyo, sielewi ni kwa sababu gani Muswada huu haukuweza kuainisha sifa za Manaibu Gavana. Hawastahili kuwa na sifa ama ni vipi, ama tumesahau? Nimejaribu kupitia Muswada wote na kuangalia lakini hakuna popote ambapo nimeona sifa.

Waheshimiwa Wabunge wengine wananiambia eti sifa zitafanana na sifa za Gavana, mimi sidhani kama ni kweli. Kwa hiyo, mimi nimesimama kupendekeza kwamba hawa Manaibu Gavana, ambao watateuliwa kumsaidia Gavana basi na wenyewe wawekewe sifa zao. Namna ya kupatikana tumeelezwa katika hiyo sehemu ya 8(3) kwamba watateuliwa na Rais. Lakini sifa zao hazikuelezwa. Naomba kwa dhati kabisa Waziri aliangalie suala hili tena na ikiwezekana na si ikiwezekana na lazima alete sifa ambazo zitamwezesha mtu kuteuliwa kuwa Naibu Gavana wa Benki Kuu. Vinginevyo tutapata watu wabovu na kwa kuwa kazi hii ni nzito na ni nyeti mimi nafikiri ni muhimu hawa watu wawe na sifa zinazostahili. Kwa hiyo, mimi napendekeza kwamba basi sifa za watu hawa watakaoteuliwa kuwa Manaibu Gavana zitajwe katika sheria hii.

Sehemu ya pili ambayo napenda nichangie ni sehemu ndogo tu, sehemu ya 11(8) kile kipengele kilichowekwa pale mimi sioni kama kina sababu yoyote kwa sababu ukiangalia sehemu ya 9(2)(c) inazungumza juu ya watu hao hao. Kwa hiyo, ni suala la kurudia tu. Kwa hiyo, mimi ninachosema hapa ni kwamba badala ya kufanya Muswada uwe mrefu sana kwa kurudia rudia mambo yale yale katika vifungu tofauti mimi napendekeza kile kifungu cha 11(8) kifutwe kwa sababu kimekwishaelezwa katika sehemu 9(2)(c).

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ndiyo yalikuwa maeneo ambayo nilitaka kuyagusia katika Muswada huu kwa nia ya kuboresha. Lakini pia nina mambo ya jumla, kama walivyosema wenzangu Benki Kuu ni chombo nyeti katika Taifa hasa kuhusu uchumi wa nchi hii. Sasa kwa sababu katika sheria iliyopita Benki Kuu haikupewa meno ya kutosha kuweza kutekeleza kazi zake sasa hivi inaonekana kwamba sheria hii itakuwa na meno ya kutosha.

Sasa mimi maombi yangu mawili, la kwanza Benki Kuu ihakikishe kwamba hizi Benki za Biashara zinasimamiwa kwa karibu na kilio kikubwa cha Watanzania ni suala la

riba. Tusimamie riba ili ziweze kushuka na Watanzania waweze kupata fursa ya kukopa na kujiletea maendeleo.

Ombi langu la pili, kwa Benki Kuu baada ya Muswada huu kupita tuangalie namna gani tutapeleka huduma za Benki Vijijini. Hivi sasa huduma zote za Benki ziko Mijini na ndiyo kilio cha wananchi na ndiyo kilio cha Wabunge tulio wengi. Kwa hiyo, mimi naomba utafutwe utaratibu kama ni kupitia *SACCOS* ama Taasisi nyingine za kifedha tujitahidi kupeleka huduma za Benki Vijijini ili wakulima walio wengi waweze kupata fursa kukopa na kuweza kuendeleza kilimo na shughuli nyingine za maendeleo.

Baada ya kusema hayo naomba tena nikushukuru kwa kunipa nafasi na natamka tena kwamba naunga mkono Muswada huu na upite uwe sheria. Ahsante sana kwa nafasi uliyonipa. *(Makofi)*

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia. Mimi mchango wangu ni mfupi sana. Nitaomba nigusie *section 11* ya Muswada huu, kipengele ambacho kinampa ruhusa Mwenyekiti wa Bodi ambaye ndiye Gavana. Kama hayupo Mwenyekiti wa Bodi ambaye ndiye Gavana ni kwamba Makamu Mwenyekiti wake ambaye ni Naibu Gavana, kipengele hiki kinampa uwezo au ruhusa ya kuitisha mkutano kama ataona Mwenyekiti kwa maoni yake ni *(in his own opinion)* kwamba inabidi kuitisha mkutano wa dharura pale ambapo mambo fulani yanajitokeza na ni ya haraka sana.

Kwanza kabisa nilitaka nifahamu hili neno kwamba *where in the opinion of the governor or the chairman* kwamba katika maoni ya Mwenyekiti, inahitajika mkutano huu kuitwa kwa dharura. Sasa hili neno limekaa kwa upana sana kwamba katika maoni yake ni mambo yapi yangeorodheshwa hapa kwa sababu huyu ni binadamu inawezekana jambo ambalo litakuwa katika maoni yake likawa siyo la msingi sana, lakini akatumia nafasi hii kusema kwamba mimi katika maoni yangu niliona mkutano huu lazima uitishwe. Kwa hiyo, ningeomba hii iwekwe vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ya pili, ni kwamba ukiangalia katika *quorum* hii ya kuitisha mkutano wa dharura unawapa nafasi Mwenyekiti ambaye ndiye *Governor* kama hayupo Naibu wake. Ni wajumbe watatu tu ambao wanapewa nafasi hii ya kuitisha mkutano huu Gavana mwenyewe, Naibu mmoja na Naibu wa pili wanakuwa *quorum* ya watu watatu. Hawa ndiyo watendaji wakuu wa Benki Kuu. Wanapokaa hawa wana uwezo wa kufanya maamuzi yatakayoibana Benki Kuu kwa ujumla na maamuzi yao hayatabadilishwa hata na *quorum.* Kwa hiyo, maamuzi yao yako *binding,* yanabana kabisa Benki Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hapa mimi nina wasiwasi naona kuna jambo la hatari sana, hawa watatu ndiyo watendaji wakuu wa Benki Kuu. Leo hii tunawaruhusu wakae waseme kwamba katika *opinion* ya Gavana wanatakiwa wakae watatu halafu wawe kama Bodi na watoe maamuzi ambayo yataibana Benki Kuu kama maamuzi ya Bodi, lakini hawaelezi ni sababu gani ni kwa nini wale wajumbe wengine wasiitwe hiyo ni dharura gani ambayo inafanya wajumbe wengine wasiweze kupata nafasi na hasa kwa

kuzingatia kwamba upashanaji habari nchini kwetu ni mwepesi kwamba haiwezekani wajumbe wengine wanne wasiweze kupatikana mpaka hawa wakae kwa dharura. *(Makofi)*

Mimi nilikuwa nashauri kwamba kama itakuwepo na dharura yoyote basi wasikae hawa watendaji watatu peke yao. Hili ni jambo la hatari sana pamoja na uhuru tunaotaka kuwapa. Basi akae Mwenyekiti japo na wajumbe wengine wawili, *non executive members.* Lakini ukisema wakae watendaji wenyewe watatu peke yao, maamuzi yao yaweze kuibana Benki kwa kweli hii ni hatari sana na hali yetu ya Watanzania bado tunaifahamu, mapungufu ya kibinadamu ni makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nionyeshe hilo katika Muswada huu. Waingereza wanasema *justice must not only be done but must be seen to be done.* Katika hili ninaamini inawezekana wakakaa watatu wakatenda haki. Lakini kwa mtazamo wa umma tunaona kwamba haki hapa haionekani kama itatendeka. Ninaomba sana kipengele hiki kifanyiwe marekebisho wasikae watendaji watatu wenyewe na wakajifanya ndiyo Bodi ya Benki Kuu na wakatoa maamuzi ambayo yanaweza kututia kwenye hatari.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi kama wenzangu naunga mkono hoja Muswada huu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, ili nami niweze kuchangia kidogo Muswada uliopo mbele yetu.

Kwanza nataka kutoa pongezi zangu za dhati kwa Waziri wa Fedha, Manaibu Mawaziri wake, Katibu Mkuu, Gavana wa Benki na Naibu Gavana wa Benki, kwa kuleta Muswada huu mbele yetu na naona umefika wakati muafaka kabisa. Nataka kusema kutoka mwanzo kwamba mimi naunga mkono Muswada huu moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sina tatizo na jinsi walivyopendekeza muundo uwe, hilo sina tatizo. Napenda kusema kabisa, wenzangu Wabunge wengi wametoa mapendekezo mazuri ambayo mimi nayaunga mkono ila tu kuna baadhi ya mambo ambayo mimi ningependa kuyazungumzia zaidi ili kuboresha Benki Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka kuzungumzia kwanza kuhusu suala zima la kusimamia thamani ya fedha zetu yaani shilingi. Wenzangu wengi wamezungumzia juu ya kuporomoka kwa shilingi kunakotokea mara kwa mara. Inatokea mara nyingi bila Benki Kuu kuingilia kati. Mimi nasema kama kulikuwa na kigugumizi, kigugumizi hiki kiishe ili mara kwa mara Benki iweze ku-*regulate* shilingi na thamani yake. Tusipofanya hivyo tutakuwa tunaumia sana kiuchumi. *(Makofi)*

Mimi naona hili ni mojawapo kubwa ambalo Benki Kuu lazima ilifanye. Nataka kutoa mifano tu kwamba wengi wetu hapa tumesafiri nchi mbalimbali na tumeona jinsi Benki Kuu za wenzetu zinavyothamini hela yao. Ukienda Ufaransa utatakiwa ulipe *bill* zako za hoteli kwa *Faranga* ya Kifaransa, ukienda Ujerumani utalipa kwa *marks,* ukienda

Uingereza utalipa kwa *pound sterling,* ukienda *USA* utalipa kwa dola na kadhalika. Sasa siku hizi wenzetu wa Ulaya wamebadili wanalipa kwa *Euro.*

Mheshimiwa Naibu Spika, unapokuja Tanzania, hatuna sheria ya aina hii, wageni wetu wanafika Tanzania na wanalipa kwa fedha zao za huko nje. Hilo tunaliona ni jambo la fahari. Sasa mimi nataka kusema kwamba hili ni jambo ambalo linapungufu sana, thamani ya hela yetu ya shilingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Benki Kuu, ikisimamia kwamba kila mtu atakayekuja nchi hii, ni lazima abadili kwanza fedha zake, kama ni *Euro* au dola kwa hela ya Tanzania, tutaiongezea thamani hela yetu hapa hapa na pia tutawawezesha wafanyabiashara mbalimbali wa *Bureau de change* na kadhalika kupata fedha zaidi kwa sababu wao watapeleka fedha hizi kwenye Mabenki zinabadilishwa zinakuwa shilingi kwa faida ya Watanzania. Lakini kama tukiachia hivi hivi kwa kweli hatutakuwa na faida yoyote kwa fedha zetu. *(Makofi)*

La pili katika hilo hilo la thamani hasa kwa wenzetu wa Zanzibar kwa bahati nzuri Zanzibar utalii umeshamili sana, lakini kinatokea nini, utakuta watalii wanaotoka Italia wao wanalipa *package tour* wanalipa fedha zote kwa *Lila,* watalii wanachukuliwa wanakuja Zanzibar, wanakiingia Zanzibar wanachukuliwa kutoka *airport* moja kwa moja kwenye mahoteli mbalimbali kule wanakula chakula cha Kiitaliano, bia ya Kiitaliano na kila kitu cha Kiitaliano bila kutumia fedha yoyote ya Kitanzania. Hii sawa jamani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji hawa waje watuletee hizi fedha ziweze kutusaidia. Sasa ikiwa Benki Kuu haidhibiti mambo haya basi Taifa letu watu watakuwa wanakuja hapa nchini anakuja na dola yake na anarudi bila hata kubadili hata senti moja na sisi hatutafaidika kwa hilo. Mimi ningeomba kabisa hili Benki Kuu waliangalia vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, si hivyo tu hata biashara zetu nyingi utakuta mathalani Taasisi zetu za fedha zinajenga nyumba, bei ya *square metre* moja ukitaka kwenda kupanga utaambiwa bei yake ni kwa dola labda dola mia tano kwa *square metre* moja. Sasa kwa nini wasilazimishwe hawa wafanye *square metre* moja shilingi kadhaa 500,000 au shilingi 600,000 kwa nini isiwe hivyo? Tunavyoendelea kutumia hii dola maana yake tunaporomosha thamani ya fedha yetu na hakuna mtu mwingine atakayekuja kutukuza fedha yetu na kuiweka value ya kutosha kama sisi wenyewe hatutakuwa tunafanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiw Naibu Spika, kwa hiyo, mimi ningependa kupendekeza kwa Benki Kuu ifanye yafuatayo:-

Moja, Benki Kuu yetu ianze mara moja kutoa maagizo kwa watoa huduma wote kwamba wawe wanatoa huduma hizo kwa kutumia hela ya Tanzania ambayo ni shilingi. Naamini kwa kufanya hivyo tutafaidika sana na watu watakaokuwa wanabadili zile fedha zao. *(Makofi)*

Mbili, Benki Kuu ikae pamoja na Makampuni mbalimbali ya utalii ili hasa wale wanaokuwa na *tours* kutoka nje ili kuwalazimisha wanapokuja nchini kwetu, gharama zao ziwe kwa hela ya Tanzania na siyo kwa fedha za kule. Hii itatuwezesha katika kubadili maisha yetu na watu mbalimbali kama wamachinga na kadhalika watapata vijisenti kidogo vya *commission. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba sana Wizara ya Fedha, isisitize kwamba Benki Kuu itumie Kanuni mbalimbali ili wawekezaji na mtu yeyote anapokuwa Tanzania watumie fedha za Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Wizara yetu ya Maliasili na Utalii iwaelekeze *tour operators* kwamba shughuli wanapokuwa Tanzania zifanyike katika fedha za Tanzania. Tukichukua hatua hizi naamini kabisa tutakuwa tumeongezea value zaidi kwa hela yetu ya shilingi na wakati mwingine inaweza hata ikaacha kuporomoka kama inavyoporomoka kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi inaporomoka kwa sababu watu hawaiheshimu. Mhindi anaona ni afadhali awe na dola kuliko kuwa na shilingi. Sasa tufike mahali ambapo sisi wenyewe tuithamini hiyo shilingi.

Hivi kama wewe mwenyewe huthamini kitu chako, kama humthamini Rais wako, humthamini Waziri Mkuu wako, hivi unategemea nani atakayekuja kumthamini? Kwa hiyo, hili naomba katika kuzungumzia sera naomba kabisa kuwe na mwelekeo huu na kuwe na mapinduzi haya makubwa ili kwamba shilingi ya Tanzania iwe na maana. Ukienda kwa hawa wenzetu Kenya, ukifika kule lazima ubadili pesa zako ziwe *Kenya shillings* na ndiyo unaweza kwenda hotelini au ukafanya biashara yoyote. Lakini hapa Tanzania siyo. Mimi langu kubwa niliona nilizungumzie hili.

La mwisho, nilitaka kusema kwamba kwa maendeleo ya vijiji vyetu, wanajaribu kwa kila njia kutaka kujiendeleza. Lakini nataka kuungana na wenzangu kwamba hali ya mabenki hasa katika vijiji ni mbaya sana. Ni lazima tukaye tuone jinsi gani mabenki yanaweza kusaidia shughuli mbalimbali za vijiji vyetu, hasa katika upande wa kilimo na biashara ndogo ndogo ili kwamba wananchi nao waweze kunufaika na haya mabenki. Namna nyingine mpaka sasa hivi, kama ilivyo, watu hawataelewa maana ya benki hizi ni kitu gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, nataka kuunga tena mkono hoja na naamini haya yaliyomo pamoja na mawazo yangu kwamba walau benki ziweze ku-*control* na kutia thamani kwa fedha ya Tanzania. Haya yakishughulikiwa kanuni zikitumika ili kuhakikisha yanatendeka, naamini kabisa Benki Kuu itakuwa imetekeleza wajibu wake vizuri bila wasiwasi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Muswada huu ambao unaendelea ulioletwa na Waziri wa Fedha. Tunapozungumza sasa hivi Rais wetu mpendwa Jakaya Mrisho Kikwete, amefikisha siku 100 na siku hizi ni siku za mafanikio

makubwa, hayajapata kutokea. Kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la Siha naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Rais wetu na Serikali yake kwa kazi nzuri ambayo imefanyika. Mimi kama Mbunge ninayetokana na Chama cha Mapinduzi najivuna kuona mafanikio makubwa yameweza kutokea katika kipindi hiki cha siku 100. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo naomba sasa nijielekeze katika Muswada wenyewe. Nimefuatilia kwa karibu. Juzi tulikuwa na semina hapa, tumezungumza na niishukuru Serikali kwa kweli. Mheshimiwa Waziri tunashukuru kwamba tulipata semina ile, maana yake ilipanua uwelewa wetu na tuliweza kubadilishana mawazo na kuweza kujua kwamba ni nini kinachozungunzwa. Lakini kipekee napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa hotuba yake ambayo ameitoa jana. *It is my judgement* kama *Member of Parliament* kwamba lugha ile ilikuwa ni lugha rahisi, nyepesi ya kueleweka na kwa hiyo unaweza ukaona kwamba walau tumepiga hatua kubwa sana katika kuelewana katika jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, humu ndani tupo Wabunge wa aina mbalimbali. Wako wanasheria, wanaweza wakakueleza *imputations* zake kisheria, wako wanauchumi, watakueleza *imputations* zake kiuchumi, wako watu wa *Political Science* watakuambia ki-*political imputations* za hili jambo. Kwa hiyo, yote ikikusanywa basi ndiyo unapata kitu kimoja ambacho sasa kinatuletea mabadiliko na maendeleo.

Napenda kusema kwamba *flexibility* ya Serikali hapa kwa maana ya kukubaliana na baadhi ya mambo tuliyozungumza imesaidia sana katika kufikia muafaka na kukubali kwamba *now* ni sawa na mabadiliko haya yanayoletwa tunakubaliana nayo. Napenda kabisa niseme hapa kwamba mimi naunga mkono hoja hii na nitaeleza kwa nini naunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko makubwa yanapotokea na ukakaa tu ukasema mimi sibadiliki, utapata matatizo makubwa sana. Upepo ukivuma, upepo unapovuma kwa nguvu sana ile miti ambayo inakwenda, unaiona inanepa, unauona unanepa namna hii, kwa kawaida haing'oki. Ile miti yote inayoiona inayumba, unaiona inacheza namna hii, unaiona inacheza, upepo uvume, hata ungevuma namna gani, haing'oki. Hiyo ni *principle* ni kanuni. Lakini miti inayokakamaa, iliyokaa mahali pamoja, inasema mimi nitatulia, ndiyo unasikia kupu, kupu, unasikia imeng'oka. Ndiyo unasikia imeng'oka. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hii ni kanuni tu na Serikali isipokuwa *flexible* katika mambo itapata matatizo. Kwa sababu itapata matatizo, utaona. *Flexibility* ya Serikali katika jambo hili imesaidia na ndiyo maana kumeletwa *amendments* kumeletwa mabadiliko. Mimi nasema kwamba naunga mkono. Hilo la kwanza.

Lakini la pili, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, alieleza hapa. Mabadiliko yanatakiwa wewe ulete yale mabadiliko, yaani usipoyaleta wewe utabadilishwa, ukishabadilishwa, utapata matatizo makubwa. Ni lazima ulete hayo mabadiliko wewe, uya-*determine* wewe, uyasimamie wewe na ndicho kinachofanywa na Serikali. Hilo la kwanza.

Lakini kinachozungumzwa hapa ni nini. Kinachozungumzwa hapa, tunazungumza habari ya *de-political economy of socialism and political economy* ya *capitalism.* Hii sina maana kwamba unachukua *economics* na *politics* unaziweka pamoja, *no!* Unazungumzia *relations of production,* ndicho kinachozungumzwa hapa. Ndiyo mambo yanazungumzwa hayo. Wewe nenda, zungumza jambo lolote na ndiyo maana tumekuwa hapa. Huwezi kusema, hapa kwetu sisi watu wanafikiri hii nchi ni nchi ya kijamaa. Haijawahi kuwa nchi ya kijamaa, ujamaa haujengwi hivyo. Hii nchi sasa inakwenda kwenye ubepari. Ubepari haujengwi hivyo. Huu unaitwa ubepari uchwara. Unakwenda kwenda nao tu hivi hivi. Huu ni mwelekeo wa kibepari. Lakini huwezi kusema huu ni ubepari. Ubepari haujengwi hivi, ubepari kuna *stage* fulani unaofika ambao kunakuwa na *industrial development* unasema kwamba sasa imefika katika hatua ambayo najenga ubepari na walau naweza nikafikiri habari ya kuujenga ujamaa. Ndicho kinachozungumzwa hapa.

Katika mfumo wa kwetu na benki hii ilipoundwa, nilisema juzi iliundwa kwa ajili ya kujenga nchi ya kijamaa. Ndiyo jukumu lake la msingi. Huwezi kuleta mabadiliko ukaondoka hapo. Nchi hii tusipozungumza habari ya kujenga ujamaa kwa maana ya kumjali Mtanzania mdogo mdogo, haina maana na watu watashangaa mimi natumia mtaji, wewe unasema hivyo, wanasema huyu anasema nini. Iko katika Katiba ya nchi hii kwamba nchi hii ni kijamaa. Waingereza wale na ubepari wao wale, bado wanasema ni wa kijamaa. Usipojenga ujamaa katika nchi hii watu watakufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki Kuu isipokuwa na mwelekeo, mimi walikuwa wanasema hivi huyu Gavana au *Deputy Governor* wake aweje, awe na digrii mbili, *masters.* Mimi nikasema andika awe mjamaa, awe mzalendo, maana yake mzalendo labda mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu spika, wewe unaweka mtu ni mtu tu. Ni lazima uangalie Mheshimiwa Zakia Meghji ni lazima umwangalie mtu mwenye mwelekeo unaofanana na kupigania wanyonge. Ndiyo unamweka kwenye Benki ile. Kwa hiyo, hii ilivyowekwa hapa, hii ilivyowekwa ni sawa. Kwanza *appointment* itafanywa na Rais. Kwa hiyo, akifanya vitu vya ajabu ajabu kule, Rais atasema *no,* hatuwezi kuendelea hivyo. Yule mwenzetu wa Kenya aliyekuja hapa alizungumza habari ya nchi ya Kenya akasema Gavana wao ana matatizo pale, Serikali iliingilia kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye nchi ya kijamaa njia zote kuu za uchumi zinakuwa mikononi mwa umma. Kwenye nchi ya kibepari mnaingia katika kanuni zinazolinda ubepari. Kuna kanuni ya utashi na urari. Kuna kanuni ya mashindano. Kuna kanuni ya *value. Below demand and supply, below of competition and law value.*Ndiyo inayofanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipozungumza habari ya je benki hii inawatazamaje wakulima wadogo wadogo? Gavana alijibu, akasema kwamba ili uweze kufanya ile riba, riba maana yake inaonekana ni kubwa sana. Asilimia 19, 20, ingiza mabenki mengi mle ndani ili sasa washindane.Wakishashindana hawa watafika wengine wataona umuhimu

wa kupunguza ile riba iende kwenye asilimia 12, asilimia 7 na kadhalika na kadhalika. *Good talk,* hawa mabwana hawa wanaweza wakafika mahali waka-*collude* ukaiona inaning'inia. Ndiyo maana kuna kitu kinachoitwa *The Financial of Leader Keys,* wanatengeneza *mark titles* wanaweza wakafika mahali ikakaa hapo isibadilike. Serikali itafanya nini? *Suppose* unakwenda unafika mahali unasema nitaziachia nguvu za soko zifanye kazi. Kunakuwepo na *market failure* utafanya nini? Serikali inafika mahali kuna mtaji mkubwa unahitajika katika ile *Union* utafanya nini? Kamsome David Ricardo, kamsome Adam Smith, nenda kamsome akina Lord Keys, wanakuambia Serikali iliingilia kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisema watu wakauze maji, wakasema watu sisi hatuwezi kuuza maji, kwa sababu hakuna biashara hapa, unafanyaje. Utasema Serikali itajitoa, hatuuzi maji na watu wanahitaji maji. Utasema Serikali lazima iingilie kati. *Autonomy* inayozungumzwa hapa ina-*pre suppose* nini? *Autonomy* mimi nakubaliana na *arrangement* hii kwa sababu imeambiwa ndiyo *the best process,* tuitafute. Tumejaribu kuangalia nchi nyingi tu. Gavana ni huyo huyo na Mwenyekiti ni huyo huyo.

Mimi nasema kwamba *pre-suppose vision* ya Tanzania ni kwamba hiyo *autonomy* ni lazima ibebe wajibu kwa wananchi Watanzania. *It must carry with the same special amount of responsibility* kwa Watanzania. Huwezi ukazungumza hapa ukaniambia kwamba utaunda Benki hapa ukaniambia kwamba haitawaangalia wakulima wadogo wadogo, halafu ukaniambia pitisha, nitakuambia *no way.* Mimi lazima nione *one function* kati ya Benki Kuu na maendeleo ya mwananchi huyu mdogo mdogo kule kijijini. Wajibu wa jamii ijitokeze wazi wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii maana yake nini. Ninachotaka ku-*conclude* hapa ni kwamba lazima tukubaliane hapa kwamba mabadiliko ya kibenki yanayofanyika hapa lazima yafanyike na kwenye sekta nyingine za uchumi wa nchi hii. Huwezi ukasema mimi nafanya mabadiliko haya halafu tusizungumze namna ya kuimarisha ushirika katika nchi hii. Huwezi ukafanya mabadiliko yanayofanyika hapa usizungumze namna ya kuwa-*empower* akinamama kule kijijini. Huwezi ukazungumzia habari hii usizungumze habari ya namna ya kuwa-*empower* vijana. Chama cha Mapinduzi katika Ilani yake ya Uchaguzi kilisema na *good enough* Waziri wetu wa Fedha ni *Member* wa *Central Committee,* tumepita tunawaambia wananchi, akinamama watawezeshwa.

**NAIBU SPIKA:** Na Mjumbe wa Ilani.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, na Mjumbe wa Ilani. Nashukuru sana nashukuru. Kwa hiyo, mimi sina wasiwasi na jambo hili. Matumaini yangu ni kwamba tutakwenda *in full.* Bunge hili haliwezi likafanya kazi ya kusema linatetea watu wakubwa wakubwa tu. Kwanza wao wana nguvu. Bunge hili *how about back position,* lazima lirudi kwa wananchi, litetee wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, chukua mkopo wa pembejeo unataka kupata trekta hapa. Nenda kapitie katika mfumo ule ulioko katika Wizara ya Kilimo mpaka ufike pale

*Exim Bank* huwezi kulipata lile trekta, uone urasimu unaotokea hapo katikati, jinsi inavyokuwa shida kupata ule mkopo pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, napata matatizo makubwa. Sasa mambo ya *inflation* haya kwamba mfumko wa bei utatokea na lini. Ukitaka ku-*deal* na suala la *inflation* na mambo mengine yote tunayozungumza hapa, ni lazima u-*deal* na suala la *production,* kama hela yako unapata kutoka kwa mkulima ni lazima urudi kwa mkulima yule yule upeleke hela kule kwa wakulima kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Marx alisema, *always the economic base determines the super structure.* Unachozungumza hapa juu hapa chini kitakataa. Kwenye banda la kuku kama unatakiwa upeleke pale mifuko mitatu ya chakula cha kuku, ukipunja siku moja hivi ukatoa miwili halafu ukasema ngoja niwapunje kidogo. Keshokutwa ukija *trey* moja linapunjwa. Kuku wanajua *economics* kuliko sisi. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, ukiendelea tena ukakaa tena ukapunja tena, kapunje hivi hivi, ukirudi tena *trey* zilikuwa 10 unakuta zimerudi 7. Sasa sisi hapa unasema mkulima huyu tutamfuata huko kijijini huko hatutamsaidia. Mimi nasema kama hatutamwangalia mkulima, Benki Kuu isipoangalia habari ya mkulima katika Tanzania haya mabadiliko yote tunayofanya hapa hayana maana. *(Makofi)*

Sasa mimi najua kitu kinachozungumzwa, najua kitu nakizungumza. Unajua wale wataalam wa mambo haya wanasema hivi, *The Government should be kept today.* Iache isijiingize katika jambo lolote. Tumesema hapa Serikali lazima mkono wake katika Benki Kuu ujitokeze wazi wazi. Wakija wawekezaji hapa halafu watu wako barabarani wanatupa mawe, halafu unasema kwamba sasa inakuwaje kuwaje. Wawekezaji endeleeni ninyi msijali mambo ambayo anakuambia *how do I invest* hapa na kule barabarani watu wanarusha mawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanasema mambo yanazungumzwa hapa ni mambo ya kisiasa. *Economics* ni *reflection* na *politics* na *politics* ni *reflection,* ni *economics*. Zinakwenda *in conformity.* Ukikataa habari hii ukasema kwamba aah, waache tu huko, hakuna *investor* atakuja kuwekeza katika nchi hii kama hapa kuna vurugu za kisiasa. Hakuna mtu atakayekuja kuwekeza hapa. Kwa hiyo, ni lazima ulipe *channel* hiyo. Benki ile haiwezi kwenda tu ni lazima itakwenda tu, itapelekwa kwa Sheria ya Utashi na Urari. Itapelekwa kwa Sheria na ushindani. Itapelekwa kwa Sheria ya amani. Itaangalia habari ya *constant capital* na *value* itaishia hapo haitafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipoanza kupata tatizo la chakula hapa, tulipokuwa na njaa hapa, si tulimwona Waziri Mkuu anakimbia kutafuta chakula. Si tulimwona Rais wetu anakimbia kutafuta chakula. Si tuliwaona Wakuu wetu wa Mikoa wanakimbia. Itakuwaje, benki ile itakaa tu pale kama kichuguu imekaa pale. Haitaweza, itafika mahali lazima ifanye kazi ya kuhakikisha kwamba nao politically inafanyakazi. Benki hii iseme kabisa katika kanuni zake iseme hii itafanya kazi ya kumtetea mkulima mdogo mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Daudi Balali alituambia siku moja akasema kwamba noti mpya zimekuja zimewekwa katika namna ambayo hatutegemei watu wanaweza wakatengeneza noti feki na hii iko katika *part three* ya Muswada tunaouzungumzia hapa. Lakini sasa hivi mtaani tunasikia kila siku watu wanazungumzia habari ya noti ambazo ni feki. Nimehama katika hilo eneo niliona nitumie muda mwingi kwenye lile eneo kwa sababu niliiona hatuelewani humu ndani. Lakini ninachosema ni kwamba mimi naunga mkono jambo hili. Naliunga mkono lakini hizi ndiyo *observations* zangu kusema kwamba jamani lakini wenyewe Wabunge wameona hili.

Je, kuna *mechanism* gani ambayo imewekwa ya kuhakikisha kwamba alituambia benki kwamba zile pesa zinazokuja hizi mpya ni pesa ambazo sasa watu hawawezi kujitengenezea hela, hizi noti feki. Lakini mpaka sasa hivi tunalo jambo hili. Moja, ni hatua gani zinazochukuliwa kuzuia hali hii isiendelee? Pili, ni kwa kiasi gani umma umeandaliwa kujua hili tatizo? Kwa sababu wao wanapokea hela huko, mimi kama Mbunge, sijajua kwamba ni lini tutakutana tuangalie ili nikikutana nalo hili niseme aah, hii siwezi kupokea maana yake hii inaonekana kwamba ni noti feki. Tungetaka tueleweshwe hilo tujue kwamba kuna hatua za namna hiyo ambazo zinachukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda kurudia tena kusema kwamba mimi naipongeza Serikali. Nasema kwamba *flexibility* hapa itatusaidia sana. Haya mengine haya yanayozungumzwa hapa ya kwamba itakuwa hivi itakuwa vile, *decision making* inafanywa na Gavana, mimi sioni taabu sana kwa sababu kama kutakuwepo na matatizo ya namna hiyo, Miswada itatungwa itakuwa Sheria lakini kama kuna problem katika implementation yake tutarudi hapa ndani na kusema kwamba bwana hili limeonekana operationalization yake ni matatizo. Kwa hiyo, tubadilishe kipengele hiki. Hakuna problem.

Kwa hiyo, nashauri Wabunge wenzangu, jambo hili tulikubali. Jambo hili ni la Serikali, kila mtu ametoa *observations* zake na dukuduku lake. Sioni tatizo sana wakati ule Gavana yule alikuwa ni Mwenyekiti, wakati huo huo alikuwa ni Gavana bado ndivyo inavyopendekezwa hapa. Kuna matatizo katika *decision making* kama tulivyoona hapa, lakini kimsingi tukubaliane na haya kwa sababu mabadiliko makubwa yanatokea katika nchi yetu na kama kwa kweli tukiacha hivi hivi tutakuwa na matatizo kule mbele ya safari tutabaki na matatizo hayo, halafu tutakuwa hatujui kwamba tunafanya nini.

Baada ya kusema hayo, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha, napenda kurudia tena kusema naipongeza Serikali na naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nichukue nafasi hii kwa kweli kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia huu Muswada wa Benki Kuu. Lakini ni vizuri vile vile niwapongeze Waziri wa Fedha, Manaibu wake, Gavana na wasaidizi wake na wataalam wote wa Benki Kuu kwa kutuletea huu Muswada hapa Bungeni. Mwisho, nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na wajumbe wake jinsi walivyoshughulikia hili suala la marekebisho. Kwa kweli wametoa mchango mkubwa sana. *(Makofi)*

Mimi kwa niaba ya wananchi wangu wa Njombe Magharibi, vile vile nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete na wasaidizi wake, akiwepo Waziri Mkuu jinsi wanavyotekeleza majukumu yao kwa sababu sasa hivi hali imeshaanza kubadilika na wananchi wanachotaka ni kuangalia mabadiliko yanaonekana kwa macho. Kwa kweli hilo nampongeza kwa niaba ya watu wangu. *(Makofi)*

Mimi nataka nichangie upande wa *appointment* za *Governors* na *Deputies.* Kwa vile *institution* hii ni muhimu sana na kama ilivyoainishwa ningeshauri kuwa ni vyema majina yanayopendekezwa ya Gavana na *Deputy Governors* yaletwe kwenye Bunge kwa kuthibitishwa. *(Makofi)*

Hii pamoja na kwamba itatoa uzito kwa uteuzi huo lakini kama wawakilishi wa wananchi tutakuwa tumethibitisha kwa niaba yao yaani wananchi tunaowawakilisha.

**NAIBU SPIKA:** Kuna watu wenye simu.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Kwa hali ilivyo ni kwamba kama uthibitisho utapitia mbele ya Waheshimiwa Wabunge, Gavana na wasaidizi wake wataona kwamba wamewajibika moja kwa moja kwa wananchi wa kawaida hasa wanyonge. Nasema hivi kwa sababu ni vizuri waelewe kwamba magavana wapo kwa ajili ya wananchi wa kawaida, wa chini kabisa. Kwa hiyo, na sisi Wabunge ndiyo wawakilishi wao. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiria kwa kweli ni muhimu sana hizi hoja ziwe zinaletwa Bungeni pamoja na kwamba tunasema tumechelewa, hatujachelewa.

Halafu jambo lingine ambalo nilitaka nichangie ni kuhusu suala la umri kwamba uzoefu wa Gavana, *Deputy Governor* walau wawe na miaka 15 kwenye uzoefu. Sasa mimi naona hapo nakuwa tofauti kidogo kwamba hapo utakuwa unamnyima huyu kijana ambaye ana uwezo pengine ni mwaminifu na amesoma kupata nafasi ya Ugavana na *Deputy Governor.* Mimi ningeshauri uzoefu walau ungekuwa miaka 10 kwa sababu hiyo ingetusaidia sna hasa upande wa vijana kupata nafasi ya Ugavana na *Deputy Governors.*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala la muda wa kukaa madarakani kwa *Deputy Governors.* Mimi ningeshauri kwamba ni vizuri uongezwe isiwe miaka mitano au walau ingekuwa 10 kama anafaa zaidi wanaweza wakaenda hata zaidi kwa sababu ungeendana na umri wa kukaa madarakani kwa Rais. Kwa sababu naye Mheshimiwa Rais ana vipindi viwili vya miaka mitano mitano. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri hapo kwamba ni vizuri hawa wenzetu watakapopata hizo nafasi walau ingekuwa zaidi ya miaka 10. Kwa sababu ukiangalia hata kwenye noti zetu hizi, utaona kuna saini ya Gavana. Kwa hiyo, ingekuwa vizuri badala ya kuweka masaini, saini kwenye noti zetu ziwe zinabadilika walau wakae kipindi cha zaidi ya miaka 10.

Jambo lingine, nitatofautiana kidogo na Waheshimiwa Wabunge wenzangu walikuwa wanazungumza kuhusu suala la hizi benki. Kwa sababu Benki Kuu ndiyo inazi-*monitor* inaziangalia hizi benki hizi za kizalendo na benki hizi za kigeni. Mimi naona kwa kweli *interest rate* wanazotoa mabenki pamoja na kwamba tunasema ni kubwa.

Mimi nilikuwa *CRDB* nilikuwa nafanya kazi *CRDB* kwa kweli naona *interest rate* siyo kubwa. Nitatetea kwa nini nasema siyo kubwa. Hizi *interest rate* zinawekwa vile kwa sababu wanaangalia ile *risk.* Kuna hawa wafanyabiashara wakubwa hawa, kuna wengine siyo waaminifu, wanachukua mapesa mengi ya wazalendo wa chini halafu wana-*disappear.* Kwa hiyo, ndiyo maana *interest rate* wanaweka kubwa zinakuwa juu kwa sababu ya kuhofu hiyo hatari kwamba inaweza ikapotea hela. Lakini nilichokuwa nashauri hapa ni kwamba tufanye *vice versa* kwamba *interest rate* zile za mabenki walau zibakie pale pale kwa wafanyabiashara wakubwa. Halafu kwa wafanyabiashara wadogo wadogo au wananchi wa kawaida ipungue. Kwa sababu sasa *interest rate* inamgandamiza mfanyabiashara mdogo mdogo na mkulima wa kawaida analipa *interest rate* asilimia 24 wakati yule mfanyabiashara mkubwa *iterest rate* anapata asilimia 12.5.

Mimi nilikuwa nafuatilia *SACCOS* moja iko hapa hapa mjini. Nilikuwa nauliza vipi jamani *interest rate* zikoje? Kwa kweli walikuwa wanalalamika sana, wao wanapewa *interest rate* kwa mwaka 12.5. Mwananchi wa kawaida anapokopa *SACCOS* anapewa *interest rate* asilimia 2 kwa mwezi. Ina maana kwa mwaka ni asilimia 24. Sasa mimi kwa mawazo yangu nilikuwa naishauri Serikali *interest rate* hizi ziwe *vice versa* kwamba hawa wafanyabiashara wadogo wadogo na hawa wakulima wadogo wadogo hizi *SACCOS* hizi zipewe *interest rate* ndogo sana ili mwananchi wa kawaida apate *interest* ndogo kwa sababu ili waweze kujiendesha lakini hao wafanyabiashara wakubwa kwa kwa sababu hizi benki tutaziua, zibakie pale pale kwa wafanyabiashara wakubwa.

Halafu ningeishauri Serikali badala ya hizi fedha kupitia kwenye mikono ya vyombo vya fedha, ni vizuri Wizara inayohusika kama ya Ushirika, ingekuwa inapewa moja kwa moja inakopesha *SACCOS* moja kwa moja au *SCULT* moja kwa moja. Kule kwangu Njombe Magharibi tumefaidika kidogo na *SCULT. SCULT* imeleta mikopo kidogo kwa wananchi wa kawaida lakini huko nyuma hali ilikuwa ni mbaya sana. Ninapozungumza Benki Kuu nilikuwa namwona kipindi fulani Gavana, ilikuwa jana kwa kweli niliona kama hayuko *serious* sana ni kwa sababu anaelewa kwanza yeye a-*deal* na watu wakubwa. Lakini aelewe kwamba mimi ni mwakilishi wa Njombe Magharibi, watu wangu kule wanapata shida, hawana vyombo vya fedha, hawana benki yoyote. Kwa hiyo, wanapata shida sana. Sasa hapo nizungumzie vile vile kuhusu suala la noti. Hizi noti hizi, ni nyepesi sana. Mimi ningeshauri kwamba watengeneze noti walau ngumu ngumu kidogo hata ziwe za nailoni zisiwe zinachanikachanika. Hiyo itasaidia kwa sisi ambao tunapata huduma kwenye majimbo mengine ya mbali labda Makambako au Njombe Mjini au Mbeya, kwa sababu mimi niko mpakani mwa Mbeya. Ingetusaidia sana hizi noti zidumu na ili kusaidia kuendana na ari mpya na kasi mpya na nguvu mpya ni vizuri *SACCOS* hizi ziimarishwe kwenye jimbo letu ili mwananchi wa kawaida kabisa na majimbo mengine ambayo hatutayataja yaweze kufaidika na hizi huduma ndogo ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho nilitaka kuchangia ni kuhusu suala la haya mabenki, suala la dhamana. Kweli hawa wafanyabiashara wakubwa wanaenda kukopa benki kule. Wanaenda kukopa kule benki, wanapewa dhamana. Lakini zile dhamana wakati fulani kuna wafanyakazi ambao siyo waaminifu wanashirikiana na

wafanyabiashara wabaya wakubwa. Zile dhamana zinawekezwa isivyo halali. Mtu anaweza akaonyesha nyumba ya jirani kwamba ndiyo nyumba yake wakati pale sehemu ile ni uwanja mtupu.

Kwa hiyo, benki inapata hasara inatoa milioni 50, milioni 200 maskini baada ya kufuatilia sana wanaona hamna kitu. Kwa hiyo, benki inapata hasara kubwa sana. Nilikuwa nafikiria kwamba ni vizuri hizi benki zetu tujitahidi kuzilinda na kuhakikisha kwamba tunaziwezesha, hata Mahakama zetu vile vile kwamba Mahakama zetu na benki zetu zinajitahidi kutetea wafanyabiashara wakubwa. Kwa mfano, mtu anakopeshwa mtu ameiba lakini unaweza ukaona mkataba ulikuwa unasema kwamba zile dhamana ziuzwe baada ya kukiuka mikataba.

Lakini unaona huyu mtu anatetewa na Mahakama na anasema wakipelekwa Mahakama anasema hatuwezi kuwaingilia uhuru wa Mahakama na Mahakama wakati fulani huwa zinakuwa na siyo kwamba pengine wote baadhi ya Mahakimu au Majaji huwa hawaitendei haki benki. Wanatoa hizi *court injunction* bila hata kuita zile pande zote mbili. Kwa hiyo, benki wanaziua kwa makusudi. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba kwa kweli uamuzi wa Mahakama au wa Jaji au Hakimu uzingatie maslahi ya benki zile kwa sababu zile benki zile hela siyo hela za yule mfanyabiashara mkubwa ni hela za watu wa chini kabisa.

Kwa hiyo, isiwe inatoa *court injunction* kiholela holela na Hakimu au Jaji anayepatikana anatoa *court injunction* kiholelaholela ikiwezekana afukuzwe kazi au asimamishwe kwamba huyu mtu mbali ya kwamba anaharibu uchumi wa mwananchi mdogo mdogo anaidhoofisha benki, benki inakufa na benki nyingine zimekufa kwa sababu ulaghai. Halafu kingine ni hawa wafanyakazi ambao walijihusisha na wafanyabiashara wakubwa ambao siyo waaminifu kwamba hawa watu wanapoiba hapa wanahamia benki nyingine, hasa Idara ya Mikopo.

Kwa hiyo, nilikuwa nafikiria kwamba mtu anayepatikana na hatia ya udanganyifu asipewe sehemu zozote za kufanya kazi, kusudi iwe wanalinda mabenki, kwa sababu wanafahamika, anaiba *CRDB* anakimbilia *Stanbic Bank,* anaiba *Stanbic Bank* anahangaika sijui *NMB.* Sasa ile kwa kweli benki tunaziua pamoja na kwamba wenzangu hawanielewi ninaposema kwamba benki zinaumia kwa kweli benki zinafanya kazi nzuri, lakini kwa kweli inatakiwa tuzionee huruma.

Mwisho niseme kwamba hii hoja naiunga mkono sina tatizo nayo na nafikiria hata wananchi wangu huko wanasikia kwamba huko Njombe Magharibi kwamba Mbunge wao anazungumza leo, nichukue nafasi hii kuwashurukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono. *(Makofi)*

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii nikushuru kwa kunipa nafasi ya kuzungumza na kuchangia Muswada huu wa Benki Kuu.

Pili, napenda kuchukua nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa kutimiza siku 100, tangu aingie madarakani kazi yake nzuri tumeiona njaa ameidhibiti na inadhibitika, majambazi jasho linawatokana mengine yote aliyoyafanya kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya tunaiona tunaomba aendelee hivyo asirudi nyuma hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kuchangia Muswada huu kwa kusoma kipengele cha saba ama kifungu cha 7 ukurasa 31 kwa ruhusa yako katika kiingereza: *"The primary objective of the bank shall be to formulate, define and implement monetary policy directed to the economic objective of maintaining domestic price stability, conducive the balanced and sustainable growth of the national economy."* Mimi kwa mtazamo na kwa mawazo yangu hapa ndipo Benki Kuu wanapotakiwa wasimame napo kwamba wanakazi kubwa ya kujenga uchumi wa nchi hii Watanzania tumechoka na umasikini.

Naomba kutoa historia kidogo, wenzetu wa Ulaya Magharibi walipoathirika na vita vikuu vya pili vya dunia walikuwa na mpango unaitwa *marshal plan* wote tunaufahamu na moja kati ya mambo ambayo waliyafanya katika mpango huu ni kukopa katika benki, mabenki ambayo yaliundwa na kuzaliwa yanayoitwa watoto wa *bitten wood, Word Bank, International Monetary Fund* na mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakachukua pesa nyingi wakazijenga nchi zao na wao wenyewe wakafaidika. Leo *Europe* bado tunaita nchi zilizoendelea na mabenki haya niliyoyataja yana nguvu kubwa katika dunia hii kwa maana hiyo basi Muswada huu, mpango huu tunauzungumza leo hapa tunaweza tukafananisha na *marshal plan* yetu katika nchi yetu hii ya Tanzania, wao MKURABITA, MKUKUTA na wengine tena wana kazi kubwa ya kuondoa umaskini katika nchi yetu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba kuzungumza yafuatayo, kwanza Gavana wa Benki Kuu na Ma-*Deputy* wake wote watakaoteuliwa na Mheshimiwa Rais, naomba sana wawe wazalendo. Wawaonee huruma Watanzania maskini, kwa hiyo, wajue wanakazi kubwa kabisa ya kuiondoa nchi hii hapa tulipo na kwenda mbele zaidi, Watanzania wamedhamiria kuondoa umaskini, hilo liwe la kwanza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama walivyosema wenzangu tuna Waziri wa Fedha, namfahamu mama Zakia Meghji, ni mchapakazi, ni mzalendo hii kazi atatufanyia ya kuwapata watendaji wazuri katika Benki Kuu yetu, pamoja na uhuru tunaowapa.

Pili, tunaomba basi Benki Kuu wakae pamoja na *Commerce Bank* zote wawaambukize haya kwamba Watanzania wanataka kuondoa umaskini katika nchi yetu, watuelewe, wakituelewa yatafanyika mambo yafuatayo:-

(i) Wataondoa woga wa kufanyabiashara za benki katika nchi yetu, kwa maana hiyo ile riba kubwa wanayoitoa kwa sababu ya *risk* wanayoiona katika biashara hii waipunguze ili Watanzania waweze kuyatumia mabenki haya na waweze kujiendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimefanya ziara katika Jimbo langu la Lulindi, nimefika mahali nikawakuta vijana wakanisimamisha, nikasimama, nikafanya katidi papo kwa papo, wakaniambia Mheshimiwa Mbunge unatuona vijana sisi ni mashababi ndio, sisi tuna nguvu za kufanyakazi hasa kilimo lakini hatuwezi kulima kwa kutumia majembe ya kingondola, tunataka kulima kisasa na kulima kisasa lazima tuwe na mtaji tupate mikopo, tutapata wapi? Kwa hiyo, kwanza nataka kusema kwamba suala la kukopa sio kwamba linaeweka mijini tu hata vijijini linaeleweka.

(ii) Mheshimiwa Naibu Spika, Benki Kuu izingumze na mabenki haya yaanze kutoa mikopo ya uhakika kwa watu wetu vijijini hasa katika eneo la kilimo. Asilimia 80 ya Watanzania ni wakulima, tutakaposema kwamba hatuwezi kwenda huko kwa sababu wakulima hawana uwezo, tutaichelewesha nchi hii bila sababu yoyote, kama ni riziki hii basi nendeni kwanza mkajaribu, mje hapa mtuambie kwamba tumekwenda, tunaona tunapata hasara sio kuzungumza katika makaratasi tu, wale vijana pale nimewaambia kwamba nimewasikilizeni na nimewaambia nitakwenda Bungeni kuzungumza kwa niaba yenu, hivi sasa hivi wananisikia huku nawazungumzia kwa niaba yao. Nendeni vijijini kwa wale vijana wa Mpete pale niliowakuta wawe na matumaini, Mpete ni mahali maarufu sana pana umeme pale wameshahamasika wanapenda maendeleo wanachotaka ni nyezo tu na moja wapo ni hii ya mabenki

Mheshimiwa Naibu Spika, mmezungumzia hapa katika magavana watatu wale kuwe na mwanamke sawa sawa  na mimi naunga mkono kwa hilo, moja atoke Zanzibar barabara ni muhimu katika kuimarisha Muungano, na Gavana wake isipokuwa la msingi kusiwe na ubabaishaji wa kuwapata watu *competent* wa kufanyakazi hii  tunataka kwenda, utaratibu maalum uandaliwe wa kuwapata watu hawa kusiwe na upendeleo kama mnaona sifa zenu hazitoshi tuambieni tutawapeni sifa nyingine za kutosha  ili wapatikane watendaji wazuri watufanyie kazi nzuri hatuna matatizo ya kuwapeni uhuru mnaotaka leo mnaupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutafutieni watu wazuri ili benki yetu ifanye kazi vizuri, tuondoe umaskini katika nchi yetu tumechoka na umaskini, kwa ari mpya, nguvu mpya  na kasi mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. CHACHA  Z. WANGWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa hii nafasi na pia ningependa kumshukuru Waziri wa Fedha kwa kuandaa Muswada huu ambao kama walivyoeleza Wabunge wengine ni kuwa umekuja kwa wakati wake yaani ni muhimu sana kwa mabadiliko ya uchumi wa nchi yetu na mimi kama wenzangu ninauunga mkono *in principle* kwamba ni Muswada muhimu kwa uchumi wetu. Isipokuwa ningependa kutofautiana kidogo katika nafasi ya kutoa mchango wa maoni ambao Serikali inaweza kuufanyia kazi ili kuboresha mfumo mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa maoni yangu naona ya kwamba haya mabadiliko katika hiyo *amendment* ni yale ambayo kwa kiingereza yanaitwa *cosmetic changes* yaani ni mabadiliko ya juu juu. Kwa sababu tunapokuwa tunazungumzia kuhusu *autonomy* na *independence* ya benki hii naona kwenye Muswada huu inamaanisha zile *administrative* yaani mabadiliko ya kimuundo yamewekewa mkazo zaidi lakini ukiangalia *section* ya tano ilipokuwa inazungumzia kuhusu majukumu ya benki hii imeeleza kabisa majukumu ya benki hii kwamba ni makubwa na mazito ambayo yanaweza kuleta maamuzi ya ufanisi au ya kuporomosha uchumi wetu. Kwa sababu katika ile *section* ya tano inasema kwamba; *"the principal functions of the Bank shall be to exercise the function of a central bank and, without prejudice to the generality of the foregoing, to formulate, implement and be responsible for monetary policy."* Sasa suala la *monetary policy* haliko peke yake lina uhusiano mkubwa sana na sekta nzima ya uzalishaji yaani *production* na *exchange* yaani ubadilishanaji wa mali ambayo imeshazalishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa ninaloliona ni kwamba kuna matatizo katika *system* nzima ya *production* na haya matatizo hayakuanza leo, yamekuwepo na Serikali ya awamu ya kwanza imejaribu kuyashughulikia kwa nguvu zote na tungempa pongezi Marehemu Mwalimu Nyerere kwa jitihada zake zote na mimi ningependa kukubaliana na yeye kwamba *basically* yeye hakuona kama kulikuwa kuna tatizo lolote na Azimio la Arusha, hakuliona Mwalimu mpaka siku zake za mwisho na alisema katika hotuba yake ya mwisho akiwa Mbeya nadhani, kwamba jukumu la kizazi chao kama viongozi lilikuwa ni kuleta Uhuru katika nchi hizi ili tuweza kuwa na nafasi ya kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini akasema jukumu linalokabili viongozi wa kizazi kinachokuja ni jukumu la kuweza kuleta Uhuru wa kiuchumi na sasa hapa ndipo tunapo suasua kwa sababu katika kusoma historia yote tunaona kabisa ya kwamba suala la *production* ni muhimu sana, maana yake *role* ya Benki Kuu kwa kuirahisisha zaidi, ni ghala, kwamba vilivyovunwa viwekwa mule ndani halafu viweze kutumiwa kwa uangalifu. Sasa sisi tunaishi kwa kutegemea misaada, nchi za kigeni, *we live on foreign aids* na hata fedha ambazo tunatarajia kuzitumia kwa mipango yetu nyingi zinatokana na misaada tunayoomba na inafikia hatua ambapo hata *production* yetu ya chakula inaharibika inabidi tuanze kuomba chakula. Kwa hiyo, hili suala la *production* ni muhimu sana, sasa tuangalie *production* inategemea vitu vitatu, inategemea ardhi, inategemea nguvu kazi na inategemea mtaji yaani *capital.*

Kutokana na ardhi yaani *land* tunapata *rent,* kutokana na nguvukazi tunapata *wages* na kutokana na *capital* tunapata *interest,* sasa wakulima ambao ndio *majority* yaani ndio watu wengi katika nchi yetu na ambao tunatarajia ya kwamba fedha zitakazo toka kwao ndio hizo zitakazojaza ghala hawana uwezo wa kuzalisha tena kwa sababu kwanza hawana *incentive* yaani motisha na motisha yenyewe ni kwamba mkulima yeyote duniani ambaye anaitwa mkulima mdogo mdogo au tumuite *peasant* kitu ambacho anacho mkononi ambacho kinamfanya awe na moyo wa kuzalisha ni ardhi. Sasa sera yetu ya ardhi, pamoja na kwamba imekuwa *reviewed* ya mwaka 1999 inasema ya kwamba mkulima atapewa fursa ya kumiliki eneo fulani kwa ajili ya kilimo. Lakini ukiichunguza

vizuri ni kwamba sheria yetu ya ardhi inatoa *right of occupancy* lakini inatoa kwa watu kama wa miji, kwa kumiliki hati au mashamba makubwa yale yanayoweza kumilikiwa kwa hati lakini mkulima hatapewa hati ya kumwezesha kumiliki lile shama na kulitumia kama collateral ya kuomba hata mkopo.

Kwa hiyo, matokeo yake ardhi yetu haina *value,* mkulima anaweza akawa na eka hata ishirini lakini zile eka haziwezi zikampa kitu kutoka kwenye mabenki ambacho wanaweza kukitumikia kuzalisha, tofauti na ilivyo katika nchi za jirani, matokeo yake wakulima sasa hawawezi kuzalisha, hawa na motisha ya kuzalisha matokeo yake *production* ya chakula iko chini na sasa hivi tunakimbia tunaomba chakula. Kwa hiyo, kama *production* hasa katika upande wa kilimo haiwezi kuongezeka na kuimarika benki hii itashindwa kufanya kazi kwa njia inayofaa kwa sababu haitakuwa na kitu, itakuwa inategemea kuomba fedha, na kwa sababu benki hii vile vile inatarajiwa kwamba ndio inayo *manage* benki zingine ndogo na kuzipa leseni kulingana na hiyo *section* ya tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoambiwa ya kwamba ndege ilivamiwa, fedha zikachukuliwa zilizokuwa zinakuja Tanzania maana yake nini, ina maana hizo fedha zilikuwa zetu zinaletwa kwetu kutusaidia au walikuwa wanakuja kuleta *investment* ya kwao kwa sababu *investment* ni kama chambo, unaweka chambo kwenye ndoano ili uvute, sasa inaonekana ya kwamba *monetary policy* tuliyonayo imeruhusu uingizaji wa mitaji mikubwa kutoka nje ambayo imerudi inapata *returns* za *profit* kubwa ambazo tena zinapelekwa nje kwa hiyo Mtanzania anakuwa hana chochote.

Kwa hiyo, nafikiri hii *monetary policy* ambayo benki inatakiwa ku-*formulate* ni lazima kwanza iangalie suala la *production* kwamba ardhi imilikiwe na Watanzania wenyewe na wale Watanzania apewe kipande chake ambacho anaamini ya kwamba hiki kipande hata nikifa mtoto wangu atakirithi kwa hiyo anakuwa na *incentive* ya kuweza kutumia ile ardhi na vile vile akitumia kama *collateral* ya kuweza kupata mikopo kutoka kwenye benki ili sasa tuondoe ile zana ya kwamba Mtanzania hakopesheki, kwa sababu katika nchi zingine inaonekana wanakopesheka na ni Waafrika kama sisi.

Suala la *labour* yaani nguvu kazi sasa hivi tumewalazimisha vijana wetu kuwa *idle* yaani kuwa wazembe kwa sababu kama hana ardhi na nadhani kutokana na ahadi ya Rais wetu kwamba atawapatia vijana ajira mimi sioni ajira itatoka wapi kama sio katika sekta ya kilimo. Kwa sababu kila mtu ana uwezo wa kulima, kwa hiyo, kama wale vijana kwanza wangepewa ardhi halafu wapewe mikopo inayotokana na benki hii ni lazima wangezalisha na hii kelele ya kukosa ajira ingekosekana machinga, wengi wanao randa randa nchi nzima wangepungua, majambazi wameshamiri kila kona wangeisha na vile vile uchumi wetu ungeweza kwenda juu. Kwa hiyo, hii nguvu ili isipotee ni muhimu ya kwamba tuweze ku-*review Land Policy* ya nchi hii. Watu wanaposikia kwamba watu wanapigana Tarime naona Serikali ina *tendency* ya ku-*dismiss* lile neno kwamba hao ni Wakurya wako hivyo wanapigana.

Lakini sio hivyo lile ni suala la ardhi, upungufu wa ardhi kwa sababu mwaka 1974 wakati watu wanakwenda kwenye vijiji waliopewa ardhi ni baba zangu mimi. Sasa mimi hapa nilipo nina watoto na wajukuu watu wanaongezeka lakini ardhi haiongezeki.

Kwa hiyo, kwa sababu kwa lile eneo sasa linaonekana *empty,* ardhi ni mali ya Serikali basi wanavamia eneo lolote wana *collide* na koo zingine. Kwa hiyo, hiyo yote inatokana na *wrong policy* ya ardhi ambayo ndio ina *discourage production.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho ningependa tuangalie sana ni kuhusu hili suala *personal wood,* haya masuala ya *personal wood descriptions* nafikiri ni masuala ya *ancient* hata Serikali ya awamu ya kwanza ime-*deal* nayo. Muelewe kwamba kila nchi ina *interest* zake hata muwe na urafiki namna gani hata mkubali kwamba sasa mmeacha ujamaa ili muweza kuwa na ubepari ili msikilizane lakini kila nchi ina kitu kinaitwa *the vital interest of that nation* na hayo yote yanatokana na uzalendo, kwa mfano Waamerika wanaheshimu *constitution* yao kwa sababu ya uzalendo ambao wanao kama Waamerika, ukienda Uingereza vile vile hutakuta ya kwamba wale ma-*capitalist* wa kule Uingereza wametoka Ufaransa au uende Ufaransa ukute kwamba wanaoshilikia uchumi pale wametoka Ujerumani ni lazima kuwe *limitation* ya *influx* ya *foreigners* katika masuala ya kiuchumi. Waruhusiwe tu ku-*invest* katika maeneo fulani fulani lakini kwa sasa hivi inaonekana ya kwamba *foreigners* wana *right* za kuweza kuingia hapa na kumiliki chochote wakati wowote na ku-*influence policy* za nchi.

Mheshimiwa Naubu Spika, hiki ni kitu *dangerous* sana hiki tusipoangalia hiki kitatuletea mgogoro mkubwa na tunapoamka kuongea hapa kama watu wa vyama vingine inaonekana tunaongea kwa chuki lakini tunaongea kwa uchungu na hili sio suala la vyama hapa au kama vile ambavyo wote tunaonekana tuko *pre-occupied* hapa, Wazanzibar wako *pre-occupied* na Zanzibar wengine tupo *pre-occupied* na sera na ilani za vyama vyetu hili ni suala la *patriotism* kwamba hata Afrika Kusini yenyewe iko vile kwa sababu walikataa uchumi wa madini yao kumilikiwa na Waingereza na ikapigana vita *the boar war* 1898 mpaka 1902. *South Africa* imeneemeka kutokana na madini yake sasa haya madini yetu ya dhahabu, nimeona hapa imeelezwa ya kwamba Benki Kuu itakuwa na mamlaka ya ku-*regulate* na ku-*control gold.*

Mheshimiwa Niabu Spika, sasa kwa kuwa *gold* ndio kipimo cha nguvu ya *currency* duniani kote hili jambo la kuachia dhahabu yetu inachukuliwa inakwenda kabisa kabisa bila hata kuwa na *control* yoyote nadhani ni suala ambalo itabidi Serikali kwa kutumia Benki Kuu iliangalie kwamba zile *gold bullion* ambazo zingetokana na *reserve* za dhahabu yetu zilikuwa zinatosha kututajirisha kabisa, afadhali tusielewane na watu na *Briton wood* katika hili lakini tuweze ku-*retain* ile mali yetu kwanza halafu inaweza ikatupa *proper gain power* katika biashara zetu tutakazofanya. Lakini kama tutaachia hii mali ambayo kwanza ni *exhaustible* ibebwe sasa hivi wanachimba dhahabu kwa kasi na nguvu kubwa sana ili kwa ndani ya miaka kumi au kumi tano iwe imeisha. Sasa kama itakuwa imeisha hatutakuwa na umuhimu kwao tena bali tutaendelea kuwa taifa ambalo linatawaliwa na watu wengine. Kwa hiyo, katika *planning* yote ambayo inafanyika na Serikali, lazima vile vile tuweze ku-*consider time frame* kwamba haya mambo kwa sababu kuna *global competition* hatuwezi kukaa pale wakati watu wengine wao wana *plan* mambo yao yanafanikiwa tuone kwamba itachukua muda gani kuweza kujikomboa na matatizo haya yanayotukabili.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho pia ningependa kumpongeza Rais kwa jinsi ambavyo ameonyesha nia njema kwa hizi siku 100 na amekubalika kwamba ana nia njema na kutokana na yale aliyoyazungumza hapa tumeona kweli anachokizungumza na kinadharia lakini mimi nadhani hapati *support* ya kutosha na inaonekana ya kwamba pengine watu wa chama chake wanampinga zaidi katika kuleta mabadiliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sisi kama wapinzani tutaendelea kumpa *support* kwa sababu yale anayoyaongea ndio hayo tulikuwa tunayoongea na tunaelewa ya kwamba wananchi wengi sio wanahitaji *changes* maana siku hizi ukisikiliza habari ni Mzee Kikwete, Mheshimiwa Kikwete, Rais Kikwete hakuna mtu anayeongelea CCM tena kwa sababu wako kimya na wao wanaangalia kwa pembeni wanaona ya kwamba huyu mtu namna gani anakuja kutudhuru nini. Kwa hiyo, na sisi tukiwa nje ya *fencyi* tunayaona hayo yote ya kwamba huyu mzee hasaidiwi lakini nia yake ni njema na katika hizo siku 100 zimeonyesha na tunatarajia ya kwamba Watanzania wote watam-*support* ili kuleta haya mabadiliko ambayo yanatakiwa kuletwa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naunga hoja, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba niwashukuru wote waliopata nafasi ya kuchangia asubuhi hii, kadri tulivyoendelea orodha ya wachangiaji iliendelea kuongezeka na hatujafunga bado orodha ya wachangiaji, kwa hiyo, kama kuna watu watataka kuchangia ni vizuri wakaleta kusudi tuweze kupanga utaratibu wa kuendesha vikao vyetu, kwa sababu tukiwa hatujui sasa tunashindwa kuwaambia Mawaziri wafunge lini. Lakini *the list still open* unaweza kujaza.

Baada ya kusema hivyo naahirisha Kikao cha Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 06.56 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunanuia kwamba hoja hii iendelee mpaka siku ya Jumatatu kwa sababu kesho asubuhi tutaingia kwenye kipindi cha Maswali, baada ya hapo tutafanya ule uchaguzi tuliosema wa *institutions* tatu, halafu tutaungana na Rais katika kuwahutubia Wazee wa Dodoma jioni saa kumi. Kwa hiyo, tutaahirisha baada ya uchaguzi huo ili tukashiriki mazungumzo ya Rais na Wazee wa Dodoma. Kwa hiyo, hii hoja itakwenda mpaka siku ya Jumatatu. Kama kuna watu waliokuwa wana wasiwasi kwamba labda imefungwa, basi bado iko wazi.

**MHE. FELIX C. MREMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia mchana huu. Nitumie pia nafasi hii kumpongeza Waziri, Gavana pamoja na Watendaji wote kwa kuwasilisha Muswada huu muhimu wenye madhumuni ya kupendekeza kutungwa kwa Sheria mpya ya Benki Kuu 2006 na kufuta Sheria ya sasa

ya Benki Kuu sura ya 197. Niseme tu bila kupoteza wakati kwamba naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri wa Fedha na Serikali nzima kwa sababu huu ni msururu wa Miswada muhimu inayoelekeza kwenye Sekta ya Uchumi kwa ajili ya kujibu kwa vitendo zile ahadi zilizotolewa na uongozi wa Chama cha Mapinduzi walipokuwa wanaomba kura mwaka jana 2005. Katika kikao kilichopita, tulipitisha Miswada miwili ya *Special Economic Zone* na nyingine *Export Processing Zones.* Sasa safari hii kuna Miswada mingine miwili muhimu hii ya Benki ya Tanzania na ule Muswada wa Sheria ya Mabenki na Taasisi za Kifedha. Sasa zote hizi ni ushahidi dhahiri kwamba Serikali kwa vitendo imeanza kwa nguvu na kasi mpya ya kushughulikia masuala ya kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Waziri alipokuwa anawasilisha Muswada huu alisisitiza kwamba Muswada huu umetungwa ili kukidhi matakwa ya wakati huu. Sasa Gavana alipokuwa anatueleza kwenye Semina alinifariji mimi sana alipokubaliana pamoja na Waziri na mapendekezo ya Kamati ya Fedha na Uchumi ya kuhakikisha kwamba mabadiliko yanafanywa kwenye Muswada ulioletwa ili kuweka yale mambo muhimu ya wakati huu. Mambo muhimu ni yale yaliyoainishwa katika Awamu ya Pili ya mageuzi katika Sekta ya Fedha, yaani *Second Generation Financial Sector Reform* inayosimamiwa na Benki Kuu.

Sasa kwa kukubali kufanya mabadiliko hayo na mabadiliko hayo yamefanywa walipokubali kuongeza kwenye majukumu muhimu ya Benki Kuu maneno yafuatayo kwamba moja ya majukumu muhimu ya Benki Kuu yatahusisha *Mortgage Finance, Development Finance* na *Leasing Financ*e. Sasa baada ya kukubali kuubeba mzigo wa namna hiyo, mimi naridhika kabisa kwamba wameanza kufanikisha hayo ambayo yanategemewa katika hii *second generation* ya *reform* kwenye Sekta hii ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna ubishi kwamba katika mfumo wa sasa hivi lipo pengo kubwa katika utoaji wa mikopo ya muda mrefu hasa katika Sekta ya Uzalishaji. Hiyo haina ubishi. Sasa kazi kubwa baada ya Benki Kuu kukubali kubeba mzigo huo ni kuweka mazingira bora ya kuanzisha mikopo hii ya rehani, yaani hiyo *Mortgage Finance*, mikopo ya kukosha mitambo, matrekta, vifaa vingine vya kilimo na kadhalika, *Lease Finance* pamoja na mambo mengine hasa lile ambalo linahusu utoaji wa mikopo ya muda mrefu kwenye Sekta ya Kilimo na Viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama tunakiri kwamba kuna pengo, basi ni wajibu wetu na kusema kweli mimi sidhani kama kuna nchi yoyote ambayo ilikuwa inaendesha uchumi wake bila kuziba pengo kama hili ni sisi peke yetu nafikiri ndiyo tulikuwa tumebakia na pengo kama hili. Sasa kusema kweli *it was long over* kuziba pengo hili. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa kutambua na nia yangu kwamba sasa baada ya kutambua hilo wataanza kazi hiyo kwa kazi inayohitajika ili tu-*catch up* na hao wenzetu ambao wametuacha mbali sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwenye hili nitajaribu kuweka mkazo zaidi kwenye mambo mawili tu. Nitajaribu kuzungumzia juu ya *Mortgage Finance.*

Ninapoitazama mimi yamekwishazungumziwa na wenzangu na mimi nitazungumza kwa maneno yangu na nitazungumza pia juu ya *Development Finance* jinsi ninavyotegemea Benki Kuu ibebe mzigo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa majengo ya kuishi au biashara popote duniani yanajengwa kwa mikopo ya muda mrefu na kawaida ni kati ya miaka 20 na 30, hiyo ndiyo *standard* mahali popote duniani. Sasa Mabenki au Taasisi za kutoa huduma zimejipanga na zinawezeshwa ili kuweza kutoa mikopo ya namna hiyo ya muda mrefu miaka 20 mpaka 30, hapa kwetu tulikuwa na *THB* ni kweli ilikuwa na matatizo lakini kwenye Taasisi kama hizi siyo jambo la ajabu kuwa na matatizo. Sisi tulishauriwa na tukakubali kwamba kwa sababu ya matatizo *THB* tuliyokuwa nayo tuache ifilisike.

Nchi nyingine Taasisi kama hizi zikipata matatizo hawaziachi zifilisike bila kuwa na mbadala. Wanatafuta njia ya kuzisaidia kuzi-*restructure* ili ziendelee kufanya kazi hiyo muhimu katika uchumi wa Taifa. Sisi bahati mbaya hatukufanya hivyo tukaacha ifilisike na tunangojea sekta ya binafsi yenyewe ifike mpaka mahali ambapo itakapofanya kazi hiyo, bahati mbaya mpaka leo hii sekta binafsi ya mabenki haijaweza kufanya kazi hiyo. Kwa nini hawajaweza kufanya kazi hiyo? Kwa sababu mwelekeo wao ni mwelekeo wa *short time and medium time* miaka mitano kabisa, kama mmeangalia mbali sana ni miaka mitano, kuangalia miaka 20 mpaka 30 mpaka sasa hivi *it is not attractive enough for these financial institution or Banks* kuwa na mtazamo wa namna hiyo.

Pili, soko letu hapa la sekta hii ya majumba ni ndogo mno, wanasema kwamba kwa mwaka sisi tunajenga nyumba ambazo hazizidi 1000 katika nchi nzima katika kipindi cha mwaka mmoja kwa sababu mfumo wetu wote wa kujenga nyumba ni *cash* na kwa sababu mfumo wa kujenga nyumba ni *cash* unatafuta Shilingi milioni 20 mwaka huu una-*succed* kupata milioni 20 unaifikisha kwenye *lintel* unangoja mwaka mwingine, unapata milioni tano unaipandisha juu, inachukua miaka mitatu au minne au mitano kujenga nyumba moja ya kuishi. Sasa ni uchumi ambao ni duni sana ambao unamfanya mtu ajenge nyumba kwa kipindi kirefu namna hiyo na kwa utaratibu wa namna hiyo. Kwa hiyo *it is not attractive.*

Mahali pengine hebu tuangalie, hatusemi kwamba wanajenga nyumba 1000 katika nchi, ni kutokana na *demand* iliyopo, lakini nyumba za kuishi mbili, lakini sisi tukifaulu sana katika kipindi cha mwaka mmoja ndiyo 1000. Hebu tuangalie wengine jirani wanafanya nini.

Kenya taarifa tulizonazo wanasema wao uchumi wao kwa kila mwaka wanafaulu kujenga karibu nyumba 50,000. Siyo kwamba hawana *deficit*, Kenya wana *deficit* karibu 600,000 za nyumba ambazo zinahitajika, sekta inashindwa ku-*satisfy* lakini wamekuja na mpango wa makusudi kabisa wa kujenga nyumba 150,000 katika kipindi cha miaka hii mitatu toka hii Serikali ya *NARC* ianze kuchukua madaraka na pamoja na matatizo yote wanakazana kufikia hayo malengo yao.

Uganda nayo hivyo hivyo, wana kitengo kinachoitwa *National Housing and Construction Company Limited.* *National* yao wameigeuza siyo *National* tu ya kupangisha ni *National Housing* ya *Construction* ya nyumba na kumilikisha wanaokaa kwenye nyumba hizo. Hizi nyumba walizokuwa nazo *National Housing* siyo kupangisha tu *for the sake of* kupangisha.

Sasa wao wana mkakati wa makusudi kabisa kwa miaka mitano ijayo wameipatia Taasisi hiyo ya *National Housing and Construction Company dollar 321,000,000* kwa ajili ya ujenzi wa nyumba makusudi kabisa. Sasa wanatambua hiyo kwa sababu kwanza ni ajira. Kila nyumba moja inayojengwa ina ajira isiyopungua 10, wakiweza kujenga 10,000 unakuwa una 100,000 ya ajira pale mara moja wanajua kwamba hii ndiyo njia ya uhakika na usahihi ya ku-*create* hiyo *million plus* inayotakiwa na ndiyo njia ya uhakika ya kusaidia uchocheaji wa ukuaji wa uchumi ikifikie kile kiwango cha asilimia nane au tisa tunayoitaka kwa kipindi cha miaka 10 ili kuweza kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nategemea sasa baada ya kuipa Benki Kuu uwezo wataichukulia kazi hii kwa uzito unaostahili. Mheshimiwa Magufuli najua wewe ndugu yangu una nguvu na kasi inayoeleweka,. Mwelekeo wako wewe uwe sasa ni kuisukuma Wizara ya Fedha na Benki Kuu ili waiwezeshe *National Housing Corporation* waweze kufanya kazi hii ambayo sasa hivi haifanyiki katika Taifa letu. Mtauliza fedha zitapatikana wapi?

Fedha, *Governor* alituambia mabenki mwaka jana yalitumia Dola bilioni 1.4 kununua *Treasures Bills* kununua karatasi tu, wanapata faida yao kwa kula kuku kwa mrija kiulaini kabisa, sasa ni changamoto kwa Benki Kuu kuwaambia hapana hizi pesa hizi msizipate kwa urahisi ielekeze katika Sekta hii ya uzalishaji hasa katika ujenzi wa majumba haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mategemeo yetu kwamba sisi kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi tutakuwa wakali kweli kwenye kuisimamia Benki Kuu kuhakikisha wanapokuja mwakani na bajeti, suala hili lipewe uzito unaostahili ili kweli hizi ahadi zinazotolewa zianze kuzaa matunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kusema ni suala la *Municipal Bonds.* Katika Muswada huu Benki Kuu ina mamlaka na uwezo wa ku-*deal directly* na *City Councils, Municipal Councils* ku-*act as the fiscal agent or banker* na kuwasaidia katika shughuli nyingine zote za maendeleo ya uchumi.

Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja pale Arusha mwanzoni mwa mwaka akatembelea soko letu la Arusha la Ngarenaro, akaona hali ni mbaya sana. Mimi na wananchi wa Arusha tunamshukuru kwamba alipoona hali ilivyo mbaya kule akaahidi kwamba atasimamia Taasisi zetu za Serikali ili tutumie fedha za *TASAF* ziweze kujenga soko la kisasa pale Ngarenaro. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Lakini utafiti wangu unaniambia kwamba pesa hizo za *TASAF* hazitatosheleza kujenga soko la kisasa pale Arusha, njia nzuri na ya uhakika ni Benki Kuu ingelitusaidia sisi ku-*package a municipal floating of a bond* tuweze kupata pesa kwenye soko tutakayoisimamia na

kuilipa katika kipindi cha miaka hiyo 20 kwa sababu hili ni jengo tuweze kutengeneza kitu kinachofanana na Jiji la ...

*(Hapa umeme ulikatika na kurudi baada ya muda mfupi)*

**MHE. FELIX C. MREMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, dakika zangu naomba niongezewe, zimechukuliwa na kuzimika kwa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mategemeo yangu kwamba katika kuubeba mzigo huu wa kutusaidia sisi kwenye *City Council* na *Municipal Council* na hii nafikiri ita-*apply* pia kwa wenzangu wa Temeke. Soko lao liko kama la kwetu Ngarenaro. Yote yanahitaji msaada wa fedha nje ya mfumo wa bajeti kwa sababu mfumo wa bajeti hauwezi ukafanya kazi hii kubwa ambayo tunataka kuifanya ya ujenzi wa miundombinu katika Miji yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nizungumzie hili suala la *Development Finance. Development Finance* kama nilivyosema ilikuwa haipo bado, ni pengo wamejaribu Benki Kuu kupitia hizi *guarantee schemes* tatu walizokuwanazo kujaribu kuziba hilo pengo lililopo katika mfumo mzima wa uchumi wa Taifa letu. Sasa kinachotakiwa sasa hivi ni ku - *instutionalize* kuimarisha Tanzania *Investment Bank* au Benki nyingine yoyote ili iweze kufanya kazi hii kwa uwezo ambao unaweza kupatikana huku huku nchini na kwa nguvu na kwa kusimamiwa vizuri na Benki ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba kwenye hili Benki ya Tanzania walipata mkopo kutoka *European Investment Bank* ya *Euro* milioni tisa kwa ajili ya kutoa mikopo ya muda mrefu kwenye Sekta za Uzalishaji. Lakini taarifa nilizonazo ni kwamba mpaka wakati huu pesa hizo ambazo zilipelekwa kwenye mabenki ya biashara hazikuweza kufikishwa kwa walengwa kwa sababu zilionekana kwamba *Administrative Cost* zake *was too much for the bank to be attracted* kusimamia mradi wa namna hiyo. Sasa ni wajibu wa Benki Kuu kuhakikisha kwamba wanatengeneza mfumo ambao zikipatikana pesa za namna hiyo tuwe na *institution* ambayo ina *capacity* na uwezo wa kuitumia na kufikisha kwa walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia katika hoja hii muhimu. Napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kutuletea Muswada huu katika kipindi hiki ambapo lengo la Muswada huu ni kutaka kuleta ufanisi zaidi katika vyombo vya fedha na zaidi katika kuchangia katika kuinua uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wachangiaji wenzangu waliotangulia wamekuwa wakinifilisi hapa na pale, lakini kwa kuwa nilikuwa nimeshajiorodhesha kuchangia, nitapenda kusisitiza katika maeneo fulani fulani ama kuweka kwa namna ambazo naona

na mimi mtazamo wangu ambavyo ungeweza kuwa ni wa hoja fulani chache ambazo napenda kuzizungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema kwamba Watanzania wanapenda sana na wako mstari wa mbele kuona wanashiriki katika zoezi zima la kuinua hali ya uchumi kwa Mtanzania mmoja mmoja na hata kwa makundi pale inapowezekana. Lakini ukianza kutazama katika Benki tulizokuwanazo kabla ya kipindi hiki, ni kwamba Benki zetu nyingi sana zilikufa ambazo zilikuwa ni Benki za Watanzania wenyewe. Baada ya benki zetu kufa sasa, Benki zetu nyingine zikafungwa kabisa ama zikafutwa kabisa na kwa hiyo, tukapata Benki nyingine mpya ambazo zimeanzishwa na nyingi zinaendeshwa kwa mtindo wa waendeshaji kutoka nje.

Kinachonifurahisha na ambacho kinanishangaza ni jinsi ambavyo Benki zimekuwa zikiongezeka kutoka siku hadi siku katika nchi ya Tanzania. Sielewi Benki zetu zilikufa kwa sababu gani, kwa sababu kila mwaka Benki zinatangaza kupata faida kubwa hali inayoonyesha kwamba Tanzania panawekezeka unapotaka kuwekeza katika mabenki.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hali hii ukiendelea kuichunguza unakuta kwamba Watanzania wengi sasa hivi ambao ni Watanzania wa kawaida kwa maana ya wakulima wa kawaida tu hawaweki fedha zao Benki, pengine sababu mojawapo ni ile kwamba faida ni kidogo kwa yule anayewekeza lakini, vilevile Benki zimefungwa katika maeneo mengi. Nilikuwa najaribu kumfikiria Mtanzania anayeishi Mkoa wa Kagera, kama anataka kwenda kuweka pesa zake kwa mfano Benki ya *NBC*, mwanakagera aende kilomita 200 mpaka 300 kama anatokea maeneo ya Ngara na maeneo ya Biharamulo ili aweze kufika Bukoba Mjini kuweza kuweka pesa zake katika Benki ya *NBC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii inatisha. Watanzania wanaweka pesa zao majumbani zinaliwa na mchwa, nondo, zinaibwa, nyumba zinaungua na pesa zinaungua, lakini ukweli wenyewe hawawezi kwenda kufika Benki, kwanza kwa umbali na kwa udogo wa pesa wanazokwenda kupeleka. Mimi nilikuwa nashauri kwamba Benki ziweze kuenezwa maeneo wanakoishi watu pamoja na kwamba kweli Benki za sasa zinatafuta kupata faida kubwa lakini ni vizuri Benki zikawa ni kwa ajili ya kuwasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo basi, mimi nashauri iwepo elimu ya kuwaelimisha Watanzania namna ya kujiwekea akiba Benki kwa sababu hakuna mtu anayeweza kujijengea mtaji wake mwenyewe kama hawezi kuwa na tabia ya kujiwekea kidogo kidogo. Kidogo kidogo ndicho kinachojenga tabia ya kuweza kupata kikubwa baadaye hata inapokuwa anapata msaada wa kuchangiwa, kama iko haja ya kufanya hivyo au anapata bahati ya kufanya hivyo, ataweza kutumia vizuri ile rasilimali yake kama amejenga tabia ya kuweka kidogokidogo na kwa hiyo kujipangia matumizi yake kidogo kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ambalo pia limejitokeza katika Benki zetu ni pale ambapo Watanzania wanapotaka kwenda kukopa zile fedha ambazo hata wao wameweka wenyewe. Riba ya kukopa inamzunguka yule mwenye kukopa

karibu ya mara tatu ya faida ambayo yeye mwenyewe anategemea kuipata kwa fedha zake mwenyewe.
Kwa Msingi huo, watu wanahofia kuanza kuchukua zile fedha kuzikopa, lakini hakuna faida ya kuweka fedha Benki kwa sababu wewe uliyeweka unapotaka kwenda kutoa ile, ukafanye shughuli zake mwenyewe za kusaidia. Wewe unailipa Benki mara nyingi na ndiyo maana Benki zinapata faida kubwa kwa sababu zinawatoza Watanzania fedha nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mimi nadhani hili jambo liangaliwe sana. Tuwe na Benki ambazo zinalenga kuwajenga Watanzania zikielewa kwamba tuna vipato vya Watanzania wakulima, Watanzania wafugaji, Watanzania wafanyakazi, Watanzania wafanyabiashara na Watanzania katika makundi yote hayo wako makundi madogo na makubwa. Benki hizi ziwe kwa ajili ya makundi yote ya Watanzania. Wafanyabiashara ndogo ndogo waweze kuweka kidogo kidogo na waweze kutoa kidogo kidogo na hata mikopo iwe katika makundi. Sasa hivi mtu anayekwenda kukopa mkopo mdogo Benki ndiye anayetozwa riba kubwa kupita kiasi. Benki hizi zijali hali hizo za Watanzania, iwe mikopo midogo na yenye riba kidogo, iwepo mikopo mikubwa na yenye riba kubwa.

Ni kweli tunataka mambo yetu yaende vizuri kama Mataifa mengine yanavyokwenda, lakini Rais wetu ametuambia kwamba watu wanalazimika kuiga kila kitu kwa sababu tu wanataka kuwafurahisha watu wengine. Sasa hiyo iwe katika mabenki. Benki isitake kufanya kazi katika kuangalia Mataifa yote duniani yanavyofanya wakati Watanzania wanaumia. Kwa hiyo, iwe ni Benki ambayo inalenga Watanzania wa makundi yote na kuwawezesha Watanzania kuweza kuingia katika Benki hizo kukopa na kwenda kufanya kazi za kuinua uchumi na kujiondolea matatizo yao yanayowakabili siku hadi siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kushauri kwamba Benki zetu pamoja na kwamba zinalenga biashara na kuinua uchumi zijali jamii inayowazunguka. Kwenye mirabaha, tunasema wajenge Shule, barabara, waweke maji ili wananchi wanaokaa maeneo hayo na wenyewe waweze kufaidika na kitu hicho. Sasa na Benki zetu zinazopata faida kubwa Tanzania zilenge kuinua hali ya maisha ya Watanzania, ziweze kuchangia hasa katika maeneo ambayo ni magumu kwa mfano upande wa watoto yatima. Watoto wengi sana ambao ni yatima Tanzania bado hawajaweza kupokea misaada ya namna mbalimbali.

Tunashauriwa kuwachukua watoto yatima kukaa nao ili wajisikie wako majumbani, lakini bado ni suala gumu kwa sababu hata familia zetu wenyewe tulizokuwa nazo bado zinakuwa ni ngumu kuzitunza. Sasa inapokuwa unakwenda kuchukua yatima kuishi naye maana yake ni kuzidi kuongeza ugumu katika ugumu wa familia. Kwa hiyo, ni lazima tutafute utamaduni wa kujaribu kuongeza vituo vilivyo vizuri vinavyofanana nyumbani ili watoto wajisikie wako kama nyumbani japo katika vituo vya kuwalea. Sasa hayo mabenki wachangie yasitutangazie tu faida kubwa ya mabilioni ya fedha wakati huku watoto wetu wanaendelea kuteseka na wale ni Watanzania wajao kwa sababu ndani ya watoto yatima wako ambao ni wazuri kesho, keshokutwa watageuka kuwa ni viongozi

wa nchi.  Lakini wawe wamelelewa, wameangaliwa, wamepewa elimu nzuri, wametunzwa vizuri, kuweza kujenga moyo wa kizalendo na kusaidia Taifa lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ninalotaka kuzungumza, napenda nizungumzie juu ya uteuzi wa Gavana. Naziunga mkono sifa ambazo zimeonekana zinafaa kwa gavana, lakini ukitazama vile vipengele vitatu vilivyoorodheshwa pale katika ibara ya nane ni vizuri sana kweli tukapata mtu mwenye upeo mkubwa wa kielimu na ujuzi wa kielimu.

Lakini suala zima la kuangalia muda wa miaka 15 halafu unasema huyu anaweza akateuliwa tena baada ya miaka mitano, mimi naona kama hii ya kuteuliwa tena pengine haizingatiwi sana kwa sababu miaka ya 15 ya uzoefu ni mingi mno. Mimi nilidhani miaka 10 inaweza kuwa imemtosha Mtanzania kwa sababu, chukulia Mtanzania wa kawaida aliyesoma kikawaida na kufanya kazi miaka kumi, umri wake unakuwa umeshakaribia miaka 40 ama umezidi kidogo miaka 40.  Kama tunaweza kuwa na Katiba unayosema kuwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania anaweza kuwa na umri wa miaka 40, mimi sioni kwanini Gavana wa miaka 40 asiweze kuwa Gavana, sijaona hapo. Naona hapo sijui kwa sababu nafasi ya Urais ni kubwa mno na majukumu ni makubwa mno ya kutazama nchi na mambo mengine!  Kwa hiyo, mimi naona nafasi ya Gavana wa Benki Kuu ni vizuri naye ile miaka 15 aliyowekewa ikapunguzwa.

Lakini la pili katika huyo Gavana nilikuwa najaribu kutazama katika suala la uaminifu na uadilifu. Huyu mtu tunatakiwa kumkabidhi majukumu makubwa kabisa, anakuwa Mwenyekiti, anakuwa Gavana na kadhalika. Kwa Msingi huo, niliamini kwamba suala zima la uaminifu, uadilifu na uzalendo wake katika kusimamia fedha za nchi, uchumi wa nchi na moyo wa kupenda nchi yetu vingekuwa ni vitu ambavyo japo havikuandikwa katika Muswada huu kuwa ni sehemu ya Muswada, lakini viwe katika kuangaliwa na kuzingatiwa ili kuona kwamba Mtanzania anayeweza    kupewanafasi hii awe ni yule ambaye ametazamwa kwa vigezo vya uadilifu, uaminifu na uzalendo wa hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nilikuwa nazama kuanzia nafasi hasa za Viongozi Wakuu, Gavana na Wasaidizi wake ambao ni *Deputy Governors* watatu ni jumla ya watu wanne. Watu hawa wanne hakujasemwa kwamba angalau mmoja awe mwanamke.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania na sasa kimataifa, suala  la *gender quality* na *gender mainstream* ni suala ambalo sasa hivi liko mstari wa mbele.  Kwa hiyo, nashauri kwamba miongoni mwa watu hao wanne kuanzia Gavana mpaka kufika kwa hao Wasaidizi wake angalau mmoja wao aweze kuwa ni mwanamke.   Watanzania wanawake wenye uwezo na wenye ujuzi unaolinganalingana kabisa na hizi sifa zilizomo ndani ya Muswada huu, mimi ninaamini Watanzania wanawake wapo.  Kwa hiyo, ninashauri kwamba miongoni wa watu wanne Gavana na Wasaidizi wake watatu, basi mmoja wao aweze kuwa ni mwanamke.  Hili naomba lifikiriwe na itakapokuwa imetekelezwa, basi tuweze kupata mwanamke mmoja katika viongozi hao wanne.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ninapenda mimi kuzungumzia ninaomba Benki yetu iweze kusaidia kudhibiti hii habari ya thamani ya fedha ya Tanzania. Sasa hivi inafikia mahali kila mmoja anatamani kama tungekuwa tunapewa mshahara kwa fedha za kigeni. Kwa sababu kila siku asubuhi fedha yetu inateremka thamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya namna hii haifanyi uchumi wetu ukaweza kuwa ni imara, uchumi wetu unayumbishwa! Kwa msingi huo, kuwepo na kila namna inayojulikana, wataalam wetu wanajua kwamba ni vipi ambavyo wanaweza wakasimamia uimara wa sarafu yetu ya kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wangu, hayo niliyochangia ndiyo yale niliyokuwa nimepanga kuyazungumza. Ninaomba kusema kwamba ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama katika kuchangia hoja hii, lakini awali ya yote nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Hakika napenda sana kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha kazi aliyoifanya yeye na Manaibu wake pamoja na Makatibu Wakuu. Utadhani Mheshimiwa Waziri amekuwa Waziri kwa muda mrefu sana katika Wizara ya Fedha. Ahsante sana Mama Zakia Meghji. *(Makofi)*

Pili, nataka kumpongeza Mheshimiwa Gavana na Benki na Watendaji wake wote hasa wale wa karibu kwa kazi nzuri waliyotuletea katika Muswada huu. Lakini kabla ya pale nilitaka kusema, lingekuwa jambo zuri Waswahili wanasema; "Mcheza kwao utunzwa." *Bank of Tanzania* baada ya uhuru ilifanya kubwa sana tukawa *reserves* mpaka Wakoloni. Hawa wazungu walikuwa wanasema tunawatia haya kwa kuwa tuna hela nyingi kwenye miaka ya 1960 mpaka 1975.

Tulivyoingia katika vita ya Nduli Idd Amin tulikwenda pale kifua mbele kabisa na mtakumbuka baada ya vita Andrew Young aliwahi kumwambia Marehemu Baba wa Taifa tufanye nini *martial plan* kwa ajili ya Tanzania maana umetoka vitani? Marehemu Baba wa Taifa akamwambia, hapana, nina uwezo wa kusimama. Akasimama, lakini ukame nao ukaja huo kwa vipindi vingi, tukapata matatizo kweli ya uchumi. *Bank of Tanzania* ilikuwa pale tunakwenda pamoja. *Bank of Tanzania* leo ina *reserve* ya kutuwezesha kufanya biashara miezi tisa. Sasa hili sio jambo la mchezo. Hongera sana Gavana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nilitaka vile vile kuwapa hongera Kamati ya Fedha na Uchumi kwa kazi yao nzuri waliyoifanya. Sitaki kwa kweli kuchukua muda mrefu kwa sababu mambo mengi mazuri yamezungumzwa. Lakini nadhani ningeomba tufungue kitabu hiki ukurasa wa 31 *section* seven na *sub-section No. 2*. Hapa mimi naona imeelezwa hapa kwamba kazi ya Benki kubwa sana, shughuli za Benki ni kusimamia kujenga uchumi na kuleta maendeleo ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwangu mimi nadhani maendeleo ya nchi hii yagawanywe katika makundi mawili. Kundi la kwanza, maendeleo Mijini, ingawaje hawa watu wa Mijini ni asilimia 20 tu ya Watanzania wote, lakini inaonekana fedha nyingi zinatumika kuleta maendeleo Mijini. Kuna waliopata mikopo mikubwa, kumejengwa mahoteli na biashara kubwa na viwanda vikubwa. Ingekuwa unazungumza haraka haraka ungesema ahaa, hiyo inatosha. Lakini haitoshi. Bado kuna kilio cha watu wa Mijini kimeishazungumzwa kwamba hatutaweza kujenga majumba kwa fedha *cash* kila siku. Nikitaka *furniture* nilipe *cash*, nikitaka gari nilipe *cash*, haya mambo Benki Kuu ingechukua kama ni vishawishi vya kudokoadokoa kuvimaliza hivi. Muswada umeeleza vizuri, kuna *Mortgage Banking,* na mimi nadhani sisi wote tunakubali kwamba Muswada huu upite na hii *section* ya *Mortgage Banking* itazamwe vizuri na ifanye kazi haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wengi, karibu wote wakija Dodoma hapa tunabeba fedha nyingi kweli kwa ajili ya kulipa hoteli na hivi. Lakini *credit card system* ikipanuliwa na ikasimamiwa, tunaweza kabisa kufanya biashara hizi bila kubeba fedha na huku tuna hatari ya kuibiwa. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani *Mortgage Banking* iliyopanuka kwa maana ya ujenzi wa majumba, ununuaji wa vitu, magari na *credit cards* iliyopanuka kuwawezesha watu wote ilimradi tu mtu ana anwani yake na vile vile ana sehemu ya kazi na ana mshahara. Nilikuwa nazungumza na ndugu zangu kule wakasema ipo siku hizi *credit*, lakini naona *very selective.* Naomba Mheshimiwa Gavana ipanuke na tuitumie kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine ukitazama sehemu ya pili ya uchumi ni ile sehemu ya uchumi au kuujenga uchumi Vijijini. Watanzania asilimia 80 wanaishi Vijijini. Kule asilimia 80 ni wakulima na wakulima hao katika Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi imesemekana pamoja na kwamba wanalima kwa jembe la mkono, wamechangia uchumi wa nchi hii kwa asilimia 50. Hilo ni jembe la mkono kwa mkulima mmoja mmoja. Hapa nadhani Benki Kuu ikubali kwamba ukiwa na mbuzi anayetoa maziwa, basi apewe nyasi nyingi na maji ya kunywa. Wanavijiji hawa watazamwe. Maana yake nini? Maana yake Benki iwe na utaratibu wa kutuhakikishia namna ya kupanua mashamba hayo na namna nzuri ni kuwa na utaratibu mzuri wa kukopesha matrekta kwa masharti nafuu na ambayo yanaashiria malipo yawe kwa muda mrefu. Kwa sababu huyu ndiye ng'ombe anayetoa maziwa.

Fedha zilizotoka katika *Banking System* kwenda katika *industrial*, biashara hizi na majumba mengine mengine ukilinganisha *return* yake bado utakuta kilimo kinatuambia kitatupa majibu mema haraka zaidi kuliko hivi viwanda. Lakini hii ni ya mpito tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kilimo kikitupeleka mbele haraka *modernization* utakuta *industrial* nayo itapanda halafu baadaye *industrial* itachukua nafasi ya kilimo na mkulima mmoja mmoja baadaye nadhani atakuwa *relevant.* Tutakuwa sasa tunakwenda katika mashamba makubwa ya ulimaji wa kibiashara. Lakini hii *entering period* Benki Kuu lazima ikubali inayo dhima ya kuhakikisha kwamba huyu mtu anayenipa *fifty percent as the economy* namsaidiaje. Kule Vijijini kuna wakulima, kuna wavuvi na kuna wafugaji kule na shughuli nyingine za Kijiji, Benki

Kuu inatusaidiaje? Basi kuwe na utaratibu wa kuzisaidia *SACCOS* za Kata! Sisi Waheshimiwa Wabunge twende kule kwenye Kata zetu tuunde *SACCOS* na Benki Kuu tunaiomba ikubali hizi *SACCOS,* ndiyo zitakuwa Benki Kata za mwanzo zipewe nafasi ya kukopa fedha kwa masharti nafuu ziwakopeshe wananchi wajiendeleze katika shughuli zao za kuzalisha mali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ulimaji huu wa kutumia jembe la mkono tumefika hapo, hivi tukiwakopesha matrekta, tukiweza kweli kuipa kila Kata *SACCOS* yake fedha ya kutosha ya kununulia mbolea, kununulia mbegu za kisasa za mahindi zinazoiva kwa miezi miwili, kununulia mbegu ya mpunga ya kisasa inayoiva kwa miezi mitatu na kuinua ukulima wa pamba, tutakwenda mbele sana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napenda sana kukubaliana na Ilani ya Chama cha Mapinduzi katika uchumi imesema, kama tukiweka fedha katika kilimo tutanyayuka haraka zaidi kwa hali ya sasa kuliko njia nyingine yoyote. Kwa hiyo, naiomba Benki Kuu ikubali kugeuza macho yake kufungua ukurasa mpya na kufanya kazi na wakulima wadogo wadogo tuwatoe katika jembe la mkono tuwapeleke katika kilimo cha kisasa na hiyo ndiyo maana ya Mheshimiwa Rais wetu anasema tutoke hapa tulipo, sio kukimbizana tu hapana, tutatoka katika kutumia jembe la mkono tutakwenda kutumia trekta, tutaishi katika uchumi wa kopa tumia lipa, kopa tumia lipa. Huo ndiyo uchumi ambao tunataka kusema labda ndiyo endelevu na ndiyo uchumi wa kisasa, tunaweza ilimradi Benki Kuu itusaidie. *(Makofi)*

Mwisho, Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumuunga mkono msemaji aliyepita. Kuna masafa marefu kati ya chombo cha fedha na wenye fedha mathalani uzalishaji. Mimi kule kwetu Rufiji, Utete kwenda Benki moja iko Kibiti ni kilomita 84 na Utete ndiyo Bomani, watumishi wako wengi na pana shughuli pale za kifedha. Lakini hawa watu lazima waweke fedha katika vikapu vyao watembee kilomita 84 wakapeleke hela Benki. Halafu wakitaka kuchukua waende tena *notwithstanding* nauli na adha za njiani na watu siku hizi wanajua mishahara hiyo inakwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nadhani jambo la kufanya ni kuiomba Benki Kuu inapotoa leseni kwa mtu yeyote anayetaka kuanzisha Benki, ingemwomba amwambie kama anataka kushughulikia sehemu gani ya *rural area* aweke Benki iliyo karibu na wananchi, kama hawezi aseme, basi atuletee hata *Agency* yake na kuwe na *incentive* kwa wale ambao wanakubali kusaidia kupeleka vyombo vya fedha karibu na watu. Aidha, majibu yatoke mapema ya leseni hizo au hata wawapunguzie zile gharama za leseni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana kusema kwamba Benki hii imeshafanya kazi nzuri sana, Benki hii imeomba nguvu mpya, tunaipa nguvu mpya na Benki hii haijatuangusha, nina imani kama wakitilia mkazo maendeleo ya kilimo Vijijini uchumi utakua zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba kuunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu wa Sheria ya Benki Kuu. Nami naanza kwa kuwapongeza wote waliohusika na kushiriki kutengeneza na hatimaye kuwasilisha Muswada huu ambao sasa hivi tunaujadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nianze moja kwa moja kuunga mkono Muswada huu kwa matarajio makubwa ya ufanisi wa chombo hiki muhimu sana kwa kuinua uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Sheria hii inalenga uwazi na uwajibikaji katika utekelezaji wa majukumu ya Watendaji kwa kiwango cha Kimataifa, ni wazi kutakuwa na mabadiliko yenye kuleta ubora na ufanisi katika uchumi wa nchi yetu kwa kukidhi matarajio ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu kwa sehemu kubwa umezungumziwa na wenzangu, lakini nina maeneo machache ya kuongezea. Kwanza, mimi binafsi nimefurahishwa na suala nzima la Benki Kuu kudhibiti na kusimamia fedha zote za wananchi zinazokusanywa na Taasisi ndogo ndogo hasa za sekta isiyo rasmi kwa mfano, *SACCOS* na *SACCAS* na baadhi ya *Microfinancial Institutions (MFIs)*.

*SACCOS* ni Taasisi ambazo zinakusanya fedha za wanachama wake kwa makusudi ya kuja kuzikopesha. Hali kadhalika na baadhi ya *Microfinancial Institutions*. Sasa kwa sababu hizi fedha mwanzoni hazikuwa na chombo maalum ambacho kinaangalia ama kinadhibiti ni jinsi gani fedha hizi zitakuwa salama, kwa kweli wananchi hawakuwa na uhakika na usalama wa fedha zao.

Kwa hiyo, Taasisi hizi ambazo zinakusanya fedha kutoka kwa wananchi ama kwa wanachama wao, sasa kwa sababu zitadhibitiwa na Benki Kuu katika sheria hii mpya, nina hakika suala hili pia litahamasisha uanzishwaji wa *SACCOS*. Suala ambalo linaonekana ni ukombozi wa uchumi kwa wananchi ama kwa Watanzania wa hali ya kawaida ama watu wa Vijijini. Vilevile, nadhani itakuwa pia ni ukombozi hasa kwa wanawake kwa sababu wanawake wengi hawana ujuzi au upeo mkubwa wa kuelewa Taasisi hizi zinafanyaje kazi. Sasa kutokana na sheria hii kudhibiti ukopeshwaji wa fedha hizi, nadhani italeta imani zaidi kwa Taasisi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na udhibiti huo, mimi nina mawazo ya kuongezea hasa kwa Taasisi ambazo zinaweka fedha hizo. Kwa sababu *SACCOS* zinaweka fedha katika Benki, *Formal Lending Institutions* kama *CRDB, NMB, NBC* na kadhalika. Sasa mimi nilikuwa nafikiria kwamba sambamba na kudhibiti *savings* za wananchi katika Taasisi hizo, vilevile Benki hizi zinazoweka fedha za wananchi zingedhibitiwa ili kuweka *Bank Interest* ambayo inaridhisha. Kwa sababu *Bank Interest* ya sasa hivi inayowekwa na Benki hizi ni ndogo sana kulingana na fedha ambazo wananchi wanaziweka. Utakuta kwa mwaka wanaweka *Bank Interest* ndogo, lakini wenyewe wamekwishazitumia hizo fedha na kuzizalisha kwa manufaa yao. Kwa hiyo, nadhani itakuwa vizuri *BoT* pia ikaangalia katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, sambamba na *regulations* hizo za *BoT* katika *savings* za wananchi, pia nilikuwa nashauri kwamba ni vizuri Benki Kuu pia ikafikiria kuwapa mafunzo wananchi ambao wanaweka fedha zao, ama wanaanzisha *SACCOS* kule Vijijini. Kwa sababu ni watu wachache sana wenye upeo wa kuelewa na *SACCOS* zinavyoanzishwa zinakaa kwa muda fulani na baadaye utakuta wananchi ama wanachama watakapoendesha biashara zao wanashauriwa wa-*graduate* ili wakope kwenye *Formal Lending Institutions.*

Sasa kama upeo wa uelewa ni mdogo hususan kwa wanawake, mimi nadhani bado itakuwa vigumu hata kama biashara itakuwa imepanuka bado mtu ataogopa kwenda kukopa fedha Benki kwa sababu ya upeo wa uelewa. Kwa hiyo, nilikuwa naona hilo nalo liweze kuangaliwa sambamba na udhibiti, basi Benki kuu iweze kutoa mafunzo kwa wananchi wa Vijijini waweze kupata angalau mwanga katika kuendesha haya masuala ya kuweka fedha katika Benki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Taasisi nyingine za fedha zinapewa fedha na wafadhili. Sasa Taasisi hizo zina-*charge interest rate* kubwa sana, si kwa sababu Taasisi zenyewe zinapenda, lakini kuna masuala ambayo yanazilazimisha kwamba zinabidi zi-*charge interest rate* kubwa. Kwa mfano, mfadhili anapokupa fedha za kukopesha kama *Revolving Loan Fund,* anakupa akikwambia kwamba ifikapo miaka kadhaa nadhani utakuwa umejitegemea na kuacha kutegemea wafadhili.

Kwa hiyo, Taasisi husika inapaswa ku-*charge interest rate* ambayo itajifanya endelevu. Sasa Taasisi yenyewe wakati inaomba hizo fedha inaeleza kwamba sisi tutakopesha watu maskini wa maskini na maskini wa maskini unapo-*charge interest rate* kubwa kwa mfano asilimia 30 bado haujatimiza ile *objective* ya kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyoelewa mimi, wafadhili wanavyotoa fedha pia wanazingatia sheria inayowekwa na nchi. Kwa sababu Muswada huu umekuja wakati muafaka, mimi pia ningetoa wito kwamba Taasisi zinazotoa mikopo kwa wananchi hususan wanawake ziweze nazo kudhibitiwa zika-*charge interest rate* ndogo angalau asilimia 10 au 15 kuliko asilimia 30 na kuendelea ya sasa hivi. Kwa sababu kwa kweli kama nia ni kuondoa umaskini bado tutakuwa tunakandamiza wananchi japo wafadhili watakuwa wanatoa fedha nyingi, lakini basi watakaofaidi sio walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyingine ambayo mimi nilitaka kuchangia ni suala nzima la *inflation rate* inayosababisha kushuka kwa thamani ya fedha zetu. Hii imechangiwa na wenzangu kwa kweli lakini pamoja na maelezo ambayo yamekwishaelezwa, nami ningependa kuongezea kipengele kidogo kwamba pengine pia ni busara kuwavutia ama kuwaruhusu wawekezaji wa ndani ya nchi zaidi kuliko kuwaruhusu wawekezaji kutoka nje. Kwa sababu kama tutakuwa na wawekezaji wengi kutoka nchini mwetu, basi fedha zetu zitakuwa zinazunguka, hazitakuwa zinalinganishwa na *forex* yoyote kiasi cha kushusha thamani ya fedha zetu. Hii nina imani kwamba ingeweza kupunguza *inflation rate.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mengine ambayo kwa kweli nilitaka kuzungumzia yamekwishazungumziwa, sina haja ya kuyarudia. Namalizia kwa kurudia kusema kwamba naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote naungana na wenzangu kuwapongeza wote waliohusika katika kuandaa Muswada huu na wale wote waliohusika kutuandalia Semina na hadi kutufikisha hapa tulipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutamka wazi kwamba naungana na wenzangu katika kuunga mkono hoja hii mia kwa mia. Pamoja na kuiunga mkono hoja hii, nina machache ambayo ningependa kuyazungumza ili kuboresha endapo itawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hili jambo la uteuzi wa Gavana na hao Manaibu Gavana watatu. Nilikuwa napendekeza ikiwezekana basi katika hao Manaibu Gavana wakiwa watatu, basi wawili kati ya hao wawe wanawake kwa sababu huenda moja kwa moja Gavana atakuwa mwanamume, basi pamoja na yule mmoja watakuwa wawili kwa wawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haikuelezwa pale wazi jinsi gani watapatikana hao Manaibu Gavana. Nilikuwa napendekeza kwamba hao waingie katika nafasi zao kwa usaili. Sasa hivi katika utendaji ambao unafanyika ulimwenguni kote nafasi nyeti kama hizo ambazo ni *professional* pamoja na kwamba ni uteuzi, lakini hao watu wanapewa usaili ambapo wanashindanishwa ili kuwapata watu ambao kwa kweli wataweza kumudu nafasi hizo nyeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, inapotokea hivyo, basi inapanua hata ile nafasi ya kuwafanya watu ambao wanajiamini kufanya kazi hizo watume *applications* zao na zishughulikiwe ili waweze kufikia kupata hizo nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna nafasi ya Katibu wa Bodi huenda ikawa ni katika wale Watendaji wa kutoka Benki Kuu. Sasa hivi inakuwa kwamba watu wanaofanya hiyo kazi ya Ukatibu wa Bodi na inapokuwa kama ni *professional,* basi wapitie katika chombo ambacho kinaitwa *Secretarial Bureau* katika kujua kwamba wanakidhi matakwa ya ulimwenguni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uteuzi wa wale wajumbe wanne ambao watateuliwa na Waziri pia nilikuwa napendekeza wapitie kwenye usaili hiyo itaondoa dhana yote potofu ya kusema kwamba amepewa fulani kwa vile anafahamika au ni vipi. Hapa lazima watu tuwe *professional* kabisa na pia tuwe wa wazi katika kujaza hizo nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nilikuwa nataka nigusie kazi za Benki Kuu pale anapozungumza kwamba mojawapo ni kutoa leseni katika Benki zinazoanzishwa. Hivi karibuni imetokea mfumko wa kila eneo au kila watu kuja na kuanzisha mabenki yao Tanzania, mwisho sasa hata wale ambao hawana shughuli zao Tanzania wanakuja kuanzisha Benki na pale inapoonekana kwamba Benki hizo hazi-*perform,* basi zinafungwa au wanashindwa kuendelea wanaondoka. Hili ni jambo la hatari sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana kwamba hapa Tanzania tukivumilia jambo hilo, basi tutakuwa sisi ndiyo jalala la watu ambao wanataka kujaribu kuendesha shughuli za Benki na wakishandwa huko kwingine ambako wanafuatiliwa wanakuja hapa wakijua kwamba nikishakuwa na mtaji wa milioni 500 au kutokana na kiwango kinachotakiwa na *BoT* nitapata leseni ya kuanzisha Benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ni hatari na ningeomba lifahamike hivyo na lichunguzwe kwa undani. Zaidi ya hapo utakuta kwamba hata sisi wenyewe kutokana na urasimu wa kupata mikopo katika Mabenki ya Biashara watu wanajikusanya wanaweza kukusanya fedha inayotosha katika ile awali ya kuanzisha Benki, basi wanaanzisha Benki ili wapate urahisi wa kupata mikopo kwenye Taasisi yao ya Benki.

Hii ni dhana potofu kwa sababu ukiwa na Benki yako wewe mwenyewe huwezi tena kujikopesha kiholela itabidi ufuate taratibu zinazotakiwa katika kujikopesha. Hii inakuwa ni hatari kwa sababu watu wanadhani labda wote wanaotaka kuanzisha Benki wanaanzisha hizi Benki ili wafanye biashara. Sio kweli! Ili uwe umeanzisha Benki na upate faida itakuchukua zaidi ya miaka mitano. Lakini watu wamekazana tu kuchanga kuanzisha Benki zao.

Kuna Benki za Mikoa, Benki za Taasisi, kuna Benki za Wananchi na kadhalika, zimeanza nyingi tu. Lakini inaelekea *BoT* inatoa leseni kwa sababu hawa wote wanakimbia yale masharti ya kuanzisha Benki. Je, kuendelea kwa Benki hizo itakuwaje? Matokeo yake unakuta Benki ndogo ndogo hizi zilizoanzishwa zinaanza biashara nyingine ndani ya Benki na wanasahau zile *core business* za ile Benki. Unakuta sasa wameanza kufundisha watu kompyuta, kuleta vitu vya misaada kutoka nje kuwauzia watu. Sasa hiyo ndiyo kazi iliyowafanya waanzishe Benki? Nilikuwa naomba hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nilikuwa naomba liangaliwe ni kuhusu elimu kwa wananchi. Watu wanaifahamu *BoT* lakini sidhani kama *BoT* nayo inaelewa jinsi gani wananchi wana kiu ya kufahamu shughuli inazofanya. Utakuta watu wanazungumzia *interest rate* ya *Treasury Bonds and Bills* iko juu, ningefurahi kama ningewekeza kwenye *Treasury Bills.* Sasa jinsi gani afike kuwekeza kule, wala hawajui vizuri wanaendaje, inawabidi wapitie kwenye *Commercial Banks. Commercial Banks* nazo zina biashara zao zinazofanya kiasi ambacho wakisema ni kufanya tu hilo hawafiki.

Kwa hiyo, ningewaomba Benki Kuu watoe elimu ambayo wananchi wataelewa wazi hivi huko *BoT* tunaposema tunakwenda kuwekeza wakati mwingine kiwango

kinafika mpaka Sh.5,000,000/=, watu wengi tu wanamudu kuwa na Sh.5,000,000/= na wangeweza kuwekeza kwenye *Treasury Bills,* inakuwaje? Kwa hiyo, ningeomba sana Benki Kuu iangalie elimu kwa raia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye *currency*, kuna jambo ambalo linasumbua. Utakuta tunahakikishiwa kwamba noti zinachapishwa na noti hizo zitakuwa ni za aina yake ambazo watu hawataweza kughushi au hazitatokea kuwa bandia. Kweli kuna *currency* za nchi nyingine ambazo mpaka kusikia leo hatujasikia kwamba kuna *pounds* ambazo ni bandia nyingi, hata *Euro* zilivyoanza hatujasikia. Mimi ningeomba *BoT* wanapokwenda kuchapisha watumie gharama kubwa, lakini tuweze kuwa na *currency* yetu ambayo ni imara haiwezi kugushiwa kirahisi. Hii itasaidia sana wananchi kuamini kwamba Benki Kuu inatengeneza vitu vinavyofaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nilikuwa tu nawaomba wenzangu kwamba hiki kipindi ulichotupatia cha kujadili Muswada huu kimefanya wengi tukaelimika kiasi ambacho sasa hata tukiuzungumzia huu Muswada tunajua tunalozungumza. Tumetoa madukuduku yaliyo moyoni kwa ruhusa ya Bunge lako Tukufu, tumeweza kuzungumza kwa mapana, wametusikiliza Watendaji wa Benki Kuu na sisi wenyewe pia tumewasikiliza wenzetu wenye kuelewa vitu katika nyanja tofauti.

Kwa vile tumepewa fursa hiyo na tukaitumia inavyopasa na huenda bado tunaendelea, mabadiliko yamefikia wakati ambapo hatuwezi kuyazuia na yanakuja kwa nia nzuri tu. Mpaka kufikia leo walipokuja kutaka mabadiliko wamekuwa wakifanya kazi nzuri japo naona hata haya mabadiliko ya kufanya hii *act* iwe imebadilika imechukua muda. Kwa sababu ingetakiwa labda iwe tumeshaifanya siku nyingi ili twende tukirekebisha vifungu. Kwa vile sasa imekuja wakati muafaka na wengi wameunga mkono, nami naungana nao nikiomba sasa tuukubali huu Muswada upite.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii nami nitoe mchango wangu katika Muswada huu. Lakini pia naomba nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa maelezo yake ya utangulizi aliyoyatoa wakati anawasilisha Muswada huu. Ni Muswada ambao kweli una nia ya kukidhi matakwa ya sasa katika sera za kifedha za nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nitumie nafasi hii kuwapongeza sana Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa jinsi ambavyo wameshiriki na kwa maelezo yao ambayo wametutolea hapa ya awali. Vile vile, naipongeza sana Serikali kwa kuitikia wito ama kufikiria yale mapendekezo ambayo Waheshimiwa Wabunge waliyatoa hapa wakati tunajadili kwenye Semina.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niungane na wenzangu na kusema kwamba naunga mkono Muswada huu kwa asilimia zote mia moja. Pamoja na kuunga mkono Muswada huu, nina maeneo kadhaa ambayo nilikuwa nadhani kwamba ni vyema nikaungana na wenzangu kuyaongelea au kutia msisitizo katika yale

ambayo tunadhani ni vyema yakaingizwa ama yakafanywa kama sehemu ya marekebisho kwenye Muswada huu ambao baadaye utakuwa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kwanza, ama eneo la kwanza ambalo nilikuwa napenda kuongelea ni kile kifungu cha 11 kifungu kidogo cha (5) kinachohusu uendeshaji wa Mikutano ya Bodi ya Benki. Wenzangu wameliongelea hili jambo jinsi ambavyo ukitazama kwa undani linapunguza fursa ya kufikia uamuzi ambao unaweza kuwa na maslahi kwa Benki.

Juzi tulipokuwa tunaongea kwenye Semina wachangiaji wengi walionyesha wasiwasi wa *quorum* ya Mkutano wa Bodi ya Benki. Ikafikia mahali Serikali ikaliona hilo ikafanya marekebisho ambayo tumeletewa juzi ambayo yanasema kwamba sasa *quorum* imetoka kwenye Wajumbe watano kufikia Wajumbe sita. Lakini wasiwasi wa awali wa Waheshimiwa Wabunge ulitokana na ile *wording* ya kwanza ambayo ilikuwa inaongelea *quorum* ya watu watano kati yao wanne ni Watendaji ama wafanyakazi wa Benki Kuu akiwemo Gavana kama Mwenyekiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele hiki kilivyo sasa hivi kinasema: "Endapo kutakuwa na jambo lenye dharura kubwa na uamuzi wake unahitaji kufikiwa bila ya kuwepo kwa *quorum* inayosemwa katika Muswada huu, basi Mwenyekiti pamoja na Manaibu Gavana wanaweza kufanya uamuzi ambao utakuwa halali na hauwezi kutenguliwa hata kama *quorum* itatimia." Kipengele hiki kinaleta utata.

Kwa hiyo, sababu ya kwanza ya kutoa mchango wangu huu ni kwamba yale mapendekezo ambayo tuliyapendekeza kuwe na uwanja mpana zaidi kuwahusisha Wajumbe wengi wakati tunaongelea maamuzi ya Bodi. Hiyo ni sababu ya kwanza. Sababu ya pili nadhani wakati kipengele hiki kinatayarishwa hakikuzingatia sana maendeleo ya Sayansi na Teknolojia ambayo dunia ya sasa imefikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ngumu kidogo kuelewa tunaposema itafikia wakati ambapo Wajumbe wanaweza wasipatikane, pengine tunakwenda kwenye *extreme* sana. Maendeleo ya sasa hivi yanaonesha na yanawezesha kufanya mikutano kwa kutumia hata mitandao ya simu na hata kama watu wako sehemu mbalimbali. Mikutano ya sasa haifanywi tu kama mmekaa pamoja kama tulivyo hapa. Tunafahamu mikutano imekuwa ikifanywa kupitia *tele-conference* lakini pia kuna *TV/ video conference.*

Hayo mambo tunaamini Benki Kuu kama Taasisi kubwa kabisa masuala ya teknolojia sio tatizo kubwa na nashindwa kupata mazingira ambayo yanaweza kusababisha kwa mfano Wajumbe watakaokuwa wameteuliwa katika nafasi hizi za Bodi za Benki Kuu wakawa mahali ambapo hawawezi kufikika kwa simu. Lakini pia kama wako ndani ya nchi lakini wako sehemu ambazo hazina mitandao, najaribu kufikiria ni mazingira gani ambayo yatafanya uamuzi ndani ya masaa kadhaa kabla mtu hajapatikana ndani ya nchi hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nadhani kwa hizo sababu mbili, la kwanza hilo la kwamba juzi tulionyesha wasiwasi na ndio maana Serikali ikakubali kuweka

marekebisho ya ile *quorum* iwe zaidi ya Wajumbe watano kwenda sita, basi pia ikihusishwa na hii fursa ya kuwepo kwa maendeleo ya Sayansi na Teknolojia ambayo inawezesha uendeshwaji wa Mikutano bila ya kutegemea watu kukusanyika kwa pamoja, basi ziwe sababu za msingi za kuhakikisha kwamba kipengele hiki kinarekebishwa ili kutoruhusu nafasi ya watu wanne kutoa maamuzi ambayo kimsingi yanahusu uchumi wa nchi yetu.

Kwa hiyo, hoja yangu ilikuwa ni hiyo. Katika suala la uendeshaji, nadhani ni jambo la msingi kwamba tufanye marekebisho watu wanne wasipewe nafasi ya kuweza kuamua kuhusu maamuzi ambayo yana *impact* kwenye nchi kwa sababu uwezekano wa kufanya mkutano au kufikia maamuzi kwa njia ya *consensus* kama ilivyo bila hata kukusanyika kwa pamoja ipo. Kwa hiyo, hilo lilikuwa ni jambo la kwanza ambalo nilitaka kuongelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nilitaka niongelee lile ambalo wenzangu wameliongelea sana. Nadhani ni kipindi muafaka kwamba Benki Kuu kama ilivyo kwa mamlaka yake na asili ya kazi zake, kweli iweke msukumo wa aina yake kuhakikisha kwamba Benki ama Taasisi za Kifedha zilizopo hapa nchini zishiriki kwa msukumo mpya kutoa mikopo kwenye Sekta ya Kilimo. Nadhani ni suala la msingi sana.

Tunajua wenzangu walishasema hili, sitalisemea kwa maneno mengi kwa sababu asilimia 80 ya sisi Watanzania tunakaa Vijijini na kule shughuli kubwa ya kiuchumi ni kilimo pamoja na shughuli nyingine, lakini shughuli za kilimo zinachukua nafasi kubwa. Kwa hiyo, nadhani ni suala la msingi kweli kwamba msukumo mkubwa uwekwe kuhakikisha kwamba wananchi ambao tunajishughulisha na shughuli za kilimo tunafaidika na hizi sera za kupata mikopo kutoka kwenye Taasisi za Kifedha kama Benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka kuongelea ni suala la Katibu wa hii Taasisi. Wenzangu wameongelea na jana liliongelewa pia na Waheshimiwa Wabunge wengine. Kwa jinsi ilivyo Taasisi hii inawezekana ikaonekana kama ni jambo dogo. Kwa hakika sio jambo dogo sana. Utata wa kutokuwepo kipengele kinachoongelea Katibu unaweza kujitokeza wakati yakitoa mapungufu katika utekelezaji wa mambo ambayo Benki inayafanya.

Kwa hiyo, nadhani ni jambo la msingi kuwepo kwa kipengele ambacho kinamtaja Katibu ama *Secretary* wa Bodi na majukumu yake pia yakaanishwa ndani ya Sheria ama Muswada huu. Kwa sababu tusipofanya hivyo, wakati fulani kunaweza kukatokea mkanganyiko. Kuna jambo moja la kutunza kumbukumbu, nani atakuwa anawajibika kutunza kumbukumbu? Sina hakika, inawezekana Mheshimiwa Waziri baadaye atatufafanulia, labda kwa mazoea ama *conventional practices* ni ipi kuhusu masuala ya Makatibu wa Benki Kuu?

Lakini nilikuwa nadhani nikiangalia mfumo wa kawaida wa *Corporate entity* kuwepo kwa Katibu ni jambo la msingi kwa minajili ya kutunza kumbukumbu, lakini pia ndiyo anayetayarisha *minutes* zote ambazo zinahusu kikao kinachohusika. Nadhani

kwamba hili nalo ni la msingi sana kuliingiza katika Sheria yetu ambayo tunatarajia kuitunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo niongelee jambo la mwisho. Kuna hiki kipengele ama kifungu cha 32, kifungu kidogo cha 2(f) kinaongelea baadhi ya kazi nyingine ambazo Benki Kuu inaweza kuzifanya. Katika hili, limeongelewa suala pia la kuweza kujishughulisha na ununuzi wa dhahabu. Waheshimiwa Wabunge wenzangu wameongelea jambo hili jana wakaelezea wasiwasi wao na mimi naungana nao kuwa na wasiwasi. Nasema kwa hali ilivyo sasa nadhani ni vyema kwanza tuka-*concentrate* kwenye hii dhahabu ambayo tunayo hapa nchini badala ya kujihusisha na ununuzi.

Endapo tafsiri sahihi ya kifungu hiki ni hivyo kwamba Benki wakati fulani inaweza kulazimika kununua dhahabu kutoka nje ya nchi, mchango wangu ni huo. Naungana na wenzangu kwamba kwa kipindi hiki si kipindi muafaka, tunaona kuna madini mengi nchi hii na wataalam na Makampuni mbalimbali yanakuja nchini kwa sababu bado kuna hazina ya madini haya, kwa hivyo nikadhani ni vyema tukayazingatia haya yaliyokuwepo hapa ndani badala ya kuanza kushughulikia hayo ya nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, naungana na wenzangu kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. RICHARD S. NYAULAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuweza kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika Muswada huu. Awali ya yote ningetaka kuwapongeza Waziri wa Fedha kwa mchango wake wa kutueleza vizuri kuhusu Muswada huu. Pongezi vile vile ziende kwa Gavana kwa maelezo mazuri ambayo alikuwa ameyatoa juzi wakati wa Semina. Lakini vile vile niwape pongezi viongozi mbalimbali wa Serikali kwa kuweza kuleta Muswada huu ili tuweze kuujadili. Kwa hakika Muswada huu umeletwa kwa muda muafaka. Wote tunaelewa kwamba kuna mabadiliko makubwa sana ambayo yametokea duniani katika mambo ya Benki na mambo ya kifedha kwa jumla.

Lakini vile vile, kumetokea mabadiliko makubwa sana katika nchi yetu. Katika kipindi cha miaka 10 iliyopita uchumi umekuwa kwa kiasi kikubwa sana, teknolojia imebadilika kwa kiasi kikubwa sana na vile vile wadau ambao wanahusika katika masuala ya fedha wameongezeka kwa kiasi kikubwa sana. Mabadiliko yote haya yanahitaji mabadiliko katika sheria iliyokuwepo miaka 10 iliyopita.

Kwa hiyo, ningetaka awali ya yote kupongeza sana Benki Kuu kwa kazi nzuri ambayo wameweza kuifanya katika kipindi hiki cha miaka 10 kiasi ambacho uchumi wetu umeweza kukua kwa kiasi kikubwa sana. *Inflation* imeshuka na *exchange rates* vile vile katika kipindi cha miaka 10 kimeweza kushuka kwa kiasi kikubwa sana, yote haya ni mafanikio. Natumaini nia ya Muswada huu ni kutaka kutoa nafasi kubwa zaidi ya mchango wa Benki Kuu kuweza kuchangia katika kukuza uchumi zaidi. Kwa hiyo, kwa yote hayo yaliyotokea na madhumuni ya Muswada huu ningetaka kuchukua nafasi hii kuunga mkono hoja iliyo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba Muswada ni mzuri nafikiri na mimi ningeweza kuchangia katika maeneo ambayo nafikiria yanaweza kuboreshwa ili kufanya Muswada uwe mzuri zaidi. Lakini kwanza nilitaka kubainisha madhumuni ya kutunga sheria. Sheria hii inatungwa ili kuiwezesha Benki Kuu kutekeleza majukumu yake vizuri zaidi ambayo yanaweza kuwa na manufaa kwa nchi nzima na kwa jamii kwa ujumla. Lakini vile vile madhumuni ya kuwa na Muswada huu na kuweza kupitia humu ndani ni kuweza kuzuia mianya inayoweza kujitokeza ambayo inaweza kutumiwa na watu ambao hawana nia nzuri. Kwa maana hiyo ni kwamba tunapotunga Muswada huu tusiangalie sana viongozi waliopo sasa kwa sababu inawezekana kwamba viongozi hawa tunawaelewa vizuri, wana nia nzuri na tabia nzuri lakini kwa hakika tunapotunga Muswada huu tunajaribu kuchukua kwa ujumla wake.

Mara nyingi Miswada inapotungwa unajaribu kuchukua hulka ya binadamu inakuwaje. Kwa kawaida wakati mwingine tunaweza kuwa na Miswada mizuri lakini tunaweza kuwa na watu wabaya wanaweza kuitumia vibaya. Kwa hiyo, ningependa kuainisha kwamba Muswada huu tuangalie sio tu namna ya kuweza kuwawezesha wenzetu kuweza kutekeleza mambo mbalimbali yanayoweza kuleta manufaa kwa jamii lakini vile vile kuzuia mianya ambayo inaweza kutumika vibaya na watu ambao hawana nia nzuri. Muundo wa sasa wa Benki Kuu ulikuwa unaonyesha kwamba kwa kiasi fulani walikuwa wanashirikiana kwa kiasi kikubwa sana na Wizara ya Fedha.

Kwa misingi hiyo, tunaweza tukasema ilikuwa inasimamiwa na Wizara ya Fedha na katika muundo wa sasa, Gavana ndiye Mwenyekiti wa Bodi. Lakini bado tuelewe kwamba juu yake kulikuwa na Wizara ya Fedha. Mabadiliko ambayo yanapendekezwa ni kuongeza uhuru wa Benki hilo natumaini sina matatizo nalo na linastahili kufanyika hivyo ili kuwapa nafasi ya kuweza kutekeleza majukumu yao vizuri zaidi. Lakini vile vile madhumuni ya pili na mabadiliko yaliyoongelewa hapa ni kuwajibika kwa Watendaji wa Benki Kuu. Natumaini hilo vile vile halina matatizo makubwa sana. Yote nayaunga mkono.

Suala ambalo linaweza kujitokeza sasa hivi ni suala la kuwajibika. Kwa sababu unapowajibika lazima uwajibike kwa mtu fulani. Katika Muswada huu haijaelezwa bayana Benki Kuu itakuwa inawajibika kwa nani. Lakini nikiri kwamba imeelezwa vile vile kwamba taarifa mbalimbali zinazokuwa zinatolewa kuja Bungeni kwa kupitia kwa Waziri, hizo ni taarifa lakini sio mambo ambayo yanahusika na utendaji wa mara kwa mara. Lakini vile vile tunaelewa kabisa kwamba, ukaguzi utakuwa unafanyika na taarifa ya ukaguzi itakuwa inaletwa Bungeni. Natumaini yote hayo ni mazuri na yote yanaungwa mkono na nawapongeza sana viongozi kwa kuyaona hayo na kuyaona kwamba ni lazima yawepo.

Lakini linapokuja kwenye suala la Mwenyekiti, hapo kidogo nilikuwa napata matatizo na kigugumizi kidogo. Kwa sababu najaribu kujiuliza, hivi kuna faida au hasara gani ya kuwa na Mwenyekiti ambaye ni tofauti na Gavana? Kama kuna hasara zingeweza kubainishwa vizuri, lakini kama kuna faida, basi nazo zingeweza kubainishwa vizuri. Lakini ninachokielewa ni kwamba kama kutakuwa na tofauti ya Mwenyekiti na

Gavana faida mojawapo ambayo tunaweza kuipata ni kuwa na Utawala Bora. Tumezungumzia kuhusu *Good Governance* na *good governance* ni pale ambapo unaweza kutoa madaraka kwa watu wawili tofauti. Hiyo ndiyo faida ninayoiona.

Lakini vile vile kwa kuwepo Mwenyekiti ambaye ni tofauti na Gavana haipunguzi hata kidogo uhuru wa Benki Kuu. Uhuru unakuwepo pale pale, kwa sababu hata huyo Mwenyekiti naye atakuwa ni sehemu ya Benki Kuu. Tofauti ni kwamba, tuna watu wawili ambao wanajaribu kuhakikisha kwamba Utawala Bora unakuwepo baina yao. Kwa hiyo, bado nilikuwa nafikiria kwamba ingekuwa ni vizuri kwamba kungekuwa na Mwenyekiti tofauti na Gavana. Inawezekana kwamba katika sehemu nyingi zile ambazo zimetembelewa za mifano imeonyesha kabisa kwamba Mwenyekiti na Gavana ni mtu yule yule, lakini inawezekana kwamba mazingira yanaweza kutofautiana sana. Wasiwasi wangu ni kwamba, tunaweza kujiingiza katika mtego ambao wafanyabiashara wengi unawapata.

Katika nchi yetu, wafanyabiashara wengi wakiona mwenzao ameanzisha biashara ya aina fulani, basi wengine wote wanaona kwamba ile biashara ndiyo inayofaa. Kama kuna mtu ameanzisha biashara ya kuku, basi wengine wote wanaanzisha biashara ya kuku. Sasa hilo linaweza kuwa tatizo kubwa kidogo.

Kwa hiyo, nilikuwa nafikiria kwamba sio vizuri kwamba sisi tumekwenda kuiga kwa sababu Kenya imefanya, Nigeria imefanya kwa sababu mtu fulani amefanya. Tuseme tunafanya hivi kwa sababu tunafikiri kwamba mabadiliko ambayo yanahitajika katika nchi yetu yanahitajika kufanya hivyo. Kwa mazingira ya nchi yetu ni msingi mkubwa wa kuweza kufanya mabadiliko ambayo yanastahili kufanyika. Lakini isiwe tu kwa kuiga kwa sababu wenzetu wameweza kufanya hivyo. Kwa hiyo, naunga mkono kabisa kwamba *best practices* zinahitajika na *best practices* unaweza kuiga vitu fulani fulani ambavyo vipo lakini inawezekana kwamba tunapochukua hizi *best practices* lazima tuziunganishe na mazingira ambapo tunafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu ambalo nilitaka kulizungumzia ni kuhusu uanzishwaji wa Benki nyingine za maendeleo. Kwa hilo, naipongeza sana Benki Kuu kwa sababu ni suala ambalo litasaidia sana katika kusukuma maendeleo. Lakini cha msingi inawezekana kwamba sio kuanzishwa Mabenki hayo kwa hakika hata Mabenki yaliyopo ni mengi ya kutosha lakini vile vile yana fedha nyingi sana za kutosha. Tatizo ambalo lipo ni kwamba Wazalendo, Watanzania hawana uwezo wa kuweza kupata mikopo kutoka kwenye vyombo hivi vya fedha.

Kwa hiyo, naweza kuwa na wasiwasi kwamba hata hizi Benki nyingine zitakapoanzishwa bado kunaweza kuwa na masharti ambayo ni magumu na ambayo yanaweza kumfanya Mtanzania wa kawaida asiweze kupata mkopo kwa ajili ya maendeleo. Kwa hiyo, natumaini kazi kubwa hapa ni kusema Benki Kuu inajaribu kuweka masharti ambayo ni nafuu ambayo yanaweza kumwezesha Mtanzania wa kawaida anayetaka kufanya biashara aweze kupata mikopo kwa urahisi kutoka kwenye Mabenki haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, la nne ni suala la Benki kukopesha Mabenki mengine. Hilo natumaini linaeleweka na ni zuri linastahili kuwepo. Lakini vile vile nilichotaka kuongeza hapa ni kwamba kama inaweza kukopesha Mabenki mengine, basi ingekuwa ni vizuri kwamba ingeweza kukopesha Vyama vya Kuweka na Kukopa. Kwa nini ikopeshe Vyama vya Kuweka na Kukopa? Kwa sababu wananchi wengi ambao wanaishi Vijijini hawana uwezo wa kuzifikia hizo Benki. Lakini Benki zao ni hizi Vyama vya Kuweka na Kukopa au Benki Kata, hizo ambazo ni nyingi Vijijini na hizo ndizo walalahoi wanaweza kuzifikia kwa urahisi.

Kwa hiyo, kama Benki Kuu inaweza kukopesha fedha kwenye Mabenki mengine, basi ingekuwa ni vizuri ikajaribu kutumia Taasisi nyingine kama *TASAF, SELF, SCULT* au Taasisi nyingine yoyote ambayo inaweza kuanzishwa ili itumike kwa ajili ya kuweza kutoa mikopo kwenye *SACCOS* zetu mbalimbali. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tunajaribu kuimarisha *SACCOS* ambazo zinahudumia wananchi wengi Vijijini. Kama tukiweza kuimarisha *SACCOS* hizo kwa kuweza kutoa mikopo, nafasi ya kuweza kupata mikopo maana yake tutakuwa tunaimarisha shughuli mbalimbali ambazo zinafanyika Vijijini, kubwa zaidi likiwa ni suala la kilimo. Kwa hiyo, mikopo yetu inaweza kuwafikia wakulima kwa urahisi kwa kutumia *SACCOS* ambazo ziko Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo ningetaka kulizungumzia ni suala la Manaibu Gavana ambao watakuwa watatu. Naunga mkono hoja ambayo wenzangu wameshapendekeza kwamba kuwe na mwanamke lakini vile vile kuwe na Mzanzibar ili kuwe na nafasi ya kuwashirikisha watu mbalimbali katika uongozi wa juu katika vyombo vyetu.

Kwa maelezo hayo, la mwisho ambalo nilitaka kulielezea linahusu maamuzi ambayo yanayoweza kufanyika na Gavana kwa kushirikiana na Manaibu wake wanne. Hapa wasiwasi wangu ni kwamba, lazima tuweke tofauti kati ya maamuzi ambayo yanafanyika ya Kibodi na maamuzi ambayo yanafanyika ya Kimenejimenti au kiutendaji.

Kama ikitokea mahali ambapo Watendaji wanaweza kujigeuza wakawa ni Bodi, basi maamuzi ambayo yatakuwa yanafanyika hayatakuwa na tofauti yoyote. Tungeweka utaratibu ambapo maamuzi ya kiutendaji yanajulikana na yanakuwa ni tofauti na maamuzi ambayo yanafanyika na Bodi na hiyo, inawezekana pale ambapo Watendaji hawatakuwa na nafasi ya kuweza kujigeuza kuwa Bodi pale wanapoona kwamba kuna masuala ambayo wanafikiria kwamba ni ya haraka zaidi, lakini mambo ya haraka kama wenzangu walivyochangia ni kwamba kwa utaratibu wa sasa mtandao ni mkubwa sana. Siku hizi watu wanakaa Marekani, lakini baada ya siku moja wanaweza kusafiri wakafika Dar es Salaam. Sasa kama sisi tuko hapa hapa Tanzania hilo suala ambalo linakuwa la haraka zaidi kiasi ambacho huwezi kuwaita wenzako ambao wako hapa hapa Tanzania linanipa matatizo kidogo.

Kwa hiyo, ningeomba kunapokuwa na mambo ya dharura, basi Wakurugenzi wengine au *Directors* wengine ambao sio Watendaji wahusishwe katika maamuzi hayo ya haraka. Hilo ndilo lilikuwa suala langu la mwisho na mchango wangu wa mwisho katika Muswada huu.

Kwa kumalizia, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Waziri, Gavana pamoja na Serikali kwa kuleta Muswada huu na mimi naunga mkono Muswada huu moja kwa moja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwanza kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kutoa mchango wangu katika Muswada huu unaohusu Benki Kuu. Lakini awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa namna alivyoweza kuwakilisha Bungeni Muswada huu na kwa kweli naamini umeeleweka na sisi kama Waheshimiwa Wabunge tumeweza kupata nafasi ya kuchangia kwa mapana na marefu. Lakini vilevile, namshukuru Gavana wa Benki kwa jinsi naye alivyoweza kutoa mchango wake wakati wa uwasilishaji wa Muswada huu. Naishukuru zaidi Kamati kwa yale yote iliyoweza kuyapitia na ikaona kwamba iyafanyie marekebisho na kwa kweli namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kuweza kuyakubali yote haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, napenda niliseme hili kabla sijaanza kuchangia rasmi. Wakati najiandaa kutoka katika Jimbo langu la Musoma, niliwaaga wananchi wangu, wakati nawaaga nikawauliza mnadhani nipeleke ujumbe gani Bungeni? Walichoniambia, peleka salamu zetu kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwambie wananchi wa Musoma wanafurahia sana na wanatiwa moyo na juhudi zinazofanywa na Serikali yake pamoja na yeye mwenyewe. *(Makofi)*

Kwa hiyo, wao kama waajiri wangu nadhani nimeona ni vyema nikalifikisha hilo katika Bunge lako Tukufu. Naomba sasa nitoe mchango wangu kidogo katika yale yote ambayo Waheshimiwa wameyazungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili suala la Muswada limezungumzwa sana suala la Gavana wa Benki Kuu kuwa Mwenyekiti wa Bodi, lakini vilevile limezungumziwa suala la Gavana pamoja na Ma-*Deputy* wake kutoa maamuzi kwa niaba ya Bodi na kwa kweli Wajumbe wengi sana suala hili limewasumbua na imefika mahala kama ambavyo tumesikia imebidi Waheshimiwa Wabunge waende kwenye *internet* kuangalia hivi nchi nyingine zinafanyaje.

Kwa hiyo, ukiliangalia suala hili ni kwamba wamefikia kukubali kwa shingo upande kwa sababu wameona nchi nyingine ndivyo wanavyofanya. Lakini kama ni matakwa yao kwa kweli wangependa Mwenyekiti wa Bodi awe tofauti na Gavana, lakini pamoja na yale maamuzi yanayochukuliwa maamuzi ya Bodi, basi yasubiri Bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi mchango wangu ukilinganisha na hali halisi ya nchi yetu tunavyoifahamu si kweli kwamba Kiongozi wa leo alivyo mwaminifu ndivyo na wa kesho atakavyokuja. Mimi nadhani kwa maana ya hawa Watendaji, nadhani kama haina kizuizi, hebu tukubali kwamba Mwenyekiti wa Bodi awe tofauti na Gavana wa Benki, halafu haya maamuzi yanayotolewa, yale maamuzi yote ya Bodi ni vizuri basi yakaweza kusubiri Bodi kwa kuwa leo katika kukutana wala sio kazi ngumu katika hii nchi yetu ya Tanzania. Lakini vile vile, ni vizuri basi na hawa, maana mimi

nachojua tokea hapo awali walikuwa na uhuru, lakini wamesema wangependa wapate uhuru zaidi.

Lakini mimi labda vingenevyo, kama wangetupatia vikwazo wangetueleza vikwazo walivyokuwa wanavipata ambavyo vinasababisha mpaka kuona kwamba hata huo uhuru ulikuwa hautoshi na wakafikia mahala pa kuona kwamba basi wao hao hao kwa maana huyo huyo ambaye ni Gavana na huyo huyo anapaswa lazima awe Mwenyekiti. Kwa hiyo na hilo kama wanalo, basi nadhani wakati wa kuwasilisha na wao watatueleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ningependa na mimi nitoe mchango wangu sasa unaohusiana na kazi kubwa ya Benki Kuu ambayo wanapaswa kuifanya, pamoja na jinsi walivyosema katika *section five* majukumu waliyonayo, lakini nadhani kwa hali halisi ya Watanzania wa sasa Benki Kuu ingeweza kujikita zaidi sana kuona ni namna gani itakavyosaidia kuondoa umaskini kwa Watanzanai hasa wenye kipato cha chini. Kwa maana kwamba ni vizuri basi na yenyewe ingekuwa na mipango ya dharura lakini vilevile na mipango yake ya kawaida.

Ninasema hilo kwa sababu leo unapozungumza suala la *interest* za Benki ni kweli kwamba zimeshuka, maana mimi nakumbuka miaka ya tisini mwanzoni nilikopa kwa riba ya asilimia 39 ambayo hata ule mkopo kuurudisha kwa kweli nilijutia. Lakini ninachohitaji kusema ni kwamba mpaka leo hizi *interests* zilizopo bado haziwezi kumsaidia Mtanzania hasa mwenye uwezo wa chini. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni vizuri Benki Kuu ingeangalia namna ya kuweza kuendelea kushusha hizi *interest* ili ziwe watu wetu wanapokopa waweze kuwa na uwezo wa kulipa. Lakini kubwa zaidi hizi riba zinazotolewa na haya mabenki ni nafuu kidogo kwenye hiyo unayosikia asilimia 12 mpaka 15 kwa wale wakopaji wakubwa kwa maana wanakopa fedha nyingi. Lakini leo unapokwenda kwenye yule anayekopa fedha kidogo kwa maana ambaye ndio mlengwa wetu kwa maana ya mwananchi yule mwenye uwezo wa chini, hizi riba ziko juu sana Hata zile *institutions* ambazo saa hizi zinazokopesha kopesha *SACCOS* zetu wanasema wengine wanakopesha kwa riba ya asilimia 10 katika kipindi cha miezi mitatu, ambayo hiyo ukija kuipiga ni asilimia 40.

Kwa hiyo, kumbe tunaposema kwamba hizi Benki zinashusha riba kumbe ni kwamba riba hizi zinashushwa kwa wale ambao ni wakopaji wakubwa lakini kwa wale wadogo wala hawana unafuu wowote na ndio maana kila leo utasikia nyumba imepigwa mnada, utasikia vyombo vimekwenda na wengine hata vitanda vinachukuliwa.

Kwa hiyo, hili kwa kweli ni ushauri wangu kwamba Benki Kuu inahitaji ijikite huko sana kuona namna ya kuweza kumsaidia huyu mwananchi wa chini. Lakini vilevile, kuna suala la Benki kukopesha. Hili suala la Benki kukopesha kwa kweli nalo ni tatizo kubwa sana. Kwanza katika utafiti wangu nimegundua kwamba Benki hizi zingependa zaidi zaidi ziwe na watu wachache sana wa kukopesha, lakini wakope fedha nyingi na ndio maana leo unapomtuma au mtu wa kawaida anavyokwenda Benki kukopa pamoja na kukamilisha masharti yote, lakini atazungushwa na hatimaye atakata tamaa.

Juzi nakumbuka mwezi wa kwanza tulipoingia hapa hata Waheshimiwa Wabunge na ninyi mnaweza kuwa mashahidi katika hili. Aidha, kwa kuwa sisi ni Wabunge, mimi nakumbuka nilichukua siku mbili tayari nikawa nimepata mkopo. Nashukuru kwamba nyumba yangu ilikuwa imekwama, sasa inakaribia kwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hivi kwa nini huu msukumo basi sisi tunaweza kukopeshwa kwa muda mfupi, hivi ni kwa nini hata wale wananchi wa kawaida wasiweze kupata hizo bahati? Kwa hiyo, wakati mwingine ni kwamba vyombo hivi kwetu kwa kuwa vinajua sisi tunashika mpini, basi ni rahisi vinafanya mambo haraka haraka, lakini ni kwa nini haya yasifanyike kule kwa wananchi wetu ambao ni wananchi wa kawaida kabisa?

Vilevile, ningependa au ningeomba zaidi hii Benki Kuu ikaangalia namna ya kuendelea kuwasaidia kwa maana ya kuwakopesha kuanzia wale wafanyabiashara wadogo wadogo. Ninao mfano hai na mfano hai naomba kuutolea kwa kinamama. Kwanza naomba kusema kwamba kati ya watu ambao ni wepesi kukopesheka na wanalipa kwa kweli ni wakinamama, lakini wakinamama hawa ndio hao ambao ukiangalia wanakuja kukopa hii mikopo zenye riba ya asilimia 40 ukiijumlisha kwa mwaka. Hivi sasa katika utaratibu huo tunawasaidia?

Kwa hiyo, matokeo yake tunawafanya wanakuwa watumishi wa hizo Benki na yawezekana wakati mwingine Benki Kuu ikadhani kwamba kadri itakavyoruhusu Benki nyingi kuja, maana tunasikia sasa tunaona kwamba Benki nyingi zinakuja tunadhani kwamba kutokana na ile *competition* zile riba zitajishusha au zile Benki zenyewe zitalegeza masharti zitamkopesha mtu wa kawaida.

Mimi katika mtizamo wangu na hata wenzangu mnaweza kunisaidia katika hili, leo hizi Benki nyingi zinakuja kwa sababu wawekezaji wengi wa kutoka nje wanapenda kuja kuwekeza katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo basi, kwa kuwa wanapenda kuja kuwekeza katika nchi yetu na wameona kwamba ni mahala ambapo pana *opportunity* ya kuweza kuvuna haya masharti, bado hayatalegea kwa sababu wale watu wana watu ambao wanaweza kuwakopesha na wana watu ambao wanafanya biashara hapa na wanaweza kuwekeza katika Benki zile, na ndio maana leo ukiangalia hata tukija katika *tender* zote, ukizungumzia tu *tender* moja ya barabara zaidi ya asilimia 80 wote ni wale makandarasi wanaotoka nje. Kwa hiyo, ndio maana tunaona kama Benki zinaongezeka, lakini kumbe ni kwamba pamoja na kuongezeka kwetu sisi kama wananchi bado hazijatusaidia.

Kwa hiyo, ni vizuri Benki Kuu ingeangalia basi kwamba hivi ni chombo gani ambacho ingeendelea kukibana kiende mpaka kule kwa wakulima au kwa wale wananchi wa kawaida wakiwemo na wakulima na namna hata ya kusaidia wakulima, wala hakuna ugumu. Hakuna ugumu kwa sababu mkulima ili alime na avune yeye anahitaji zaidi zaidi apate maji. Akishapata maji na trekta, ana uhakika wa kuvuna. Lakini kumbe basi ni kwamba kama wakiwezeshwa ni rahisi kuangalia namna ya kuwachimbia malambo ili

waweze kufanya *irrigation*, lakini vilevile hata kutoa katika vyanzo vya maji vilivyopo ili waweze kulima.

Kwa hiyo, na huo ulikuwa ni mchango wangu kwamba hebu Benki Kuu ingejikita zaidi zaidi kwenye kuangalia basi kwamba ni kwa kiasi gani ingetoa mchango wake mkubwa kuhakikisha kwamba mwananchi wa kawaida ananufaika na hata anaielewa Benki Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana leo hii watu wengi ukizungumzia habari ya Benki Kuu wanajua kazi yake ni kutunza fedha. Kwa hiyo, baada ya kusema hayo na mimi napenda kuunga mkono, lakini ningetoa ushauri kwamba hebu yazingatiwe yale yote ambayo yanaweza kumsaidia mwananchi wa kawaida. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI HAMIS SUEDI KAGASHEKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika Muswada huu wa Benki Kuu wa mwaka 2006.

Kwanza kabisa naomba nitoe shukrani zangu kwa Waziri wa Fedha Mheshimiwa Zakia Meghji, kwa mchango wake alioutoa wakati akitueleza juu ya Muswada huu na pia ningependa nitoe shukrani zangu katika semina ambayo tuliipata na mawazo ambayo tuliyapata kutoka kwa wahusika mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningependa ku-*focus* katika suala la *best practices,* kwa sababu hili ni suala ambalo hata mtaalum kutoka Kenya aliyekuja hapa wakati wa semina aliweza kulitizama kwa undani zaidi. Lakini pia nataka nimnukuu nadhani alituambia kwamba tusirukie hili suala la kufanya mabadiliko katika Benki kwa sababu Kenya wamefanya au Chile au Mauritius wamefanya, lakini tufanye kwa kuzingatia kwamba ni kitu kina maslahi kwa nchi yetu na ni kitu ambacho tukifanye kwa kuzingatia mazingira ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika sasa tukitizama *the best practices* ambazo zimesemwa mimi kwa kweli matumaini yangu nilikuwa nategemea kabisa kwamba mbali na hizi nchi za Nigeria, Mauritius, Chile au Kenya ambazo wanazitaja, mimi nilifikiri wangeweza kutueleza, mfano Uingereza, kwa sababu nchi ya Uingereza wamebadilisha kabisa wameingia katika huu mfumo, *Bank of England* nafikiri hata Gavana yupo hapa anajua hii vizuri kabisa hawana hata miaka kumi. Nafikiri wamebadilisha kuipa *The Bank of England independence* ambayo wanaita *Independence* sasa hivi nafikiri ni mwaka wa saba au wa nane.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi naweza nikaichukulia hiyo ni kama *a best practice* na nafikiri tungeweza tukaitazama *function* hiyo na kuitizama Benki ya Uingereza ina- *function* vipi tangu mwezi Mei, 1997 wakati Goldon Brown, *Chancellor* wa *Exchequer* aliposema kwamba anaipa *Bank of England* uhuru na alivyofanya vile mwaka uliofuata 1998 ilipitishwa *The Benk of England Act* ambayo ilieleza kabisa Benki ya Uingereza itakwendaje na hiyo *Independence* iatakuwaje na *in fact* ukitizama *Act* yao unaona kabisa wameweza kuielezea hiyo *independence, independence from what.*

Sisi hapa tumekuwa tunakuwa tunazungumza tumekuwa tunajiuliza tunasema *Bank of Tanzania* wanataka wapate uhuru wanataka wapate *independence*.

Lakini mimi ninasema katika *best practices* tukiweza tukatizama hiyo *Act* ya Uingereza ambayo haina hata miaka kumi ni kitu ambacho mimi nadhani bado ni kipya kwa Uingereza

Mheshimiwa Naibu Spika, na hiyo *independence* naomba niseme kwamba wameipa Benki ya Uingereza baada ya miaka 300. *After its existence for the last 300 years.* Baada ya miaka 300, *for the first time* katika mwaka 1997 ndiyo Goldon Brown akasema kwamba wanaweza wakatoa uhuru katika *Bank of England* na Bunge la Uingereza mwaka 1998 *as recently as 1998* wakasema kwamba tunaweza tukawapa *independence* hiyo na *after 300 years*, maana sisi Tanzania tumekuwa *independent for the last 44 years,* hao wakubwa miaka 300 Benki yao imekuwa ina *operate* na imekuwa chini ya Wizara ya Fedha ya Uingereza na baada ya miaka 300 wakatoa hiyo *independence.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba hapa tunaelimishana na tunapeana taarifa. Walipotoa hiyo *independence* walikuwa *very specific* walisema kwamba itakuwa *operational independence* kwa maana ya kusema kwamba waliwapa ule uhuru lakini bado wakaweza ku-*define* ile *independence* gani walikuwa wanaipa *Bank of England* na kusema kwamba *operation independence* ambayo ita-*focus* kabisa katika *domestic interest rates.*

Kwa hiyo, sisi tunapotizama *Bill* yetu hii tuliyonayo, mimi nasema ni nzuri lakini bado *in room* ya kuwa *improved* kama tunaweza na tuna nia ya ku-*improve*. Lakini sasa tunapoambiwa kwamba *IMF, World Bank* wanasema kwamba hii ndiyo njia nzuri ama ndiyo njia bora, mimi nasema kwamba hawa watu wa *IMF* ikitizama wao *The IMF has been in existence for the last sixty years* na ukitizama miaka 20 au 25, mataifa yote yamekuwa yanajaribu kui-*reform the IMF* imeshindikana. Wameshindwa kui-*reforms* na *IMF* ina *operate* na Mheshimiwa Zakia Meghji yuko hapa na Gavana yuko hapa, *the IMF* ina *operate* siyo katika misingi ambayo iliwekewa wakati imewekwa pale sasa ina kwenda tu katika misingi tofuati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu *IMF* iliwekwa pale kutizama suala la *balance of payments* za nchi ambazo zilikuwepo *at the time* na kutizama *the gold standard* na kuweza ku-*monitor* na kuhakikisha kwamba *the exchange rate regimes* zinakuwa *actually match* na hali iliyokuwepo wakati ule. Wamarekani walipotoka katika *Gold Standard,The Gold Standard* ika- *collapse the exchange rate* wameachia soko huru, inakwenda kama inavyokwenda halafu *the so called World Bank* hawa walikuwa ni Benki ambayo imekuwepo *for the purpose the of the reconstruction of Europe* hiyo imekwisha *Europe* imeendelea wamejiwekea Benki yao nyingi sasa ya maendeleo.

Kwa hiyo, *focus* kubwa imekuwa ni kututizama sisi *how they can manage us, how can control us, how they can run away economies etc*. Sasa mimi nasema kwamba hiyo ni *fine,* maendeleo yawepo kwa sababu wimbi la mabadilko lipo kwa hilo twende na hilo

wimbi la mabadiliko lakini ningeomba hii *independence* ambayo tunaipa *The Central Bank of Tanzania, that is the Bank of Tanzania* wana haki kabisa ya kuwa na *operation independence.*

Lakini nadhani hiyo *operation independence* ingekuwa *very clear defined* katika *Bill* hii ambayo tumejiwekea. Sasa hiyo haipo na Waingereza ambao mimi nimewataja katika *Act* yao wakati walipokuwa wanatoa *operation independence* walitoa *limitation,* kwa sababu bado Serikali Goldon Brown, *The Chancellor of the Exchequer* amebakisha mkono wake katika ku-*control the Bank in the sence* kwamba amewaambia kwamba wanaweza waka-*operate* katika kutizama *the interest rate* jinsi zinavyokwenda lakini aliwapa *limit* na *limit* yenyewe alii-*set since 1997,* na ndiyo inayo-*operate* mpaka leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *limit* yenyewe ni kwamba *the interest rates* za Uingereza zitakuwa kila mwaka wanazi-*review* lakini zisiende zaidi ya *2.5 percent* inaweza ikawa *plus or minus but not more* na kama wao watakuwa wana-*operate* katika ku-*set the domestic interest rate* za Uingereza basi *the operation burn* itakuwa ni hiyo na kama kutakuwa na haja kwamba uchumi wa Waingereza umekuwa na matatizo zaidi itabidi warudi kwa Goldon Brown na kwa maana hiyo mimi nasema kwamba Benki yetu kama matatizo yangekuwepo inabidi warudi kwa Zakia Meghji ambaye ni Waziri wa Fedha.

Lakini ukitizama jinsi walivyoweka hii *Bill* kabisa ni kama *Government* haina *control* ni kama *in fact* utakuta Bodi wamejiwekea wao wata *operate* wenyewe. Lakini pia mimi nataka kusema katika *best practices* ukitizama nguvu yao waliyoweka katika ule mfumo wa *Bill* ya Uingereza ambayo ni *modern* mimi nasema katika *best practices,* kwa sababu *it doesn't even have ten years* tangu imewekwa, unakuta kwamba nguvu zao nyingi wameweka katika *monitory policy committee* na ni *monitory policy committee* ambayo wameipa nguvu ya kuweza kufanya kazi za kutizama masuala ya *interest rates, growth etc.* Lakini pia Waheshimiwa ndugu zangu Wabunge napenda kusema kwamba *the act* ya Waingereza ilikuwa *very clear* ingawa wamewapa uhuru huo lakini pia katika *act* wame-*set the interest rates* ambazo *the bend* ambayo wanaweza waka-*operate* lakini pia wakawaambia kwamba Benki haina njia nyingine ya ku-*support economic policy* ya Serikali *including its objective for growth and employment* hii imo ndani ya *act* yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ambayo mimi nasema sasa kwamba na sisi tunataka tuwape *independence the Bank* waweze ku-*operate independently* lakini ile *independence* yao iwe *clearly defined* na nguvu bado ya Wizara na nguvu ya Serikali lazima iwe pale pale siyo kwamba ni suala la kuingiliwa ama nini. Nchi yetu bado changa, Waingereza wamefikia pahala walipofikia kusema kwamba wametoa hiyo *operation independence for The Bank of England* baada ya ku-*exist for the last 300 years.* Sisi Benki yetu *hardly* miaka 44 tuko hapa sasa hivi tunazungumza kusema kwamba *the Government* iweke *hands down* iwaachie waamue wanavyotaka *the International Ministry of Finance which is the IMF* waje wa-*set* ma-*conditions* wanavyotaka, mimi nasema kwamba *this is totally unacceptable* lakini kama mnavyosema ndivyo *the wind of change* inavyokwenda ni sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitizama uchumi ingawa tunasema kwamba hii *independence* itaboresha uchumi na itaboresha kwamba Benki itaweza ku-*operate* vizuri lakini ukitazama masuala ambayo tumekuwa tuna matatizo nayo ambayo Waheshimiwa Wabunge wamezungumza kwa kirefu sana masuala ya *interest rates, of course* unakuta kwamba Benki haina *control,* masuala ya *prices* hakuna *prices stability* katika nchi hii. Utakuta kila mtu anajiwekea bei anazotaka na ukiuliza wanakwambia ni soko huria unakuta kwamba *the currency* yetu ina *depreciated* vibaya sana *versus the dollar.* Wakati *dollar* inapoteremka chini na shilingi inateremka chini wakati *dollar* inakwenda juu shilingi inateremka chini.

Sasa *we don't understand* kwa kweli ni kitu ambacho hakieleweki, *unemployment* (tatizo la uajiri) liko pale pale hakuna kinachofanyika, mfano mdogo nitakao kupa ndiyo maana nasema kwamba hata tukizungumzia kwamba tunaboresha uchumi na tukitoa *independence to the bank* itasaidia zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano mtu wa Bukoba kule ninakotoka mimi, unakuta kwamba leo mfuko wa *cement* Dar es Salaam leo unauzwa shilingi 8,000 sana sana *may be* 8,500 lakini unapofika Bukoba pale leo bei za sasa hivi unazungumzia shilingi 16,000 mfuko mmoja na ukitoka pale Bukoba mjini na ukaupeleka *let say* maeneo kama ya Ngara unazungumzia mfuko mmoja shilingi 25,000.

Sasa kweli mimi nimwambie mtu wa kule Bukoba uchumi unakwenda vizuri mambo yanakwenda vizuri kweli atanielewa? Ni vitu viwili tofauti kwa sababu yeye uchumi kwenda vizuri ni kuona kwamba mambo yanayomzunguka kama ni kujenga inakua ni rahisi, kama ni bei za vitu inakuwa ni rahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba haya mambo kwa kweli tuyatizame, mimi sina kipingamizi naona Waheshimiwa Wabunge wengi wanaunga mkono, ni sawa lakini haya ni mambo kwa kweli ya kutazama kwa umakini na kwa undani sana tusisukumwe kwa sababu eti *the international institution* wanataka hivyo ama eti *the international environment* inakwenda hivyo. Lakini mimi nafikiri kikubwa ni maslahi ya nchi yetu na maslahi ya Watanzania wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kuna suala hapa nilikuwa nalitizama si kubwa sana. Lakini ukilitizama kwa upande wa *accounting, auditing and reporting* na hii ni katika *section 20,* ukurasa wa 40 kutakuwa kuna suala la *Head* wa *Internal Auditing* katika Benki. Mimi hapa ninatizama *function* ya *internal auditing* ni nzuri na ni *important* kama ilivyo ya *external auditing.* Hapa ndugu zangu Wabunge mmelizungumza vizuri na mmelitetea vizuri lazima hatuwezi tukashughulika tu na kampuni kutoka nje kuja ku-*audit,* hapana lazima pawepo na mtu wa ndani. Lakini hapa ukitazama mtu wa ndani hapa katika *auditing* kwanza *auditing committee* ambayo imetajwa hapa hatuambiwi idadi yake watakuwa wangapi, *function* zake hazielezeki hapa katika Muswada huu na ingekuwa vizuri kwamba ielezeke na ieleweke.

Lakini pia kubwa zaidi mimi ninasema *report* ya *internal auditing* isiishie kwa Gavana peke yake. *Honestly* hii *report* inge-*find the way* ingekwenda mpaka kwa Waziri. *It is important.* Kwa sababu hii itamsaidia Waziri wa Fedha kuweza kutambua.

Mheshimiwa Naibu Spika naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. CASTOR M. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Mimi napenda kwanza nimshukuru Waziri na Gavana kwa kuwasilisha Muswada huu vizuri, lakini katika hoja nzima ya Muswada huu mimi sina pingamizi na napenda hapo hapo mwanzo kabisa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajikita zaidi kwenye utekelezaji, naomba ndugu zangu Wabunge mnisikilize kwa makini.

**NAIBU SPIKA:** Wanakusikiliza, wanakusikiliza kwa makini.

**MHE. CASTRO R. LUGALAMA:** Ndugu zangu Mheshimiwa Mporogomyi na Mheshimiwa Mwanri waliongelea sana juu ya *SACCOS* kwa uchungu mkubwa, hasa Mheshimiwa Mporogomyi kwamba Benki Kuu ihakikishe pesa zinafika *SACCOS* ili wananchi wetu wakope. Hicho ndicho tulichowaahidi wananchi.

Lakini nina wasiwasi, inawezekana tunaongea lugha mbili tofauti. Sisi tuna Ilani ya Uchaguzi; je, wenzetu wana Ilani? Inawezekana haya tunayoongea sisi tuna-*pack* kwa *time* ya miaka mitano na *we are already time bar.* Miaka minne na nusu tayari imebaki hatujatekeleza. Sasa, Benki ya *Standard Chartered* inaweza kuja kwa wakulima wangu wa miwa Kilombero au hata *SACCOS* ya Kidatu pale ikawakopesha? Benki ya *Standard Chartered* inaweza kwenda kwa wakulima wangu wa mpunga kule Mpanga, Mlimba ikawakopesha?

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ambayo inaweza kufanya kazi hii ni Benki tuliyoizoea ya *CRDB* na Benki hii iliishaanza mpango huu. Imeanzisha *program* ya *Microfinancing* kwa Mikoa minne ambayo ni Dodoma, Morogoro, Iringa na Mbeya kwa majaribio na ikawa *very successful.* Baada ya kufanikiwa, wao walikuwa wana-*deal* moja kwa moja wanakwenda kwa *SACCOS*. Wanazi-*organize* wanazipa *infrastructure*, wanazipa zile fomu za ushirika, fomu za kibenki na vitu vingine kama *Tembo Card, POS* wanawakopesha wale *SACCOS. SACCOS* inamkopesaha mkulima wa miwa kwa sababu inamfahamu. Matokeo ya kufanya zoezi hili la *program* ya ukopeshaji wa *CRDB* kwa miaka kama mitano umekuwa *successful. Recovery* ya mikopo hiyo ni *hundred percent. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kufanya kazi hiyo, tarehe 23/08/2004 *CRDB* ikapeleka maombi Benki Kuu kuomba leseni ya kuanzisha *subsidiary* ya *Microfinance* ili waweze kufanya kazi hiyo *officially*. Mpaka leo hii hawajapata leseni kwa sababu Benki Kuu inasema haiwezi kukubali *insurance regulations* zao kufanya *wholesale Microfinancing.* Lakini *concept* ya *Microfinancing* iko nchi nyingi. Benin ipo, India ipo

na *reserve Bank* ya India ambayo ni *Central Bank* ya kule inafanya hivyo, inaruhusu. Sasa wao wamesema hawawezi kufanya hivyo.

Kwa hiyo, yale maombi yapo Benki Kuu mpaka leo tangu Agosti, 2004 na sisi tumeahidi watu huko kwamba ingieni kwenye *SACCOS* pesa zitakuja kupitia *SACCOS*. Sasa unaona snag hii? Sisi ajira yetu inategemea miaka mitano, wenzetu *retirement*. Inawezekana Gavana hajui! Wote tumepiga kelele hapa, *SACCOS, SACCOS*, lakini sasa angalieni hii *snag*, tangu Agosti, 2004. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza yafuatayo: -

Kwanza, hiyo *regulation* inayozuia *wholesale micro financing* tuilete hapa tui-*discuss*, tuibadilishe, badala yake iandikwe" *"Any Commercial Bank* ambayo ita-*feel free* kufanya *any Microfinancing as a subsidiary* ifanye *provided* ihakikishe kwamba inaleta tija." Itashindwa ku-*substitute* hiyo?

Ya pili, *SACCOS* nyingi zinangojea *program* hiyo, *CRDB* wapewe leseni yao. Waitoe hiyo leseni ya kufanya *wholesale* hiyo, *Microfinancing* kwa sababu *is workable*. Mpaka pale kwenye Kata wanaweka kila kitu. Angalia Kibaigwa ni *mini bank,* jamani! Hata kule kwangu nina Kamakimu, ni *mini bank,* Mang'ula pale. Sasa vitu hivi vingeendelezwa yaani sisi Wabunge tungepata raha kwa sababu tungekuwa na mahali pa kuwaambia watu wetu nendeni pale *CRDB* italeta hela mtakopa. Utalima, utalipa na *interest rate* siyo kubwa. Halafu hata Benki katika kuwakopesha wale haidai *collateral*, wanasaini tu Mkataba wa ubia kati ya Benki na *SACCOS*, *that's all.* Hamna *collateral* kusema mtu atakupa hela hizi kwa *collateral* hii na kudai labda nyumba zenu. Kwa hiyo, ndugu zangu, la pili nilikuwa naomba hiyo *CRDB Bank* tuwape leseni yao.

Ya tatu, mimi nasema inawezekana Gavana hajui, ni Mkurugenzi anayehusika na utoaji wa leseni, kwa sababu ni miaka miwili. Tukifika *August this year 2006* ni miaka miwili, maombi ya leseni yako pale ya kuomba hawa watu wafanye *wholesale microfinancing*. Lakini nyinyi mnasema tu *regulation* yetu hairuhusu kufanya *wholesale*. India wanafanya, Benin wanafanya. Kwa hiyo, tunamwomba huyu Mkurugenzi anayehusika na leseni tumpe Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005 - 2010 aone, sisi tumeahidi nini kwa wananchi? Kwa sababu sisi tuna deni, atusaidie ili awaruhusu wale watu, ile Benki tuliyoizoea tuweze kuitumia kupata maendeleo katika nchi yetu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nadhani Wabunge mmemsikiliza Mheshimiwa Ligallama vizuri.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Muswada uliopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Gavana kwa kuileta hii hoja mbele yetu ambayo ni nyeti. Ndugu zangu Wabunge, suala hili ni zito na uamuzi tunaoupitisha inawezekana tunajichinja wenyewe au tunajiweka vizuri. Mimi kwangu naliona ni zito sana na hasa nikiangalia hili neno uhuru. Ninajaribu kuangalia historia; je, nyuma walikuwa hawana uhuru? Wanataka uhuru katika kitu gani? Uhuru usio na mipaka au wa namna gani? Je, kisheria *implication* yake ni nini? Kiuchumi *implication* yake ni nini? Je, hawa watu wasipoelewana *implication* yake ni nini? Je, wakitokea wajanja waka-*collude, implication* yake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa inanipa mawazo mengi sana, halafu najaribu kuangalia kifalsafa. Wenzetu wanasema *the truth of yesterday is not the truth of today.* Mwenzetu asubuhi amezungumza kwamba, tunaye Balali sasa hivi ni mzuri, anaweza akamwona Mheshimiwa Waziri akampokea vizuri akamwambia ajione kama Bosi. Lakini keshokutwa anaweza kupata mwingine ambaye Waziri akimwita anaweza kusema: "Wewe nenda, mimi nina *autonomy* yangu, nina shughuli zangu."

Suala hili linanipa maswali mengi sana. Sisi Wabunge tumekuwa tukiamua, lakini baadaye sheria inakuja inatugonga. Unajiuliza, hapa tulikosea wapi? Ni wazo zuri sana tukifikiri kwamba mambo yatakwenda hivyo na Tanzania itakwenda hivyo hivyo. Lakini binadamu anabadilika. Ulivyokuja hapa Bungeni sivyo ulivyo mpaka sasa hivi. Sasa hivi kujenga hoja kumeongezeka. Kwa hiyo, hawa viongozi wanaoingia na wenyewe wanakwenda wanabadilika, kama hubadiliki, basi una matatizo. *(Kicheko)*

Ndugu zangu, mimi nitaomba nielezwe wanataka uhuru up? Mpaka wapi? Iwe *defined*. Nilikuwa nafikiri hawa ni kama Rais, kama Mungu au namna gani! Hata Rais juzi tulimpa nafasi 10 za kuteua Wabunge, lakini tukampa *condition* kidogo kwamba watano wanawake, watano wanaume. Sasa hawa, ni wapi tunaingia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakuwa na wasiwasi kwa sababu mwaka jana niliuliza swali moja, sikujibiwa. Nilimwuliza Waziri wa Fedha nikiwa pale Bungeni Dar es Salaam kwamba, hicho kitu kinachopanda juu kinatumia gharama kiasi gani na kiliidhinishwa na nani na lengo lake ni nini? Kwa sababu sasa hivi tunajua *technology* imekua, fedha zinawekwa kwenye kakitu kadogo, kompyuta vitu vyote vinatoka, hilo ni la nini? Hapo kuna lengo la biashara. Tutapangisha au tutafanya nini? Sikupata jibu! Nikawafuata kwenye Kamati, Waziri akasema: "Unajua Benki ni *autonomy?"* Je, sisi tutakuwa na nafasi ya kuzungumza nao hapa? Kwenye Muswada huu ipo nafasi hiyo ya kwamba tutawaita waje hapa? Je, wakikataa kuja itakuwaje? Hiyo ni hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, ningependa kufahamu jinsi suala la Waziri na Gavana lilivyowekwa, maana imeandikwa kwamba watajadiliana. Nani ataita mwenzake hapa? Kwa jinsi lilivyowekwa, ninavyoona labda kwa kutokuelewa, Mheshimiwa Meghji hana mbavu za kumwita Gavana: "Njoo hapa nikueleze mambo haya." Hana mbavu hizo! Je, Serikali inaingiaje hapo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri tufikie kuwaamini watu wetu. Muamini Gavana, ni vizuri kumuamini kama wenzetu wanavyoamini, *of course* wana historia ndefu. Hatuhitaji kuwa na Mwenyekiti, lakini najiuliza kwa nini Mwenyekiti asiwepo? Sasa najiuliza, *here comes a judge, who can judge his own case?* Huyu Hakimu anayeamua kesi yake mwenyewe, inanipa tena utata!

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri ndugu zangu wajaribu kunifafanulia, kunipa mipaka hii ya uhuru inayopungua ni ipi. Ni kweli na ni vizuri wawe na uhuru wa kufanya mambo mbalimbali, lakini mimi bado haijaniingia kichwani. Hivi tunavyozungumza wananchi wanatusikiliza, kila mmoja anatusikiliza tunaloliamua, ni zuri sana, lakini twende kwa makini tuangalie. Nimemsikiliza Mheshimiwa Balozi amezungumza sana kwa uchungu na kwa nguvu. Nafikiri hapa tuna haja ya kufikiria mara mbili kabla hatujapitisha uamuzi.

Aidha, turekebishe vipengele ili viweze kufanya kazi vizuri kesho yake tusije tukaambiwa nyinyi mlicheza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nieleze kile kipengele wanachosema kuna *immunity in good faith.* Kwa namna gani? Ni mambo yapi ambayo yatakuwa *considered* katika hilo? Mtu anaweza akasema ilikuwa nia njema, lakini kishapoteza mabilioni ya fedha. Anaamua anasema kitu fulani kipitishwe na kinakubaliwa na Benki kinakwenda, kinafika kule mnasema: *"It was in good faith."* Kama wanasheria wanavyosema: "He *adhered in a law,* ingawa ameshamfunga. Alikosea ndani ya sheria, kwa hiyo yeye yuko salama mtu ameshakwenda. Nafikiri watueleze hapo wana maana gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo wenzangu wamelizungumzia na mimi nalizungumza ni kuhusu kilimo. Wenzetu wanasema kilimo ni *high risk,* kwa hiyo kukipa *priority,* ni tatizo kwamba inawezekana wakapata hasara. Lakini wenzetu wameanza kuwasaidia wakulima wao katika mazingira hayo na sasa hivi wakulima wakubwa wanakopeshwa. Mkulima wa kwetu ataendelea kuwa hivyo hivyo, atakuja Mzungu yeye atakopa kwa sababu ana fedha. *(Makofi)*

*Of course business* ni *risk*, usipokubali kuingia kwenye *risk* huwezi kufanya biashara, hilo ukubali kwamba *business is risk.* Sasa ndugu zangu mnaposema kilimo ni *high risk* wasipewe mikopo, wasifanye nini, wataendeleaje? Naomba Benki Kuu wasaidie mabenki au washauri iwekwe mikakati, kuna kitengo cha utafiti pale Benki Kuu waangalie ni wapi wanaweza kuingilia kumsaidia huyu mkulima ambaye analima kwa jembe la mkono aweze kutumia trekta, aweze kutumia miundombinu mizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo ni *high risk*, ni hivyo hivyo hata kwa wachimbaji. Suala la uchimbaji ni *high risk*, lakini kule ndiko nafikiri na kwenyewe mnaweza mkaingia. Hamjafanya utafiti wa kutosha kuhusu suala la wachimbaji. Kuna wachimbaji ambao wameshaweza kufikia mahali ambapo hawezi kuhama, hawezi kutoroka na wana mitaji mizuri, wanaweza wakafanya kazi. Wakishirikiana na mabenki wanafanya vizuri, lakini wanakwama kwa sababu Benki haiwezi kuwakopesha ila inawakopesha Wazungu wa nje. Wenyewe wakitoka nje kuja kukopa wanakubaliwa kwa sababu wanakuja na watu wao wanawapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimweleze Gavana kwamba, mwaka juzi, 2004 tulipokuwa kwenye Tume ya Madini, *paper* iliyoletwa na Benki Kuu kwa kweli haikutufurahisha. Ni katika *paper* ambazo zilionyesha watu walikaa wakasoma taarifa tu za migodini wakatoa *paper*! Hawakuweza kuangalia ni nini kinatakiwa kwa wananchi na wale wachimbaji wanafanya nini kule kwenye migodi mikubwa. Nendeni kule muangalie wananchi wa kawaida wanafanya nini na wachimbaji wakubwa wanafanya nini ndiyo mnaweza kupata taarifa. Kuna hivyo vitengo, watu wafanye kazi ili wachimbaji wawezeshwe. Kwa mfano, mchimbaji wa Rwamgasi kama leo akiwezeshwa yule anaweza kuajiri zaidi ya watu 10,000. Akina Ahmed wakiwezeshwa wanaweza kuajiri watu wengi, ndiyo *MKUKUTA* wenyewe. Sasa hawa tutawatoa lini? Tutaishia kumpa *GGM* uwezo kuliko kumpa Mtanzania! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwaomba hawa ndugu zetu wanisaidie katika hili la uhuru na mipaka yao ya uhuru wanataka iwe wapi, kwa sababu hakuna kitu duniani ambacho unaweza kusema ni uhuru wa moja kwa moja. Halafu wanieleze, uchumi wetu bado ni tegemezi, wao wanataka uhuru gani katika uchumi tegemezi? Watusaidie kuelewa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba majibu hayo niyapate kabla hili tukio halijapita. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniruhusu niweze kuchangia kwenye hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Lenin katika siku zake za mwisho wakati anaugua alijutia mateso yaliyokuwa yanampata akasema: *"What a poor way of dying, what a poor way of dying."* Alijutia aina ya kifo alichokuwa anakufa kwa sababu asingeweza kuchagua. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika hii *bill* hapa ni lazima niunge mkono hivi hivi. *Who am I to oppose a bill of this nature* kama wote mmekwishasema ndiyo? Lakini hata hivyo ni vizuri wale wenye msimamo fulani katika jambo fulani ni lazima tusimame na kuhesabiwa kwa sababu *history* itakuja kutuhukumu. Hiki chombo ni cha nani, hii *BOT*? Ni mali ya nani hii? Yaani haina Wizara! Haina mtu! Sisi ndiyo tumewekwa na wananchi wa nchi hii kwa kuchaguliwa, tunaunda vyombo ambavyo baadaye vinageuka kuwa *monsters* yaani tusiviguse. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani hapa Waheshimiwa Wabunge wanauliza swali la kimsingi. Uhuru gani unataka zaidi ya huu? Uhuru bila mipaka ni ghasia. Uhuru wowote ni lazima uwe na mipaka, sasa hii mipaka nani atasimamia? Hata majeshi tunasimamia, kila chombo tunasimamia, isipokuwa hiki chombo tunataka tusikisimamie! Sasa tusikisimamie chombo ambacho ni chetu, lakini kinashindwa kazi!

Mheshimiwa Naibu Spika, *inflation* sasa hivi imefikia nadhani asilimia saba na zaidi, leo inakaribia nane. Riba katika mabenki yetu haya hazisimamiwi wala hakuna anaye-*regulate.* Nchi za kibepari zimefanikiwa kujenga uchumi wa kibepari, uchumi

wa soko, lakini zina nguvu ya kusimamia *regulations* ambazo zimetunga. Kama huna uwezo huo ni kama umewaachia nyang'au tu kuendesha mambo yao. *(Kicheko)*

Kama huna uwezo wa kusimamia *regulation* za kusimamia *Private Sector* ni kazi ngumu sana kwa nchi maskini. Kusimamia uchumi wa *market economy* ambao ni *private* hatuna uwezo na ndiyo maana wanatupiga chenga, wanajificha na tunabaki tunalialia tu. Sasa na hiki chombo ambacho ndiyo nguzo ya uchumi, hiki ndiyo chombo kinachotakiwa kusimamia biashara katika nchi, sasa kinataka uhuru zaidi. Hizi riba ambazo zinakua wanavyotaka na mabenki yamejaa fedha na watu hawawezi kwenda kuzichukua, wanaoweza kwenda kuzichukua zile fedha kwa mfano *NBC* nadhani ni makampuni ya *South Africa* na Wahindi *(Social Service)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi vyombo vinakaa hapa kwa lengo la ku-*serve* nani? Kama hiki ni chombo cha Watanzania ni lazima kiwe na sura inayo-*reflect* watu wenye mali ile, vinginevyo hakuna sababu. Kama kwa sababu ya *pigment* hatuna uwezo, then ni kwa nini tulitafuta uhuru katika nchi hii? Tunaweza uhuru tu wa bendera isipokuwa hivi vingine hatuwezi? *Political independence without economic independence, is this possible?* Kwa nini tulitafuta uhuru? Kama ni hivyo hakuna haja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine wale watu wanaokuwa ndani ya chombo ndiyo wanaoamua sura ya chombo kile. Sasa hili ni gumu zaidi. Siyo lazima wawe weupe au Wazungu au weusi. Lakini nasema kwamba hiki ni chombo chetu na kwa bahati nzuri kwa sababu kazi zake ni nyeti kiko *highly insulated.* Kimefunikwa sana siyo *exposed* kama Waziri wa Fedha. Hiki kinakingwa, ndiyo maana inawezekana hawaelewi hata matatizo tunayopata sisi Wanasiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *CRDB* imeomba leseni kwa zaidi ya mwaka sasa majibu bado na hii ndiyo inayo-*support SACCOS* ambazo ndiyo benki za wananchi. Mwananchi wa kawaida anaijua *NBC?*

**MBUNGE FULANI:** Atathubutu?

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Au hii *Micro Bank* sijui nini *Bank Chartered.*

**MBUNGE FULANI:** *Standard Chartered.*

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Hizi ni benki za wafanyabiashara, hata mwakilishi anashindwa kuisema. *(Kicheko)*

Hizi ni za wakubwa, ni za watu waliopiga tai, wanaojua fedha. Huyu mtu wa shilingi elfu hamsini au laki mbili anaelewa hii benki? Kwa hiyo, benki hii ambayo ndiyo ikakopesha *SACCOS* ambazo ndiyo zinatupa *image* zinapata matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo la *lack of sensitivity to public demands. This is a disease.* Ni ugonjwa mkubwa sana na *usually* tabia hii kwa vyombo ambavyo ni

*insulated*, havionekani kwa umma ndiyo tabia yake. *Peasants,* robo tatu ya Watanzania hawajui jengo la *BoT* liko wapi. Mimi nimewahi kuingia labda mara mbili tu tangu niwe Mbunge. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, tusipoangalia mambo haya tunayoyafanya hapa kwa kweli tutakuja kuonekana ndiyo wasaliti. Mimi nasema hivi, sisi wa kuwajibika kwetu ni Zakia Meghji. Wewe kazi yako ni kusoma tu, kwamba unapewa taarifa ya mwisho usiwe unauliza mambo yanavyokwenda. Kwa nini asilete mwenyewe hapa! Umewekwa wewe kwa sababu ndiyo *politically accountable,* ndiyo watu wanakujua, ulikwenda kuomba ridhaa yao, ndiyo maana unawekwa hapa. Sasa hapa unapokuja kuwakilisha jambo ni kama kasuku tu. *(Kicheko)*

Samahani, yaani utakuwa unawakilisha kama kasuku kwa maana kwamba unaandikiwa wakasema: “Soma hapa” basi! Ukiulizwa kule, huyu anasema usiniingilie. Hii ni *disengagement* kwenye chombo cha watu, ni *alienation*, ni *refusal to obey.*

Waheshimiwa Wabunge, pale London pana mahali panaitwa nadhani *Ferguson square* ambapo ukiwa na dukuduku juu ya Serikali yako, basi unakwenda pale asubuhi unachukua na *breakfast* yako na chakula chako mpaka mchana unaingia pale au unangojea wenzako wa aina yako mnakwenda pale juu kwa zamu. Mtu anapiga kelele mpaka akichoka anatoka, halafu anaingia mwingine tena anakula chakula, hivyo hivyo mpaka jioni.

Inasemekana hata Hayati Kenyatta alipokwenda Uingereza alikuwa amekwenda kwa sababu ya kupinga *female circumcision,* lakini alipofika pale akakuta wenzake wanazungumzia mambo mengine wakamuuliza: “Wewe Kenyatta, kule si mna tozo la ardhi?” Akasema: “Ndiyo.” Wakamwambia: “Sema hilo.” Inawezekana alisema ndiyo, wakampangia mawazo siku nyingine naye akaingia pale kwenye lile jukwaa. Sasa pale ni kupumua, ni ku-*vent* matatizo yako halafu ukishamaliza jioni labda *pressure* inakuwa imepungua. Sisi hatuji hapa kupumua. *This is our country*, tunakuja kujenga nchi yetu. *This is our country* na tutafia hapa hapa. Tunaweza tukafia kwenye majela, lakini hatuwezi tukafukuzwa, tutakwenda wapi? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili nilidhani kwamba hili suala la kukosa *sensitivity* kwa mambo yanayotokea ni *reflection* kwamba chombo hiki kinahitaji mabadiliko. Kwanza *IMF* ingawa hatuwezi kusema hapa, masharti mengine inawezekana ndiyo hayo, sasa huna *choice* kwani nani anayetawala *IMF*?

**WABUNGE FULANI:** Wazungu.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Wazungu ndiyo, lakini ni nani? Marekani! Kwa hiyo, ndiyo inakuja sasa mpaka hapa na ndiyo mwisho tunakuwa hapa tunazungumza maneno tu hivi hivi. Sasa kama hukukubali maana yake ni kwamba watakunyima, kwa hiyo kubali. Sasa hii *independence* hii, *what a poor way of dying! (Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilidhani sisi hapa katika hili tukubaliane mambo yafuatayo: - Moja, ni lazima awe ana-*consult* Waziri wa Fedha kwa maamuzi yote yale makubwa. Ya pili, wale Magavana watatu wajiepushe na tabia ya kufanya maamuzi *in the name of* dharura, kwa sababu ukitaka kitu si uta-*create* tu. Unasubiri aondoke halafu unasema ilikuwa dharura. Kwa hiyo, wajiepushe na hayo ili wasije wakatumia Bodi kama ni *rubber stamp.* Ya tatu, kuwe na *regular* na *frequent reporting* ya Benki hii, vile vi-*pamphlet* ili kusudi sisi wote tuwe tunaona na tunapiga kelele. Sisi tunachoweza kufanya hapa ni kupiga kelele tu. *(Kicheko)*

Ya nne, haya mambo ya *SACCOS* ambayo ni nyeti na *urgent* sijui tutafanyaje maana hatumo. *SACCOS* zinakosa fedha na leseni hazitolewi kwa *CRDB* na *CRDB is the only Bank with a black face.* Sasa nayo hii inanyimwa! Huyu anayenyima fedha ni nani wakati *BoT* ni ya kwetu?

Ya tano, Benki hii kama inavyotakiwa i-*support SACCOS* kwa kweli ijihusishe na mahali pale ambapo ndiyo *source* ya nguvu yake, yaani ya wakulima. Ni kweli kilimo ni *risk*, sasa *option* ni ipi? Dhahabu ikiisha yote utakwenda wapi? Ndiyo maana ukitazama *transactions* zake inawezekana nyingi ziko kwenye biashara. Kwa nchi kama Tanzania nadhani hakuna mtu anayeelewa uchumi anaweza akaingia kwenye kilimo bila kuwa na *assurance* ya *support* kutoka kwenye mabenki au vyombo vya fedha, vinginevyo ndiyo maana wote hawataki kwenda kulima. Utakuwa mjinga wewe uka-*sink* hela yako kwenye kilimo wakati kwenye ukame kama huu hauwi *protected*.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku moja nilikuwa natoa hotuba pale Amerika, Muamerika mmoja akauliza: *"Who is the rum-pen proletariat?"* Nilisema *rum-pen proletariat* ni hawa kandambili wanaotembea tembea Mitaani. Aliponiuliza swali hilo nilishangaa kwamba hata Muamerika hajui! Lakini baadaye nikasema: "Nenda huko Mitaani utawakuta watu wa namna hiyo." Akasema: "Aaah na wewe je?" Nikasema: "Mimi ni *civilized* kidogo, *rum-pen proletariat* wa ngazi ya juu zaidi." *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani kuna *problem*, tunaweza kuwa tunafanana, mnazungumza lugha moja, lakini nadhani kuwa weusi siyo *passport* au *prove* kwamba sisi ndiyo Wazalendo zaidi. *I think we are facing a problem.* Mtu wa kumtetea mkulima katika nchi hii ni Benki. Hawa watu wetu wanalima kwa sababu ya utamaduni wao tu, kama wangefanya mahesabu ya kazi yao hii ya kulima na *risk* ambazo ziko *involved* katika kilimo kwa kweli hakungekuwa na kilimo katika nchi hii. Lakini ndiyo hawa wamelima mara ya kwanza mazao yamekauka, mara ya pili yamekauka, mwaka kesho wataendelea kulima tu! Hana *choice*, atafanya kazi gani nyingine!

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipatia nafasi hii. Naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kutokana na busara nyingi zilizotokea leo, nadhani ni vizuri mzitafakari halafu kesho kama nilivyosema tutakuwa na kipindi cha maswali, baada ya kipindi cha maswali kuna wenzetu walioomba tuwapigie kura kuhusiana na Taasisi ya Mbeya, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia, Chuo cha Mwalimu

Nyerere na *Commission* ya *University*. Kwa hiyo, tutafanya hiyo kazi kesho asubuhi baada ya maswali.

Tutaahirisha Kikao cha kesho kusudi mchana saa kumi tuweze kushiriki mazungumzo ya Rais na Wazee wa Dodoma, Kilimani na Mlimani *Club* kule juu. Kwa wale ambao hawana usafiri wao magari yatatoka hapa saa tisa. Pengine kwa sababu ya *fence* ndogo ya ku-*pack* magari kule, watu wakienda kwa mabasi itakuwa vizuri zaidi kuliko na magari. Kwa hiyo, kesho asubuhi tutakuwa na shughuli za namna hiyo.

Tutaendelea siku ya Jumatatu na Muswada huu. Nategemea kipindi cha asubuhi Wabunge waliobakia kuchangia watachangia halafu wataitwa Manaibu Waziri, halafu Waziri mwenyewe, nadhani ata-*conclude*. Jioni ama siku inayofuatia tutaingia ule Muswada mwingine wa fedha.

Baada ya kusema hayo naomba niahirishe Kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.29 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa Tarehe 31 Machi, 2006 saa tatu Asubuhi)*